Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Saba - Tarehe 21 Aprili, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Utalii Tanzania kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2002, *(The Report of Audited Accounts of the Tanzania Tourist Board for the Year ended 30th June, 2002).*

Taarifa ya Mwaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* kwa Mwaka 2002/2003, *(The Annual Report of Tanzania National Parks (TANAPA) for the Year 2002/2003).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Shirika la Makumbusho ya Taifa kwa Mwaka 2002/2003, *(The Annual Report and Audited Accounts of the National Museum of Tanzania for the Year 2002/2003)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 88

**Majukumu ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya**

**MHE. MUSA A. LUPATU** aliuliza:-

Kwa kuwa katika mjadala juu ya Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge suala la majukumu ya Wakuu

wa Mikoa na Wilaya lilichukua nafasi kubwa katika mjadala kutokana na watu wengi kutofahamu vizuri majukumu makubwa waliyo nayo viongozi hao:-

(a) Je, ni yapi majukumu ya viongozi hao?

(b) Kwa kuwa katika Muundo wa Vikao vya Mikoa, iko Kamati ya Ushauri ya Mkoa, lakini Wilaya haina Kamati kama hiyo, je, Mkuu wa Wilaya anapata ushauri kutoka wapi?

(c) Kwa kuwa Mkuu wa Wilaya anawakilishwa na Katibu Tarafa katika ngazi ya Tarafa, je, katika ngazi ya Kata anawakilishwa na nani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Musa Lupatu, Mbunge wa Korogwe Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, yameainishwa kwenye Sheria ya Tawala za Mikoa Namba 19 ya mwaka 1997. Chini ya Sheria hiyo, majukumu ya viongozi hawa yamefafanuliwa katika Kifungu cha 5,6 na 14(1),(2) na (3).

Aidha, nyongeza C na F ya Waraka wa Utumishi Na.1 wa mwaka 1998 zinaelezea kwa uwazi zaidi majukumu ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Nyongeza C imetaja majukumu 19 ya Wakuu wa Mikoa na Nyongeza F inataja majukumu 9 ya Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya majukumu hayo ni pamoja na kusimamia masuala ya ulinzi na amani katika maeneo yao, kusimamia na kuratibu shughuli zote za maendeleo katika Mkoa au Wilaya, kutoa ushauri wa kitaalam kwa Halmashauri ili ziweze kutoa huduma bora kwa wananchi, kutoa tafsiri na mwelekeo wa utekelezaji wa Sera za Serikali, kuziwezesha Halmashauri kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kuhakikisha kuwepo kwa mazingira mazuri ya kuweza kufanya hivyo na kutekeleza majukumu mengine yote watakayopewa na Sheria mahsusi au watakayokasimiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Mikoa ni wawakilishi wa Rais na Wakuu wa Wilaya ni Wasaidizi Wakuu wa Wakuu wa Mikoa.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19/1997 iliweka muundo wa vikao katika ngazi ya Mkoa ambavyo ni Kamati ya Ushauri wa Mkoa *(RCC)* lakini katika ngazi ya Wilaya Kamati hizo hazipo. Kasoro hii ilisababisha Mkuu wa Wilaya ashindwe kupata ushauri na pia taarifa za Mipango ya Maendeleo ya Wilaya kutoka kwa wataalam waliopo kwenye Wilaya. Kwa

kulitambua tatizo hili, suala la kuwepo Kamati za Ushauri za Wilaya liliingizwa kwenye Waraka wa Baraza la Mawaziri wa Kuboresha utendaji kazi wa Sekretarieti za Mikoa ulioandaliwa na TAMISEMI na kuwasilishwa katika Baraza hilo. Baada ya Waraka huo kujadiliwa, Baraza liliagiza kwamba Kamati za Ushauri za Wilaya zianzishwe.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako kuwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanakamilisha marekebisho ya Sheria ya Tawala za Mikoa Na.19/1997 ili masuala mbalimbali yaweze kuzingatiwa.

(c) Kimuundo Serikali Kuu inashia ngazi ya Tarafa ambapo Katibu Tarafa anamwakilisha Mkuu wa Wilaya katika ngazi hiyo. Hata hivyo, kufuatia kutambua umuhimu wa Katibu Tarafa katika kusukuma maendeleo na ili kumwezesha kushiriki kikamilifu katika harakati hizo, Serikali ilitoa mwongozo wa uwajibikaji wa Makatibu Tarafa katika Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa uliotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa barua yake ya tarehe 8 Desemba, 2003. Kulingana na Mwongozo huo, Makatibu Tarafa watawawakilisha Wakuu wa Wilaya kwenye ngazi ya Kata kwa kuwa watawajibika kushiriki na kutoa ushauri kuhusu upangaji wa mipango ya maendeleo katika eneo la Tarafa anayosimamia. Pia watawajibika kuratibu na kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika maeneo yao kama zitakavyopokelewa kutoka kwa watendaji wa Kata na kuziwasilisha kwa Mkurugenzi Mtendaji na Mkuu wa Wilaya/Katibu Tawala wa Wilaya inayohusika.

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa hivi sasa Makatibu Tarafa wanayo majukumu makubwa kama alivyoyataja, je, Serikali haioni kwamba ingekuwa jambo la busara kuwaongezea kidogo marupurupu ili waweze kufanya kazi zao vizuri? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, suala la kuongezewa marupurupu Makatibu Tarafa ni wazo zuri lakini ni jambo ambalo litazingatiwa na Idara Kuu ya Utumishi katika kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma kwa ujumla.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake lakini kwa kuwa amesema kuwa mojawapo ya kazi ya Wakuu wa Wilaya pamoja na Makatibu Tarafa ni pamoja na kusimamia na kuratibu maendeleo na kwa kuwa kwa sheria nyingine kazi hizo pia ni kazi za Wakurugenzi wa Wilaya na kwa kuwa kumetokea mgongano kutokana na mwingiliano wa kazi hizo, je, sasa ni lini Serikali italeta sheria ya kuondoa mgongano huo na kuhakikisha kwamba kazi za maendeleo ziko chini ya mtiririko wa kiongozi mmoja na kuondoa migongano ambayo inajitokeza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimhakikishie Dr. Slaa kwamba kwa kweli hatuna taarifa za migongano kati ya Halmashauri na Wakuu wa Wilaya ukiondoa matatizo ya hapa na pale yanayojitokeza *including* pale Karatu kwa Dr. Willbrod Slaa. *That is a very unique case* na tusiichanganye na mambo mengine.

Lakini kama nilivyosema, tunakamilisha mapendekezo ya kuboresha sheria ile ya mwaka 1997 na tunadhani kwa kiasi kikubwa itazingatia mambo mengi ambayo yatawasaidia Wakuu wa Wilaya kufanya kazi vizuri zaidi.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inatambua kuwa Makatibu Tarafa ni sehemu muhimu ya kuhimiza maendeleo ya wananchi vijijini na kwa kuwa hakuna vikao ambavyo viko kisheria vya kuwasaidia Makatibu Tarafa kusukuma shughuli hizo za kimaendeleo na kuwaunganisha kwa utaratibu mzuri wao na Watendaji wa Kata, je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuleta sheria ya kuwawezesha Makatibu Tarafa kuwa na vikao halali au vya kisheria katika Tarafa na Kata? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ndio maana katika maelezo nimeeleza wazi kabisa kwamba upungufu huo ulikwishabainika na tulichofanya katika hatua ya awali kwanza tumetoa mwongozo *(Administrative Arrangement)* ya namna ya kufanya huyu Katibu Tarafa aweze kuwa *effective* katika ngazi ya Kata na awe ni kiungo kati ya Mkurugenzi Mtendaji na maeneo ya ngazi ya chini.

Mheshimiwa Spika, lakini sheria hiyo nyingine tunayoizungumzia itakapokuwa inafanyiwa marekebisho nayo tunaamini tutaingiza utaratibu ambao ni wa kisheria zaidi kuweza kumweka katika hali ambayo ni ya kisheria kuliko ilivyo sasa.

Na. 89

**Kuthibitisha Kata Mpya**

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kata za Ulaya Wilayani Kilosa, Kidodi, Mabwerebwere na Masanze zimekwishakaa na kugawa Kata mpya katika Kata hizo; na kwa kuwa kichama zimekwishatambulika tangu mwaka 2000 zimepata hadhi ya Kata na Chama kinachotawala (CCM)(W) kupata uongozi:-

(a) Je, ni lini Serikali itazithibitisha Kata hizo za Ruaha, Mhanda, Dodoma Issange na Tindiga ambazo tayari vikao vya Kata husika vimeshafanyika na kupeleka mapendekezo hayo Wilayani?

(b) Kwa kuchelewa kugawa maeneo hayo wakati vigezo vyote na sifa zote zipo kunachelewesha kusogeza madaraka karibu na wananchi, je, Serikali haioni kwamba inachelewesha maendeleo ya Kata hizo hasa kwa kuzingatia ukubwa wa eneo na wingi wa watu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christopher Wegga, Mbunge wa Jimbo la Mikumi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ina uwezo wa kugawa au kupendekeza Kata baada ya kutimiza vigezo na sifa zinazohusika na mapendekezo hayo kuthibitishwa na Kamati ya Ushauri ya Mkoa. Halmashauri na Mkoa itawasilisha maombi ya mapendekezo ya Kata pamoja na muhtasari ya vikao husika kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Ofisi yangu itachambua maombi hayo na kutoa ushauri wa kukubali au kukataa maombi hayo. Halmashauri itaarifiwa kama ombi limekubaliwa au la. Ofisi yangu imepokea barua toka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro ya tarehe 30 Desemba, 2003 ikielezea mapendekezo ya Kata mpya za Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa bila kuambatanisha muhtasari ya vikao husika.

Katika kufuatilia suala hili ndani ya Ofisi yangu tumeweza kupata muhtasari Na. 3/2003 wa mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 28 Agosti, 2003 ambao unahusu mapendekezo haya lakini bado tunahitaji kupata muhtasari kutoka kwenye kikao cha *RCC.* Kwa hiyo, tunaomba tushirikiane na Mheshimiwa Mbunge tuweze kukamilisha kazi hiyo na hatimaye Ofisi yetu iweze kuona lipi linakubalika na lipi linakataliwa.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa lengo la kugawa Kata ni kusaidia kuharakisha maendeleo kwa wananchi kwa kusogeza karibu wataalam wa ushauri na utawala kwa jumla. Kutokana na msingi huo, Serikali imekuwa ikigawa Kata kila mara Halmashauri za Wilaya na Mikoa zinapotoa mapendekezo kwa kuzingatia maelekezo mbalimbali yanayotolewa. Kwa upande wa Kata hizi alizozitaja za Kidodi, Mabwerebwere na Masanze tatizo limekuwa ni kuchelewa kuwasilisha kumbukumbu muhimu ndiko kumesababisha hatua za haraka kutokamilika. Nina hakika tukishakamilisha hayo, huenda basi baadhi ya mambo tukayakubali pengine mengine tusiyakubali.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

(a) Kutokana na majibu mazuri niliyopata kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, je, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba Kata hizo na Kata nyingine Tanzania nzima zinahitaji usafiri kwa Makatibu Kata kwa sababu katika

Tanzania Makatibu Kata hawana usafiri wowote ule wakati ikifikiriafikiria namna ya kuzipitisha hizi, huenda zikapitishwa atakubali kuzipa pikipiki?

(b) Nimwombe basi kwa sababu ngazi zote hizo zinazochelewa kumpa taarifa zipo mikononi mwake yuko tayari kuhimiza uongozi wa Mkoa na Wilaya walete taarifa mapema ili tuweze kupata maamuzi haraka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nina hakika itakuwa ni ulimi uliteleza tu hawa tunaowazungumzia sio Makatibu Kata ni Watendaji wa Kata. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ndiyo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Lakini hoja yenyewe ya msingi juu ya usafiri kwa ajili ya Watendaji wa Kata ni kweli wanahitaji usafiri na sisi tunaliona na tunalikubali na baadhi ya Halmashauri wamejaribu kutumia njia zao wenyewe kutokana na mapato yao kuwawezesha Watendaji hawa kuwa na vyombo vya usafiri hata kama sio pikipiki lakini angalau baiskeli. Kwa sasa sio rahisi kusema jambo hili linawezekana tumehangaika sana kupata usafiri kwa ajili ya Makatibu Tarafa na imetugharimu fedha nyingi na watendaji hawa ni wengi zaidi ya 3,000 suala la pikipiki kwa kweli litahitaji mkakati mzuri na wa namna ya pekee ili tuweze kulifanikisha lakini hoja tunaielewa tatizo ni pesa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuhimiza Mkoa kuleta kumbukumbu muhimu, Mheshimiwa Christopher Wegga, nimesema sisi tumeshaingilia kati suala hili lakini na wewe basi tusaidie maana na wewe una kauli vile vile na Mkoa ili kazi hiyo iende haraka.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika taratibu alizozieleza Mheshimiwa Naibu Waziri, Manispaa ya Morogoro pia ina mgawanyo wa Kata zake na ukizingatia kwamba sasa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unakaribia, je, anayo maelezo yoyote ya Kata sita ambazo zimeongezwa kwenye Manispaa ya Morogoro ili ziweze kuanza shughuli mapema? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe wito wa jumla kuhusiana na suala hili la Kata maana najua tunaenda kwenye kipindi cha uchaguzi mwaka kesho na kwa hiyo pengine *pressure* ya Kata itakuwepo.

Tunachoweza kuwaomba Waheshimiwa Wabunge ni kwamba tulishatoa maelekezo kwenye Halmashauri zote kufanya kazi ya kuandaa mapendekezo kwa ajili ya kuwasilisha Ofisini kwetu. Vile vile tulishakubaliana tarehe 31 Mei, 2004 itakuwa ndio mwisho kabisa wa kupokea mawazo haya.

Sasa ni jambo linalotugusa wote, nadhani kila Mbunge ajaribu kuona na kujiridhisha. Tayari tumeshapata baadhi ya mapendekezo na tumeshaanza kuyafanyia kazi. Kubwa ni sisi wote tu-*check* na sisi tutaendelea kufuatilia kwa karibu.

Na. 90

**Uchumi wa Soko na Taasisi za Kulinda Walaji**

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU** aliuliza:-

Kwa kuwa kote duniani nchi zilizotangaza uchumi wa soko kama ilivyo hapa kwetu zimefanikiwa kukuza uchumi wao kwa kuunda vyombo au taasisi za udhibiti zilizothabiti kuwalinda walaji kama walivyofanya wenzetu wa Marekani, Japan na nchi za Ulaya; na kwa kuwa sera ya Uchumi wa Soko imeruhusiwa hapa nchini tangu mwaka 1984:-

(a) Je, ni mashirika/vyombo vingapi kwa majina vya udhibiti *(Regulatory)* vimeanzishwa hapa nchini hadi sasa?

(b) Je, ni sababu zipi zinazofanya ugumu wa uanzishaji wa vyombo vya *SUMATRA, EWURA* wakati sheria za kuruhusu kuundwa kwa vyombo hivyo zilishatungwa miaka mitatu iliyopita?

(c) Je, Serikali inasema nini kuhusu kupanda kwa bei ya mafuta kwa kiwango cha kuhatarisha uchumi wa nchi na Serikali imekaa kimya kama vile haijui madhara ya kupanda ovyo kwa bei ya mafuta kwa uchumi wa nchi yetu; na je, Serikali inatoa tamko gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, napenda kutoa utangulizi kuhusu usimamizi wa uchumi wa soko na taasisi za kulinda walaji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imefanya marekebisho makubwa ya mfumo wetu wa uchumi kwa kupitisha Sera ya Ushindani na Udhibiti wa Sekta za Huduma na Miundombinu ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, sera hii inatambua kwamba, ili kuleta ufanisi katika uchumi, nguvu ya soko ndiyo itakuwa kigezo muhimu katika kufikia maamuzi ya kiuchumi. Lakini kuwa na uchumi wa soko *(Market Economy)* hakuna maana ya kuwa na soko vurugu, inabidi sheria na taratibu za kulinda maslahi ya nchi kwa ujumla na maslahi ya mlaji zifuatwe lakini kwa namna ambayo itaweka pia mazingira mazuri ya kuwekeza katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo huo, Serikali imeruhusu ushindani kuwa ndiyo Mdhibiti Mkuu wa sehemu kubwa ya uchumi na biashara katika nchi yetu. Lakini pale ambapo ushindani hauwezi kuwepo kwa sababu ya ukiritimba asilia na hivyo kuwepo wawekezaji wanaoweza kutumia nafasi yao kutoza bei ya juu, kutoa huduma duni na kunyanyasa wateja, mfumo wa udhibiti wa kiutawala *(Administrative Regulation)* utakuwepo kwa lengo la kumlinda mlaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Bunge limekwishapitisha sheria za kuanzisha vyombo sita vya udhibiti. Vyombo hivyo, pamoja na maeneo vitakayoyashughulikia ni kama ifuatavyo:-

(i) Kamisheni ya Ushindani wa Haki itakayohakikisha kuwa zile sehemu za uchumi zenye ushindani, zinajiendesha kwa ushindani wa haki ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa wafanyabiashara hawafanyi njama kupanga bei, kubagua walaji, kutumia vibaya nguvu ya soko kuzuia wengine wasiingie kwenye biashara na kudanganya wateja.

(ii) Mamlaka ya Kudhibiti Huduma za Nishati na Maji itakayodhibiti sekta za maji, umeme, gesi na petroli.

(iii) Mamlaka ya Kudhibiti Usafiri wa Barabara, Maji, Reli na Bandari.

(iv) Mamlaka ya Tanzania ya Kudhibiti Mawasiliano itakayodhibiti maeneo ya simu, posta, masafa, utangazaji na mawasiliano ya habari.

(v) Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania itakayodhibiti usafiri wa anga, viwanja vya ndege pamoja na uongozaji wa ndege.

(vi) Mahakama Maalum ya Kushughulikia Ushindani wa Haki. Hii ni Mahakama maalum itakayoshughulikia masuala yatakayotokana na maamuzi ya mamlaka tano nilizozitaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, mamlaka hizi za udhibiti zimepewa uwezo wa kusimamia masuala ya uchumi, usalama na ubora wa bidhaa katika sekta husika. Hata hivyo, maeneo ambayo yana ushindani hayataguswa na udhibiti wa kiuchumi katika kupanga bei.

(b) Mheshimiwa Spika, mfumo huu mpya wa kuangalia uchumi wa soko unahitaji maandalizi mazuri na rasilimali nyingi katika kuanzisha. Vyombo vya *EWURA* na *SUMATRA* havijaanzishwa kutokana na kutokamilishwa kwa taratibu mbalimbali za kusimamia uendeshaji wa vyombo hivi ili kuondoa migongano ambayo ingejitokeza katika utekelezaji wa mamlaka hizi.

Mheshimiwa Spika, matayarisho ya kuanzisha mamlaka zote nilizozitaja kwenye sehemu yanaendelea vizuri ikiwa ni pamoja na kuteua na kupitia mapendekezo ya wataalam waelekezi wanaosaidia kuhakikisha kuwa mamlaka zitakazoanzishwa zitazingatia misingi ya kisasa ya udhibiti.

(c) Mheshimiwa Spika, bei za mafuta zinaendelea kupanda kutokana na hali ya vita na machafuko hasa katika maeneo yanakozalishwa mafuta hayo na ambako ndipo tunakonunua. Kwa bahati mbaya Tanzania kama nchi nyingine hatujazalisha mafuta na hivyo tunapokea tu bei kama walaji *(price takers).* Pamoja na hali hii, shughuli za udhibiti kupitia *EWURA* zitahakikisha kuangalia usalama na ubora wa mafuta na kuwazuia wafanyabiashara kuungana kwa lengo la kupanga bei za mafuta zisizohimilika.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, athari ya msingi kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri na athari kubwa katika uchumi wa soko ni ujenzi wa tabaka kati ya maskini na matajiri, hivi Serikali inajua leo kupanda kwa bei ya vifaa vya kawaida vya matumizi ya wananchi kwa mfano sukari imepanda kutoka shilingi 600 kwenda shilingi 800, unga wa ngano kutoka shilingi 300 kwenda shilingi 500, bomba ya kutolea maji machafu limepanda kutoka shilingi 7,000 kwenda shilingi 12,000 hiyo inatokana na kwamba hakuna udhibiti wa kutosha, je, Serikali inasema nini katika hali hii ambayo inawakabili wananchi wetu? *(Makofi)*

(b) Kutokana na udhibiti ambao hauridhishi katika eneo la mafuta ambapo mafuta ndio kichocheo muhimu cha kuyumbisha uchumi, je, Serikali inaonaje kama *TPDC* ambayo ndio ilikuwa inasimamia usambazaji na uingizaji mafuta hapa nchini ikapewa jukumu la kuendelea kudhibiti mpaka hapo uwezo wa nchi utakapokuwepo ili nchi isiyumbe sana kiuchumi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kama hakutakuwepo na udhibiti hasa ule unaoangalia kupanda holela kwa bei za bidhaa muhimu itakuwa ni njia mojawapo ya kuathiri wananchi hasa wale wenye kipato cha chini. Kwa mantiki hiyo, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi chombo tulichokiunda ni Kamisheni ya Ushindani wa Haki *(Fair Trade Practices)* ambapo kilipitishwa na Bunge hili. Nina hakika baada ya kuimarika kwa chombo hicho, upandaji wa bei holela wa bidhaa hizi hususani zile muhimu kwa wananchi wenye kipato cha chini hautaendelea, utadhibitiwa na hivyo kufanya bei zote ziwe sawasawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la upandaji wa bei za mafuta, ni kweli kabisa kwamba mafuta ni kichocheo cha uchumi wetu na kwa sababu ni kichocheo cha uchumi wetu, kupanda kwa bei ya mafuta holela vile vile kunaathiri sio sekta ya usafirishaji tu lakini sekta nyingi za uzalishaji katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kitu tunachokifanya sasa hivi kwa sababu tumeanzisha utaratibu wa soko huria katika sekta ya mafuta bado chombo hiki hiki cha *Fair Trade Practices* kitaangalia kuhakikisha kwamba bei hizo zinahimilika na watumiaji wa mafuta hayo.

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina swali moja la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa Bunge lako Tukufu linaletewa Miswada hapa ikiwa na nia kwamba ipitishwe Bungeni na iwe sheria kwa ajili ya kutumika sasa yapata miaka mitatu imepata tumepitisha sheria kwa ajili ya kuanzisha hizi *Regulatory Board,* Mheshimiwa Waziri anatuahidi ni lini sheria hii itaanza kutumika iwapo miaka mitatu imepata mpaka leo hii haijaanza kutumika? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, tumefanya marekebisho makubwa katika uchumi wetu na marekebisho hayo vile vile yanaendana na uanzishaji wa taasisi mpya lakini vile vile na kurekebisha taasisi nyingine ili kuendana na mfumo wa uchumi uliopo. Ni kweli kabisa kwamba tumeanzisha vyombo hivi kwa muda wa miaka mitatu iliyopita lakini vyombo hivi kuanzishwa kwake vinahitaji raslimali nyingi hasa raslimali fedha.

Lakini vile vile tunataka kuhakikisha kwamba vyombo hivi tukivianzisha vinafanya kazi vizuri zaidi hususan ya kuondoa migongano kati ya sekta ambazo zinasimamia maeneo hayo na uchumi kwa jumla kwa sababu ukiviweka vyombo hivi chini ya sekta ya maji tunataka kuhakikisha kwamba maji kama mdhibiti vile vile inaendelea kufanya vizuri isiwe maji ikawa ndio hakimu na mtoa kosa la chombo hicho kilichokosea.

Mhehsimiwa Spika, kwa hiyo, uko utaratibu wa kuona kwamba tunaviratibu vyombo hivi na vikishaanza kazi vinaanza kazi vizuri.

Na.91

**Mafao ya Mtumishi Aliyejinyonga**

**MHE. EDSON M. HALINGA** aliuliza:-

Kwa kuwa mtumishi akijinyonga familia yake haipati mirathi yoyote kwa mujibu wa *Pension Ordinance (Cap.375)* na *Public Service Retirement Benefit Act No.2/99:-*

(a) Je, Serikali haioni kuwa inawanyima haki wategemezi wa marehemu kwani wao hawahusiki?

(b) Kwa kuwa Serikali inashauri wahusika wamwandikie Rais ili aweze kuruhusu mafao hayo yatolewe, je, utaratibu huo si usumbufu zaidi kwa wafiwa?

(c) Je, Serikali iko tayari kuifuta sheria hiyo kwa sasa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edson Halinga, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Sheria ya *The Pension Ordinance (Cap.375)* ilifutwa na Sheria mpya ya sasa ya *The Public Service Retirement Benefit Act* Na.2 ya mwaka 1999. Kwa kuwa Sheria ya *Pension Ordinance* haipo, ningependa kujibu swali la msingi la Mheshimiwa Mbunge kulingana na sheria ya sasa ya pensheni yaani *Public Service Retirement Benefit Act* ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, sheria ya sasa ya pensheni haizungumzii chochote kuhusu kuwanyima mirathi ndugu wa marehemu ambaye amefariki kwa kujinyonga. Mirathi hulipwa kwa wategemezi wa marehemu baada ya kufuata taratibu za ufunguzi na usimamizi wa mirathi. Aidha, sheria haizungumzii chochote kuhusu uhusiano wa chanzo cha kifo cha mtumishi na malipo ya mafao kwa wategemezi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 27 cha Sheria ya sasa kinatoa ruhusa kwa Watumishi wa Umma peke yake na siyo wategemezi, kuomba msamaha wa Rais ili alegeze masharti yanayoweza kuwazuia wasipate mafao ya pensheni au kiinua mgongo kwa mujibu wa masharti ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imebainika kwamba sheria hii haikatazi malipo ya mirathi kwa wategemezi ambao marehemu wao amefariki kwa kujinyonga, Serikali haioni kama ni muafaka kufuta sheria hiyo.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri pingamizi kidogo linalotokana na hilo.

Wapo watu ambao wamenyimwa na hasa Askari Polisi ambao walijinyonga na familia zao hazijalipwa mpaka sasa na nilipofuatilia nikaambiwa na kuonyeshwa kwamba sheria hizi ndizo zinazofanya wasilipwe. Je, yuko tayari kunihakikishia nikiwatuma wale watu waje watapewa malipo yao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kama ushahidi upo na mambo yote yanathibitika kwamba kweli walijinyonga na walikuwa watumishi wa umma na kama alivyosema ni Askari Polisi, basi wana haki ya kulipwa. Naomba tuonane na aniletee kumbukumbu zote watalipwa. *(Makofi)*

Na. 92

**Nafasi ya Rais wa Zanzibar**

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI (k.n.y. MHE. MUTTAMWEGWA B. MGAYWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa muundo wa Muungano wa Tanzania una Serikali mbili yaani Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar:-

(a) Je, katika muundo huo, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ana nafasi gani katika Serikali ya Muungano?

(b) Je, Rais huyo ana haki zipi anazostahili katika Serikali ya Muungano?

(c) Je, Rais huyo anapokuwa nje ya nchi anatambuliwa kama Kiongozi wa nchi na je, anastahili kukagua gwaride kama kiongozi Mkuu wa Serikali?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mbunge wa Mwibara, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni mmoja wa Viongozi Wakuu wa vyombo vyenye mamlaka ya utendaji katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo kwa mujibu wa Ibara ya 46(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mmoja wa Viongozi Wakuu katika Serikali ya Muungano ambaye anayo haki pamoja na wajibu wa kulinda, kuimarisha na kudumisha umoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kula kiapo kwa ajili hiyo.

(b) Akiwa mmoja wa Viongozi Wakuu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni mjumbe wa Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ana haki ya kuhudhuria na kushiriki vikao vyote vya chombo hicho chenye jukumu la kuchukua maamuzi muhimu katika uongozi wa nchi.

(c) Tanzania ni nchi moja yenye Serikali mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Mkuu wa Nchi na Kiongozi Mkuu wa Serikali ya Muungano na Amiri Jeshi Mkuu ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rais wa Zanzibar siyo Mkuu wa Nchi na anapokwenda nje ya nchi hatambuliwi kama Mkuu wa Nchi.

Mheshima Spika, Rais wa Zanzibar anapokuwa nje ya nchi itifaki ya mapokezi inategemea utaratibu wa nchi husika. Hivyo, anapokwenda kwenye nchi zenye itifaki inayoruhusu, Rais wa Zanzibar hupokelewa kwa kukagua gwaride kwa hadhi inayolingana na ile anayopewa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anapokuwa nje ya nchi.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kila Mtanzania anayo nia ya kuutunza na kuimarisha Muungano wetu na hasa katika mambo ya msingi ambayo yalikubaliwa wakati wa kuuunda Muungano huo na kwa kuwa katika mabadiliko ya 11 na 12 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaliiondosha nafasi ya moja kwa moja ya Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Je, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa niaba ya Waziri haoni ni wakati muafaka sasa kwa sababu mabadiliko ya Katiba yanakuja ikarudishwa nafasi ile iliyokuwepo ili kuutunza na kuimarisha Muungano wetu? *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, Serikali haikusudii kuleta mabadiliko katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ili kurejesha nafasi ya Makamu wa Rais kama ilivyokuwa huko nyuma.

Marekebisho ya 11 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano yaliyofanywa na Bunge lako Tukufu yalilenga katika kutambua hali ya sasa tuliyonayo ya mfumo wa Vyama Vingi na Katiba lazima iweze kutabiri mambo ambayo yanaweza kutokea. Unataka uhakikishe katika mfumo huo kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano na Makamu wake wanatokana na Chama kimoja na hiyo ndiyo ilikuwa mantiki ya mabadiliko hayo.

Nafasi ya Rais wa Zanzibar katika Muungano ipo na itaendelea kuwepo na ndiyo maana nimesema katika jibu la msingi kwamba Rais wa Zanzibar kwa wadhifa wake ni mjumbe wa moja kwa moja wa Baraza la Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pili ni miongoni mwa Viongozi Wakuu katika dola wenye jukumu la kulinda, kutetea na kuhifadhi Katiba ya Jamhuri ya Muungano ikiwa ni pamoja na Muungano wenyewe. *(Makofi)*

**MHE. USSI YAHAYA HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Baada ya kupata majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba kuna sababu za kuwekwa sawa jina la Rais wa Zanzibar, kwa sababu katika makabrasha mengi wanaandika Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hakuna Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuna Rais wa Zanzibar na kuna Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hiyo, ingekuwa vizuri kila panapotajwa Rais wa Zanzibar, atajwe Rais wa Zanzibar, si Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hiyo ni taarifa tu umeitoa haihitaji majibu.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwanasheria Mkuu kwa majibu mazuri aliyotoa. Lakini nilikuwa nataka kuuliza swali dogo tu.

Je, Serikali ina uhakika kuwa Watanzania wote wanaelewa hivyo alivyojibu suala hilo kama lilivyojibiwa na kama hawaelewi Serikali itachukua wajibu gani kuwaelimisha Watanzania?

**SPIKA:** Jibu hili ndilo linawaelimisha. *(Kicheko)*

Na. 93

**Mradi wa Umeme Mlalo**

**MHE. CHARLES H. KAGONJI** aliuliza:-

Kwa kuwa tangu Mradi wa Umeme wa Mlalo ukamilike mwaka 2000 hakuna tena usambazaji wowote wa umeme uliofanyika hata kwa vile Vijiji vilivyosahaulika wakati wa mradi huo na kwamba upo ushahidi wa kutosha kwamba Vijiji na maeneo mengi ya jirani zetu wamepatiwa umeme katika kipindi hicho.

(a) Je, katika hali ya namna hiyo, nitakosea nikisema kuwa usambazaji wa umeme Vijijini unafanyika kwa upendeleo, licha ya majibu ya mara kwa mara ya Serikali ya kujihami kwa kusema ukosefu wa fedha, wakati Vijiji na maeneo yaliyo mengi yanapatiwa umeme, fedha zinatoka wapi?

(b) Naomba kufahamishwa kwa uhakika kuwa je, ni mpango gani umeandaliwa wa kupeleka umeme Gologolo, Manolo, Rangwi, Sunga, Mtae, Mnazi na Mng’aro?

(c) Je, Vijiji vya Mlesa, Dule, Zaizo, Ngazi na Mhelo vilivyoachwa kwa makusudi wakati wa utekelezaji wa mradi nilioutaja tangu awali vitapatiwa lini umeme?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mradi wa kupeleka umeme katika baadhi ya maeneo Jimboni Mlalo ulifanyika chini ya mpango wa mradi wa kusambaza umeme maeneo ya Vijijini uliokuwa unaitwa *Power IV*. Mradi huu ulikuwa unahusisha ujenzi wa laini ya umeme kilovolti 33 yenye urefu wa kilometa 12, ujenzi wa laini ndogo za kusambaza umeme yenye urefu wa kilometa 12 na ufungaji wa transfoma 11 za kusambaza umeme. Vijiji vilivyohusika katika mradi huu kulingana na Bajeti iliyotengwa ni Mnadani, Viti, Malindi, Moa, Nyasa, Majulai, Mlalo Mjini na Misioni ambavyo vyote vya ujumla wake vilipatiwa umeme mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama iufatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haina upendeleo katika kusambaza umeme hususan kwa wananchi wake walio wengi ambao wanaishi Vijijini. Ukosefu wa fedha ya kutosha ndiyo kikwazo kikubwa katika kukidhi azma ya Serikali ya kusambaza umeme katika maeneo yaliyo mengi ya Vijijini kwa wakati muafaka.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali bado inafanya juhudi ya kutafuta fedha kwa ajili ya kupeleka umeme katika Vijiji vya Gologolo, Manolo, Rangwi, Sunga, Mtae, Mnazi na Mng'aro. Gharama ya kupeleka umeme katika Vijiji hivyo inakisiwa kuwa ni shilingi milioni 748. Vijiji hivi vitapatiwa umeme kadri ya upatikanaji wa fedha. Hivyo tunaomba Mheshimiwa Charles Kagonji, atupe ushirikiano wake katika kutafuta fedha kutoka kwa Wahisani au Wafadhili wa ndani na nje ya nchi ili maeneo yaliyotajwa yaweze kupatiwa umeme katika muda muafaka.

(c) Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Mlesa, Dule, Zaizo, Ngazi na Mhelo kama nilivyoeleza katika maelezo ya awali havikuwa miongoni mwa Vijiji vilivyolengwa katika mpango wa kuwekewa umeme chini ya mradi wa *Power IV* uliokamilika mwaka 2000. Mpango uliopo kwa sasa ni kwamba Kijiji cha Mlesa kimeombewa bajeti katika mwaka huu wa 2004 na kinatarajiwa kupata umeme mwaka 2005. Vijini vya Dule, Zaizo, Ngazi na Mhelo vitapatiwa umeme kadri ya upatikanaji wa fedha toka vyanzo vya ndani au nje ya nchi.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu ambayo sikuyafurahia sana ya Mheshimiwa Waziri, naomba kwanza nimfahamishe Mheshimiwa Waziri kwamba Vijiji nilivyovitaja vilikuwa kwenye mpango huo wa mradi wa kwenda Mlalo na ushahidi akiutaka upo na kama nikimletea ushahidi wa maandishi, je, atabadili kauli yake na kuchukua hatua?

Pili, sijui, ndiyo kwamba nasikia Waheshimiwa Wabunge wanatakiwa wasaidiane na *TANESCO* kutafuta wahisani wa kupeleka umeme au maendeleo kule kwao. Nilidhani Serikali hii iliyopewa madaraka na Watanzania ni juu yake kwa kushirikiana na Wabunge waliopo ili waweze kusaidia kuleta maendeleo ya wananchi. Je, sera zetu zimebadilika au kauli hizo ni bahati mbaya tu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kwamba tunatofautiana katika kutaja Vijiji ambavyo vimo ama havimo ndani ya Mradi wa *Power IV,* naomba baada ya kikao hiki tuonane naye ili kuangalia Vijiji hivyo na tuweze kulisahihisha.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba Serikali ishirikiane na Waheshimiwa Wabunge katika kutafuta wafadhili, kazi ya kuleta maendeleo hapa nchini ni yetu sote na sisi Serikalini tupo wangapi, wachache sana, kila Mbunge anaelewa Jimbo lake vizuri sana na Wabunge wengi tu wametusaidia sana naweza kutaja wawili watatu hapa ambao

tumeshirikiana nao katika kusukuma kuleta maendeleo hasa ya nishati katika Majimbo yao.

Kwa mfano, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, tulikaa naye, tukafuatilia, yeye anatusaidia kueleza matatizo yaliyopo katika Jimbo lake na sisi kama Serikali tunaelezea yale ambayo yanatuhusu sisi, kwa mfano kutia saini Mikataba na kuwahakikishia wale wawekezaji kwamba miradi hiyo kweli ipo katika mipango yetu ya kufikisha umeme sehemu hizo na tukapata umeme katika Jimbo la Ukerewe na kuna wengi ambao wamefanya hivyo. Wengi wenu tumekwenda kwa Mabalozi, tukatafuta fedha za mashule na kadhalika. Kwa hiyo, hili siyo jambo jipya au ni sera mpya. Tunaomba tushirikiane kwa sababu wote ni kazi yetu kuleta maendeleo katika Majimbo yetu.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tatizo alilolitaja Mheshimiwa Charles Kagonji katika Vijiji vya Gologolo na Manoro vinafanana kabisa kabisa na Vijiji vyangu vya Mulgha, Kijota na Ngimu ambako katika Kijiji cha Wali tumejenga sekondari ya wasichana kwa fedha za Wadachi yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni moja. Je, Waziri atakubaliana na mimi sasa muda umefika na aniambie ni lini wananchi wa Kijiji cha Kijota watapata umeme kwenye sekondari yao, Kijiji cha Ngimu watapata umeme kwenye sekondari ya Ngimu na Kijiji cha Mulgha watapata umeme katika sekondari ya wasichana ya Mulgha? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, sitakuwa na jibu la uhakika moja kwa moja hapa, itabidi Mheshimiwa Mbunge tuonane, tuwaone *TANESCO* watuambie mpango wao ukoje wa kupeleka umeme katika Vijiji hivyo ili shule hizo ziweze kupata umeme mapema iwezekanavyo.

Na. 94

**Ahadi za Kupeleka Umeme Wilaya Zote Nchini Ifikapo 2005**

**MHE. ROBERT K. MASHALA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikiahidi kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya zote nchini ambazo hazina umeme kabla ya mwaka 2005 na kwa kuwa bado mwaka mmoja tu muda wa ahadi hii uishe bila dalili za utekelezaji wa ahadi:-

(a) Je, Serikali haitakuwa imelidanganya Bunge kwa kuahidi uongo?

(b) Je, kama ahadi hii ni kweli ni Wilaya ngapi zimepatiwa umeme tangu mwaka 2001 hadi sasa?

(c) Je, kwa Wilaya ambazo bado hazijapata umeme nini mkakati wa Serikali wa kuzipatia umeme Wilaya hizi kabla ya mwaka 2005 kama ilivyoahidi?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Robert Kaji Mashala, Mbunge wa Bukombe lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali hapo awali ilikuwa ni kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya zote ifikapo mwaka 2005 kadri upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi hiyo ya umeme. Mara nyingi fedha za utekelezaji wa miradi ya umeme hupatikana kutokana na mapato ya ndani au wafadhili na wahisani kutoka nje ya nchi.

Ukosefu wa fedha na upatikanaji wa wafadhili kwa wakati muafaka imekuwa ndiyo kikwazo kikubwa katika utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme katika Makao Makuu ya Wilaya zote. Hivyo ahadi ya kukamilisha upelekaji wa umeme Makao ya Wilaya zote ifikapo mwaka 2005 haitakamilika. Serikali inaomba imtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kuwa haiwezi kutoa ahadi za uongo, ila ufinyu wa Bajeti ndiyo tatizo kubwa linalochangia kukwama kwa utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo kwa wananchi wake wote ikiwemo sekta ya umeme.

(b) Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2001 hadi sasa Serikali kwa kutumia mapato yake ya ndani imepeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya tano pamoja na vitongoji vyake ambazo ni Geita, Tandahimba, Sikonge, Igunga na Mbarali.

(c) Mheshumiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kuwa baadhi ya Wilaya zitapata umeme kabla ya mwaka 2005 na Wilaya hizo ni Biharamulo, Ngara, Ukerewe, Serengeti, Urambo na Rufiji. Wilaya zilizobaki zitapata umeme kadri ya upatikanaji wa fedha na Serikali imeweka mpango wa muda mrefu na matarajio kuwa ifikapo mwaka 2010 Wilaya zote zitakuwa zimepata umeme.

Aidha, Serikali iko katika hatua za mwisho za kuunda Wakala wa Nishati Vijijini na Mfuko wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Fund )* ambayo itasaidia kuongeza kasi ya kusambaza umeme Vijijini baada ya sekta binafsi kushiriki katika biashara ya umeme.

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nilitaka kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Je, kwa kuwa Serikali iliahidi kwamba ifikapo mwaka 2005 Wilaya ya Bukombe itapata umeme, naomba alithibitishie Bunge hili Mheshimiwa Waziri je, ahadi hizo hazikuwa za kweli?

La pili, katika mazungumzo yetu mimi na yeye, Mheshimiwa Waziri alisema kwamba mpango mahsusi umefikiwa wa kupeleka umeme Wilaya ya Bukombe kupitia wafadhili wetu pamoja na kampuni ya *KMTL* ya *Kahama Mining.* Je, ahadi hizo zilikuwa za kisiasa au za kweli? Naomba majibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nielezee jambo moja kuhusu umeme kwa wakati huu. Jana tulikaa kama Serikali nadhani hii ni

wazi sasa, kwamba tulipeleka maombi sisi Wizara ya Nishati na Madini kupatiwa fedha za kuweza kuhakikisha kwamba nchi hii haingiii kwenye mgawo wa umeme katika siku za mbeleni.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwanzo tu kwa sababu hiyo basi Waheshimiwa Wabunge ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Robert Mashala, naomba wakiona tunasita au tunachelewa kutekeleza ahadi ambazo tumetoa ni kwa sababu hiyo ya tatizo la fedha ambalo limetukabili kwa sababu ya ukame uliopo.

Sasa swali lake, je, Wilaya ya Bukombe itapata umeme mwaka 2005? Ni imani yangu kwamba jitihada zinazofanywa na *TANESCO* zitafikisha umeme wakati huo. Naamini kama hali ya fedha itakuwa nzuri tutafikisha umeme kama tulivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mazungumzo kati ya *Kahama Mining Company* na Serikali kuomba tusaidiane nao kufikisha umeme Bukombe yanaendelea na tunaamini kwamba yatasaidia kufikisha umeme maana sasa hivi wanajenga kituo tayari na watasambaza umeme baada ya hapo katika Wilaya hiyo ya Bukombe kabla ya 2005.

**SPIKA:** Tunajua kila mtu ana tatizo la umeme lakini tusubiri Bajeti. Lakini Mheshimiwa Waziri *Hansard* haitaandika siku za mbeleni tutaandika siku za usoni.

Na. 95

**Wawindaji Ambao Hawana Ushirikiano**

**MHE. PARSEKO V. KONE (k.n.y. MHE. LEKULE M. LAIZER)** aliuliza:-

Kwa kuwa wamiliki wa maeneo ya uwindaji (vitalu vya uwindaji) hawana ushirikiano na wananchi, hawatoi msaada kwa miradi ya maendeleo huku wakiwinda wanyama kila wakati:-

Kwa kuwa ni wananchi ambao wamepata hasara ya wanyama hao huku mwindaji anafaidika, je, kwa nini wananchi wasipewe utaratibu wa kumkataa mwindaji kama huyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ugawaji wa maeneo ya uwindaji wa kitalii hufanywa kwa kuzingatia ushauri wa Kamati Maalum iliyoundwa mwaka 1996. Muundo wa Kamati hii ya ushauri ulizingatia uwakilishi wa wataalam wa wanyamapori, wanasheria na wananchi kwa maana ya Wabunge. Vigezo muhimu katika ugawaji wa vitalu huzingatia vile vile mapitio ya utendaji wa kampuni husika katika viwango vya matumizi ya kitalu, uchangiaji wa miradi ya maendeleo ya jamii, uboreshaji wa miundombinu na kuchangia kazi za kudhibiti ujangili katika maeneo wanakowinda.

Mheshimiwa Spika, pamoja na michango hiyo ambayo hutolewa na kampuni za uwindaji wa kitalii kwa kufuata utaratibu wa kisheria, Serikali hutoa kiasi cha asilimia 25 ya mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii kwa Halmashauri za Wilaya zenye maeneo ya uwindaji wa kitalii. Fedha hizo hutumika katika kuboresha huduma za jamii kwenye maeneo ambako shughuli za uwindaji wa kitalii hufanyika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kampuni ya uwindaji wa kitalii zimekuwa zikitimiza masharti ikiwa ni pamoja na kuchangia shughuli za maendeleo ya wananchi kama zinavyotakiwa kisheria. Kampuni ambazo hushindwa kutimiza masharti hayo huchukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa kitalu.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2000/2001 hadi 2002/2003, michango ya kampuni za uwindaji wa kitalii ilikuwa shilingi 3,116,094,583.02. Aidha, katika kipindi hicho Halmashauri ya Wilaya ya Monduli ambayo hujumuisha Jimbo la Longido ilipata mgao wa jumla ya shilingi 151,032,360 kutokana na asilimia 25 ya mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika maelezo yangu ya awali, muundo wa Kamati ya Ushauri wa kugawa maeneo ya uwindaji umezingatia uwakilishi wa wananchi. Hata hivyo, kufuatia uamuzi wa Serikali wa kuanzisha maeneo ya Jumuiya ya Uhifadhi Wanyamapori *(Wildlife Management Areas - WMA)* eneo ambalo litakuwa litakapotengwa kuwa *WMA,* taratibu za kugawa eneo hilo kuwa kitalu zitazingatia kanuni zinazosimamia uanzishaji wa maeneo hayo *(Wildlife Management Areas Regulations, 2002).* Kanuni hizo zinatamka kuwepo kwa uwakilishi wa wananchi kutoka kwenye maeneo hayo katika Kamati ya Ushauri ya Kugawa Vitalu.

Mheshimiwa Spika, kanuni za maeneo ya Jumuiya ya Uhifadhi Wanyamapori zilizinduliwa rasmi na kuanza kutumika Januari, 2003 katika maeneo 16 ya majaribio likiwemo eneo la Pori Tengefu la Longido. Hivyo namwomba Mheshimiwa Lekule Laizer, aendelee kutoa ushirikiano katika kusimamia utekelezaji wa kanuni hizo pamoja na kutoa ushauri kwa lengo la kuboresha utekelezaji.

Aidha, Wizara yangu iko tayari kupokea taarifa kuhusu wawindaji wasiokuwa na ushirikiano pindi zitakapobainika. Napenda kutoa wito kwa makampuni yote yanayomiliki vitalu vya uwindaji hapa nchini kuwa yanalazimika kuchangia shughuli za maendeleo ya kijamii jirani na maeneo yao ya vitalu.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hawa wawindaji baadhi yao hawana ushirikano na wanakijiji kwa sababu wanajua hawana namna ya kuwasiliana nao wakati wa kupewa hivyo vitalu

vya uwindaji. Waziri ameeleza kwamba kuna Kamati inayojadili hizi leseni za uwindaji na kuna maeneo ya *WMA* yaliyoanzishwa ili wananchi wapate sehemu kubwa ya kuchangia katika kuwapendekeza ni nani wapewe maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, je, kwanza, Waziri anaweza kutueleza mafanikio ya maeneo hayo 16 yaliyoteuliwa kama majaribio ili iweze kuenezwa katika maeneo mengine?

Swali la pili, wakati tukisubiri utaratibu huu ufanikiwe ama ushindwe kufanikiwa Waziri atakubaliana nami kwamba ni vizuri hawa waombaji wa Vitalu vya uwindaji wakapeleka maombi kwanza katika maeneo yanayohusika ili watoe maoni yao na kupeleka mpaka Wizarani na kwenye hiyo Kamati inayogawa maeneo hayo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, katika maeneo haya 16 niliyoyataja ya majaribio ya *WMA* ni kutoa nafasi zaidi au usimamizi zaidi kwa wanavijiji. Kwa maana hiyo kwa siku za baadaye ni kwamba hawa wanavijiji ambao watahusika moja kwa moja na wale wawindaji wa kitalii.

Kwa hivi sasa kwa sababu jambo hili ni geni tunachofanya katika maeneo haya 16 ni kuhamasisha maeneo yale na tumeshaanza katika maeneo ya Longido na kuna maombi katika eneo la Loliondo pia ambalo karibuni tunafanya mikutano kwa ajili ya kuwahamasisha na kuwaelewesha viongozi pamoja na wanavijiji.

Kwa hiyo, programu hii tayari kama nilivyosema imeanza, hatuwezi tu kuanza moja kwa moja kwa sababu hawataelewa. Inawezekana ikawa viongozi wachache wakaelewa, halafu wanavijiji wenyewe wasielewi kukawa na matatizo. Kwa hiyo, tumeanza na programu ya uhamasishaji na hili ndilo ambalo linafanyika.

Mheshimiwa Spika, suala la kusema kwamba maombi haya yaende kwanza katika maeneo husika. Ni kwamba sheria yetu ya mwaka 1974 inatamka bayana utaratibu ambao unatumika.

Lakini niseme kwamba hivi sasa tuko mbioni katika kurekebisha Sheria hii ya 1974, na ninahakika kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi katika maeneo yao wamehusika na kutoa mawazo hayo. Kwa hiyo, tungoje mpaka wakati ambapo sheria hii tutaileta hapa Bungeni. Nina uhakika kwamba mawazo mengi yataweza kutolewa.

Na. 96

**Mipaka ya Hifadhi ya Lukwati**

**MHE. PAUL E. NTWINA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekamilisha ahadi yake ya kupokea Meneja Pori kule *Lukwati Game Reserve;* na kwa kuwa nyumba na ofisi zimeanza kujengwa:-

Je, ni lini sasa barabara na mipaka ya Hifadhi au Pori la Lukwati vitaanza kupimwa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge wa Songwe, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Pori la Wazi la Lukwati na Msitu wa Hifadhi wa Muipa yaliunganishwa na kutengwa kuwa Pori Tengefu mwaka 1974. Pori hilo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 3,146.7 lilipandishwa hadhi na kuwa Pori la Akiba kwa Tangazo la Serikali Na. 459 la tarehe 8 Agosti, 1997. Pori la Akiba la Lukwati lipo katika Wilaya ya Chunya Mkoani Mbeya. Pori hilo kwa kupande wa Kaskazini Magharibi limepakana na Pori la Akiba la Rukwa, upande wa Kusini Magharibi limepakana na Ziwa Rukwa na upande wa Kusini Mashariki limepakana na vijiji vya Gua, Ngwala na Piti na upande wa Kaskazini - Mashariki limepakana na Pori la Wazi la Piti.

Wizara yangu inaandaa Mpango wa Usimamizi *(General Management Plan)* wa Pori la Akiba Lukwati ambao upo katika hatua za mwisho za maandalizi. Mwezi Oktoba, 2003 Wizara yangu ilipeleka watumishi katika kituo cha Ngwala kwa ajili ya usimamizi wa Pori hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya msingi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 Wizara yangu imepanga kufyeka na kuweka alama za mpaka *(beacon)* katika pori la akiba la Lukwati.

Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa katika Pori la akiba Lukwati hakuna barabara za kudumu kwa hivi sasa. Aidha, njia zinazotumika na wawindaji wa kitalii *(Tracks)* hutumiwa pia katika shughuli za usimamizi wa pori hilo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara yangu inaandaa mpango wa kufungua na kutengeneza barabara kutoka:-

(i) Kambi ya Rungwa kupitia Mto Mwipa hadi Kijiji cha Ngwala, yenye urefu wa kilometa 140.

(ii) Kambi ya Wuku kwenda kambi ya Rungwa yenye urefu wa kilometa 60.

(iii) Kambi ya Wuku kwenda kijiji cha Gua yenye urefu wa kilometa 50.

(iv) Kambi ya Wuku kuelekea Ziwani Kasisi na baadaye kuelekea Kambi ya Mtakuja umbali wa kilometa 70.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo niliyoyatoa, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge wa Songwe, kwamba Wizara yangu iko tayari kupokea na kusikiliza ushauri utakaotolewa wenye lengo la kuboresha usimamizi wa Pori la Akiba la Lukwati. Nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Paul Ntwina, kwa jitihada za kufuatilia kwa karibu uanzishaji, usimamizi na uendeshaji wa Pori la Akiba la Lukwati.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pia napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kukamilisha ahadi yake kupitia kwa Mheshimiwa Waziri .

Kwa kuwa wananchi wa vijiji vinavyopakana na Pori la Wazi la Lukwati vijiji vya Ngwala, Gua Kaparara, Kininga, Udide, Some na Rukwa wamefurahi sana kuja kwa Meneja.

(a) Sasa kwa kuwa Wizara ina sera nzuri za misitu, uvuvi na hifadhi ambazo zimeboreshwa na mazao mengine zinazolenga wananchi wenyewe. Je, sasa kwa kuwepo Meneja wa lile Pori Wizara itatusaidia kuboresha ufugaji wa nyuki na upande mwingine kule Ziwani uvuvi bora?

(b) Sasa hivi pori lile limeingiliwa na wavunaji wa miti ya mininga ambalo ni pori pekee ambalo limebaki lenye miti ya mininga mikubwa. Je, Serikali itatusaidiaje kuzuia uvunaji huo wa miti hiyo ambayo imekuwa michache sasa hivi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli kupeleka meneja katika Pori lile ni katika suala la kuleta maendeleo. Tunatumai kwamba katika shughuli mbalimbali za maliasili ambazo tunasema siku zote zinufaishe wananchi, basi meneja huyo ataweza kushirikiana na uongozi wa Wilaya kwa karibu kabisa ili kuhakikisha kwamba jambo hili linafanyika. Pamoja na suala hili la uvunaji wa miti ya mininga haramu ambao siku zote Serikali imekuwa ikipiga vita na ikipiga makelele. Tunatumai kwamba Waheshimiwa Wabunge kote nchini watasaidia azma ya Serikali na kazi ya Serikali ili kuhakikisha kwamba maliasili hii haiwezi kutoweka nchini kwetu.

Na. 97

**Wagonjwa wa Akili Wanaozurura Kwenye Miji**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa ongezeko la wagonjwa wa akili katika Miji yetu mikubwa kama vile Dar es Salaam, Arusha, Zanzibar na kadhalika inazidi kuongezeka na huwa wanazurura ovyo kwenye Miji na kuhatarisha amani kwa wananchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwakamata wagonjwa hao na kuwashughulikia kwa kuwapa matibabu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba idadi ya wagonjwa wa akili wanaozurura katika Miji yetu mikubwa ni wengi.

Hata hivyo, jukumu la kuwafikisha wagonjwa wa akili kwenye vituo vinavyotoa huduma za matibabu kwa wagonjwa hawa ni la ndugu wa mgonjwa na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya unyanyapaa na umaskini vinachangia kwa kiwango kikubwa hali ya wagonjwa wa akili kutengwa kudhalilishwa, kunyimwa haki zao za msingi na kutopewa misaada wanayostahili na jamii. Jambo hili limefanya wagonjwa wengi kucheleweshwa kufikishwa kwenye huduma za matibabu na hivyo kupungua kwa kiwango kikubwa uwezekano wa kupona.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya inalipa kipaumbele suala la kueneza stadi za kuwahudumia wagonjwa wa akili katika ngazi ya Vituo vya Afya, Zahanati na ndani ya jamii kwa kuwashirikisha wananchi. Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Manyara, Mtwara na Tanga tayari ina mfumo wa kutoa huduma za afya ya akili ngazi ya msingi.

Pamoja na kuendelea kuboresha huduma katika Mikoa hii, Mikoa mingine sita itaingia katika mpango huo mwaka ujao wa fedha. Mpango huu unategemewa kupunguza idadi ya wagonjwa wa akili ambao hawapati tiba sahihi na kuishia kuzurura ovyo mijini. Hospitali zetu za Rufaa kama ile ya Mirembe, Muhimbili, Bugando na Mbeya zina uwezo wa kupokea baadhi ya wagonjwa hawa. Pia Hospitali za Mikoa ya Iringa, Kigoma, Kilimanjaro, Mtwara, Lindi , Morogoro, Ruvuma, Tabora na Tanga zina huduma za kulaza wagonjwa wa akili

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kutumia vituo hivyo vizuri , tunahitaji msaada wa ndugu na jamaa zao kuwapeleka sehemu za matibabu. Itakuwa vizuri kama viongozi wa Serikali za Mitaa watashirikiana na ndugu na vyombo vya usalama kuwapa msaada wa kuwapeleka kwenye vituo vya matibabu wagonjwa wa akili ambao wanaonekana kuhatarisha maisha ya watu wengine katika jamii.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa wengi wa wagonjwa wa akili wanaonekana kuwa ni vijana. Je, Serikali imeishafanya utafiti ni nini kinachosababisha matatizo hayo na Serikali inatoa tahadhari gani kwa vijana wengine? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, sababu za magonjwa ya akili ni nyingi, lakini hususan kwa vijana, madawa ya kulevya ni moja ya sababu kuu za magonjwa hayo. Lakini isichukuliwe kwamba hiyo tu ndiyo sababu ya magonjwa ya akili, lakini yapo magonjwa kama *Schizophrenia* na mengineyo ambayo pia huweza kuwapata vijana.

Mheshimiwa Spika, tahadhari tunayotoa ni kuhakikisha kwamba vyombo vinavyohusika na kudhibiti matumizi ya madawa ya kulevya vinafanya kazi yake ipasavyo na tunatoa wito kwa vijana kujiepusha na madawa ya kulevya ambayo yanaweza kuleta maradhi ya akili.

Na. 98

***Global Funds For Malaria***

**MHE. MARTHA M. WEJJA (k.n.y MHE. DR. BATILDA S. BURIAN)** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara zinazofaidika na Mfuko wa Fedha wa Dunia kwa ajili ya Malaria *(Global Funds for Malaria):-*

(a) Je, ni wanawake wangapi wamefaidika na programu hiyo tangu ianze na kwa vipi?

(b) Je, Serikali inaweza kutoa mchanganuo wa wanawake waliofaidika kati ya wale wa Mijini na Vijijini na jinsi walivyofaidika?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria una lengo kwamba ifikapo mwishoni mwa mwaka 2005 asilimia 60 ya mama wajawazito na watoto wa chini ya umri wa miaka mitano wawe wanatumia vyandarua vilivyotiwa dawa.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia lengo hilo ambalo liliridhiwa na Wakuu wa Nchi za Afrika katika Azimio la Abuja la mwaka 2000, Wizara ya Afya imebuni mradi wa miaka mitatu ujulikanao kama Hati Punguzo ambao utagharamiwa na Mfuko wa Fedha wa Dunia kwa ajili Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria. Mradi huu utawanufaisha wanawake wajawazito na watoto. Chini ya Mradi huo, wanawake wajawazito watapewa hati maalum wanapohudhuria klinki ambayo itawawezesha kununua vyandarua vilivyotiwa dawa kwa bei nafuu.

Kwa kuanzia, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto *(UNICEF)* limeanzisha mradi wa majaribio katika Wilaya za Kibaha na Kilosa kuanzia mwezi Aprili, 2003 ili kuona kama mradi huu unatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kibaha inayokadiriwa kuwa na wanawake wajawazito 5,457 sawa na asilimia 4 ya wakazi wote 136,402 kulingana na sensa ya 2003, katika kipindi cha miezi minane (Mei-Deseamba 2003) mama wajawazito walionufaika na mradi huu wa hati punguzo ni 3,037. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 86 ya hati punguzo 3,336 zilizokabidhiwa katika Vituo mbalimbali vya huduma za tiba Wilayani humo.

Aidha, Wilaya ya Kilosa yenye makadirio ya wanawake wajawazito 20,090, asilimia 4 ya wakazi wote 502,252 kwa kipindi cha miezi mitano (Mei - Septemba, 2003) wanawake wajawazito waliofaidika ni 3,612 ambayo ni sawa na asilimia 37 ya hati punguzo 9,725 zilizokabidhiwa kwenye vituo vya tiba Wilayani humo.

Mheshimiwa Spika, imeonekana kwamba majaribio hayo katika Wilaya hizo mbili yamefanikiwa kuhamasisha sana wanawake kuhudhuria kliniki kwa wingi na mapema zaidi kuliko kipindi cha nyuma. Aidha, wanawake wameweza kupata fursa ya kuelimishwa kuhusu umuhimu wa jinsi ya kujikinga na malaria wakati wa ujauzito.

(b) Mheshimiwa Spika, katika majaribo haya, mchanganuo wa wanawake waliofaidika Mjini na Vijijini ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kibaha Mjini 1,625, Vijijini 1,150 na Kilosa Mjini 911 na Vijijini 2,700.

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Pamoja na kwamba vyandarua vitauzwa kwa bei rahisi Mheshimiwa Naibu Waziri anajua kwamba vyandarua hivyo vya bei rahisi huwa haviwafikii akinamama wote, vinapofika vituoni vinakuwa vya wanaohusika katika vituo hivyo na akinamama hawapewi?

(b) Je, akinamama watakaokuwa wamezaa kwa njia ya uzazi wa mpango watapataje hivyo vyandarua wakiwa wako majumbani pamoja na watoto wao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba utaratibu huu bado haujaanza rasmi. Kwa hiyo, haya niliyoyazungumza ni majaribio tu katika Wilaya mbili za Kilosa na Kibaha, na huko imeonekana kwamba vyandarua vinawafikia wahusika. Pindi tutakapoanza utaratibu huu, mamlaka ya udhibiti wa kuhakikisha kwamba vyandarua hivyo vinawafikia walengwa itakuwa ni Halmashauri husika. Kwa hiyo, tutawataka Halmashauri husika kuhakikisha kwamba vituo hivyo

vinafikisha vyandarua vile kwa wahusika na visibaki na watumishi wa vituo vinavyotoa huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la wanawake wanaotekeleza uzazi wa mpango kuweza kupata vyandarua hivi. Kama nilivyosema awali kwamba vyandarua hivi vimelengwa kwa wanawake ambao ni wajawazito. Kwa hiyo, endapo watakapokuwa wajawazito ndiyo watapatiwa vyandarua hivi, na wale wote wenye watoto chini ya umri wa miaka mitano wanapokuwa wanawapeleka watoto kliniki wataweza vilevile kupatiwa vyandarua hivi. *(Makofi)*

Na. 99

**Shule za Sekondari za Wananchi**

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa Shule za Sekondari za Wananchi zimekuwa ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya elimu nchini; na kwa kuwa maagizo ya Wizara ya Elimu na Utamaduni ni kuwa shule hizo zinatakiwa ziendeshwe kwa ushirikiano kati ya Halmashauri husika na wananchi wa mahali shule zilipo:-

(a) Je, kufuatana na sera ya elimu ya shule hizo, ni nani mmiliki na meneja wa shule hizo?

(b) Je, ni nini wajibu wa Mkurugenzi wa Halmashauri kwa shule hizo katika Halmashauri yake?

(c) Je, ni nini wajibu wa Diwani na wananchi mahali shule zilipo katika Kata?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 mwenye shule anaweza kuwa ni Serikali, Halmashauri ya Wilaya, Jiji, Manispaa na Mji au mtu binafsi au kikundi cha watu kinachomiliki majengo ya shule. Meneja ni yule anayewajibika kuhusu utawala na uendeshaji wa shule au shughuli zinazowahusu wanafunzi.

Kwa hiyo, kwa kuzingatia fasili ya neno mwenye shule na meneja na sera ya kuanzishwa kwa shule za sekondari za wananchi zinazoendeshwa na Serikali, mmiliki wa shule hizo ni wananchi wa sehemu husika kwa kushirikiana na Halmashauri yao kwa kuwa ndio wanaojenga majengo ya shule husika wakati meneja wa shule ni Serikali Kuu kupitia Idara ya Sekondari ya Wizara yangu kwa kuwa ndiyo inawajibika

kuipatia shule ya aina hiyo walimu, vitabu, vifaa, mafungu ya fedha na uendeshaji wa shule wa kila siku.

(b) Mheshimiwa Spika, wajibu wa Mkurugenzi wa Halmashauri kwa shule hizo ni kutoa msaada wa kiufundi katika kuanzisha, kujenga na kusimamia utekelezaji wa miongozo mbalimbali itolewayo na Serikali kuhusu uendeshaji wa shule.

(c) Mheshimiwa Spika, wajibu wa Diwani ni kuhamasisha wananchi wa kata yake katika shughuli za ujenzi wa shule, kuwaandikisha watoto wao walioteuliwa kujiunga na shule hiyo na katika maendeleo ya shule hiyo kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, wajibu wa wananchi ni kushiriki kwa hali na mali katika ujenzi wa majengo ya shule, upatikanaji wa samani na utunzaji wa majengo ya shule na aidha, kuwaandikisha watoto wao waliofaulu mtihani wa darasa la saba na kuwalipia ada hadi kuhitimu elimu ya Sekondari.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa majibu yake ya ufasaha. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema wamiliki wa shule hizo za wananchi ni wananchi wenyewe. Je, wananchi hawa wanawakilishwa vipi katika uongozi wa shule hizi na kwa uwiano upi?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, wananchi kama wamiliki kwa kawaida wanashirikishwa katika uongozi wa shule hiyo kupitia bodi ya shule ambayo kwa sasa huteuliwa na Mkuu wa Mkoa na tumetoa mwongozo kwamba Mwenyekiti wa kikundi kilichojenga shule awe anateuliwa kuwa mjumbe wa bodi ile ili kuwa na hali endelevu.

Na. 100

**Walimu wa Ziada Ngorongoro**

**MHE. ELISA D. MOLLEL (k.n.y MHE. MATHEW TAKI OLE-TIMAN)** aliuliza:-

Kwa kuwa kutokana na hali halisi ya mazingira, maisha na uchumi wa wafugaji pamoja na kuwa nyuma kimaendeleo, idadi ya wanafunzi kwa darasani huwa chini ya 40 kulingana na utaratibu wa sasa wa uwiano wa 1:40 ni dhahiri kwamba shule nyingi kwenye maeneo ya wafugaji zitaendelea kuathirika kwa kutokuwa na walimu wa kutosha:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna sababu za kimsingi za kutoa upendeleo wa makusudi wa walimu wa ziada nje ya utaratibu wa sasa kwa shule kwenye maeneo ya wafugaji ili nao waweze kupata elimu ya msingi ambayo ni haki ya kila raia wa Tanzania?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mathew Taki Ole-Timan, Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Kimsingi Serikali ya Tanzania imekubaliana na Jumuiya ya Kimataifa na kuazimia kutoa elimu ya msingi kwa watoto wote kwa mujibu wa Tamko la Dakar la mwaka 2000. Ili kutekeleza azimio hilo Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Utamaduni iliandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) 2002-2006. Mpango huu umeainisha wazi mikakati mbalimbali ya kutoa elimu ya msingi kwa watoto wote wakiwemo watoto wa wafugaji ambao hulazimika kuhama hama kutafuta malisho na maji kwa ajili ya mifugo yao. Mkakati wa Serikali wa elimu kwa watoto wa wafugaji wa aina hiyo ni kuwaandikisha katika shule za msingi za boda ambazo tunazo jumla ya shule za aina hiyo 24 katika Wilaya za Karatu iko 1, Monduli ziko 5, Ngorongoro ziko 5, kwa Mkoa wa Arusha na Simanjiro 3, Kiteto 5, Mbulu 1 ambayo iko katika hatua za mwisho za ujenzi na Hanang ziko 5 kwa Mkoa wa Manyara.

Hata hivyo, Wizara yangu inafahamu kuwa bado wapo watoto wengi wa wafugaji wanaosoma katika shule za msingi za kawaida ambao huhama na wazazi wao na kusababisha upungufu wa wanafunzi katika shule walizokuwa wanasoma hasa katika madarasa ya V, VI na VII na kusababisha shule hizo kupangiwa walimu wachache kwa kuzingatia uwiano wa mwalimu 1 kwa wanafunzi 40. Ushauri wa Wizara ni kuwa shule hizo zitumie mkakati wa ufundishaji wa kuchanganya madarasa unaojulikana Kimataifa kama *Multi Grade Teaching.*

Ufundishaji huo ni ule wa mwalimu mmoja kufundisha madarasa mbalimbali mada moja katika chumba kimoja au madarasa mbalimbali katika chumba kimoja kufundishwa mada mbalimbali kwa wakati mmoja. Ufundishaji huu husaidia shule zenye watoto wachache katika madarasa tofauti kuweza kufundishwa na mwalimu mmoja au walimu wachache waliopo. Aidha, utaratibu huu husaidia shule zenye wanafunzi wachache kuwa na walimu wachache wanaoweza kuwafundisha vizuri, kama shule za kawaida zenye uwiano mwalimu mmoja kwa wanafunzi 40.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Idara ya Ualimu inatoa mafunzo ya ufundishaji kwa kutumia mbinu hii ya kuchanganya madarasa kwa wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu ili hatimaye waweze kutoa mafunzo hayo kupitia Vituo vya Ualimu vilivyo katika Wilaya mbalimbali. Aidha, katika muda wa miaka miwili iliyopita Wizara yangu iliwapanga walimu 31 katika shule za msingi za Wilaya ya Ngorongoro na mwaka huu wamepangwa walimu wengine 85 katika Wilaya hiyo. Kwa hiyo tatizo hili la upungufu wa walimu katika Wilaya ya Ngorongoro linazidi kupungua.

Na. 101

**Kilimo cha Umwagiliaji Serengeti**

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA** aliuliza:-

Kwa kuwa Jimbo la Serengeti lina mabonde mengi kama yale ya Kemogesi, Hekwa, Nyamatoke, Iharara ambayo yanaweza kutumika katika kilimo cha umwagiliaji maji ili kuondoa kero ya chakula katika Jimbo hili:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji maji katika Wilaya ya Serengeti?

(b) Je, Serikali inatarajia kuanza na kukamilisha kazi hii lini na itagharimu kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia Mpango kabambe wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani, umekwishaainisha mabonde ya Kemogesi, lenye hekta 280, Hekwa lenye hekta 300; Nyamatoke lenye hekta 150 na Iharara lenye hekta 180, kuwa yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani.

Aidha, Serikali imekwishafanya usanifu wa Bwawa la Mesaga lililoko kwenye Bonde la Hekwa. Iwapo bwawa hilo na mfumo wa umwagiliaji maji vitajengwa, eneo lenye ukubwa wa hekta 270 litaweza kumwagiliwa maji.

(b) Serikali inakusudia kujenga bwawa la Mesaga katika mwaka wa fedha wa 2004/2005. Gharama za ujenzi wa bwawa hilo zinakisiwa kuwa shilingi milioni 100. Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti inashauriwa kufanya usanifu wa mabonde ya Kemogesi, Hekwa, Nyamatoke na Iharara yenye eneo la jumla ya hekta 910 na kuyaombea fedha kutoka Serikalini chini ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Wizara ya Kilimo na Chakula itaendelea kutoa misaada ya utaalamu na ushauri pale itakapohitajika.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kukumbusha kwamba tayari Halmashauri yetu imeshafanya *feasibility study* ya Bonde la Kemogesi na hivyo kuiwasilisha Wizarani. Je, ni lini sasa Serikali itatimiza ahadi yake ya kuwapatia wananchi wa *Kemogesi Irrigation Scheme* katika sehemu hiyo kwa sababu tayari tumeshapeleka *study* yetu kule Wizarani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kama hiyo *study* imewasilishwa karibuni, fedha za mwaka huu zimekwishatumika.

Kwa hiyo, tusubiri fedha za mwaka unaoanzia Julai 2004/2005. Vinginevyo si vibaya tukawasiliana tufuatilie kwa pamoja suala hili. Pengine bado hiyo study haijafika Wizarani ili tuokoe muda tushirikiane kwa suala hili.

Na. 102

**Sikonge kupata Hadhi ya Mkoa katika Uzalishaji wa Tumbaku**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Sikonge inazalisha Tumbaku nyingi lakini mpaka sasa haijapewa hadhi ya Mkoa kiuzalishaji na hivyo kuifanya Bodi ya Tumbaku kutofungua Ofisi ya Bodi Wilayani Sikonge:-

(a) Je, Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku haioni kwamba kutokuwa na ofisi Wilayani Sikonge kunawakosesha wakulima ushauri wa karibu wa kitaalamu wa zao hili muhimu la biashara Wilayani Sikonge?

(b) Je, ni lini wakulima wa Sikonge watapata hadhi ya Kimkoa kwa uzalishaji wa Tumbaku?

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza idadi ya wateuzi wa Tumbaku ambao uchache wao umekuwa unachelewesha masoko ya Tumbaku katika kipindi cha msimu wa mauzo na hivyo kuwapa hasara wakulima kwa kuharibikiwa kwa Tumbaku yao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sehemu za (a) na (b), nafurahi kumjulisha Mheshimiwa Juma Nkumba na Bunge lako Tukufu kwamba Wilaya ya Sikonge ilipewa hadhi ya kuwa Mkoa wa Tumbaku tangu tarehe 5 Aprili, 2004 na kufungua ofisi ya Bodi ya Tumbaku Wilayani Sikonge.

Mheshimiwa Spika, ili eneo linalozalisha Tumbaku lipewe hadhi ya kuwa Mkoa wa Tumbaku ni sharti lizalishe zaidi ya kilo 2,500,000 za Tumbaku, kiwango ambacho Wilaya ya Sikonge ilifikia katika msimu wa mwaka 2000/2001.

Katika msimu wa mwaka 2002/2003, Wilaya ya Sikonge ilizalisha kilo 3,299,676 na Wilaya hiyo inatarajiwa kuzalisha kilo 4,500,000 katika msimu wa mwaka

2003/2004 ambazo ununuzi wa Tumbaku yake unaendelea. Nawapongeza sana wakulima wa Tumbaku wa Sikonge kwa mafanikio hayo. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, Bodi ya Tumbaku inao wateuzi wa Tumbaku 19 wenye uwezo wa kuteua jumla ya kilo milioni 95 za Tumbaku kwa msimu ikilinganishwa na kilo milioni 33 za Tumbaku zilizozalishwa mwaka wa 2002/2003. Mteuzi mmoja ana uwezo wa kuteua tani 5,000 za tumbaku kwa msimu.

Aidha, Bodi ya Tumbaku iliajiri wateuzi wanafunzi sita mwezi wa Januari, 2004 ambao wanapatiwa mafunzo ili kuongeza uwezo wa uteuzi katika Bodi.

Tatizo, kwa hiyo, siyo uchache wa wateuzi bali ni kuwapo kwa vituo vingi vidogo vidogo vya kununulia Tumbaku ambavyo vinawafanya wateuzi wa tumbaku kupoteza muda mwingi wakisafiri kutoka kituo hadi kituo.

Kwa kuwa Mkoa wa Tumbaku wa Sikonge haujafikia uzalishaji wa tani 5,000 za Tumbaku, mteuzi mmoja aliyeko angetosheleza mahitaji ya Mkoa huo kama kusingekuwepo na vituo vingi vidogovidogo. Bodi ya Tumbaku inashirikiana na wadau wengine wa zao hilo ili kurekebisha mtandao wa vituo vya kununulia tumbaku nchini kwa kuanzisha vituo vichache vikubwa vya kununulia tumbaku kwenye maeneo yanayolima zao hilo.

Aidha, kutokana na ombi la Mheshimiwa Juma Nkumba, Mkoa wa Tumbaku wa Sikonge utaongezewa mteuzi mwingine mmoja wa tumbaku mapema iwezekanavyo.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kukamilisha kwa haraka ombi hili la kupata hadhi ya mkoa na kuniahidi kunipatia mteuzi wa pili na *Hansard* imeandika. Sasa swali.

Kwenye jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Bodi inashirikiana na wadau wa zao kuanzisha vituo vichache vikubwa vya kununulia tumbaku. Je, gharama za kusafirisha kupeleka kwenye vituo hivyo itakuwa ya nani ili vituo hivyo visije kuongeza gharama kwa wakulima? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa Serikali kupitia Bodi imekubali kuongeza mteuzi wa pili. Je, Serikali inaangalia vipi suala la vitendea kazi vya Ofisi ukiwepo pia usafiri ili wateuzi hao wafanye kazi kwa ufanisi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vituo hivyo vitapangwa kwa umakini ili visiwe mbali sana na wazalishaji wa tumbaku hatutegemei usafirishaji wa tumbaku utaongeza gharama.

Pili, kufuatia kuanzishwa kwa mkoa mpya wa Sikonge Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku imepanga Mteuzi wa Tumbaku Mfawidhi wa Mkoa huo ambayo yuko Sikonge

tangu tarehe 5 Aprili, 2004 alipoanza kazi rasmi. Aidha, ataongezewa mteuzi mwingine wakati wa uteuzi ili kuhakikisha huduma ya uteuzi inatolewa kwa kiwango cha kutosha.

Vile vile Bodi imepanga kununua gari la mkoa mpya wa Tumbaku Sikonge wakati wa mauzo ya tumbaku wa sasa 2004/2005. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Kwa hiyo mnataka mwongozo. Ehe !!! lete.

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO:** Naomba mwongozo wa Spika. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wakati anajibu amesema kwamba kuna mkoa wa tumbaku. Je, mikoa iliyopo nchini umeongezeka mmoja. Naomba kufahamishwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo ni swali la nyongeza. Lakini nilishatangaza kama muda wa maswali umekwisha. Kwa hiyo, lihifadhi mpaka siku nyingine.

Matangazo ya vikao vilivyopangwa kwa leo. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala , Mheshimiwa Janguo anawatangazia wajumbe wake wakutane leo tarehe 21 kwenye ukumbi Na. 133 kuanzia saa 4.30 yaani kuanzia mwisho wa kipindi cha maswali.

Kamati nyingine ni Uwekezaji na Biashara. Mheshimiwa Mwenyekiti Shellukindo, anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 5.00 katika chumba Na. 227 ghorofa ya 2.

Vikao visivyokuwa vya Kamati za Bunge viwili. Mheshimiwa Kimiti, Mwenyekiti wa Wanachama cha Wabunge cha Masuala ya Idadi ya Watu na Maendeleo, anaomba wanachama wa chama hicho cha hiari wawe na kikao kifupi leo saa 7.00 mchana mara baada ya kuahirisha Bunge, inawezekana Bunge halitaahirishwa saa 7.00, kwa hiyo imaanishe kwamba wakati muafaka tutakapofikia hatua hiyo.

Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Vijana naye anaomba wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya chama hicho sio wote wakutane jioni saa 10.00 katika chumba 231 vyumba vya Kamati.

Mwisho wa vikao. Jana Waheshimiwa Wabunge niliwatangazia kutokuwepo Bungeni kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa nawatangazia kwamba amerejea Bungeni na yupo hapa. *(Makofi)*

Kuhusu *order paper* ya leo Waheshimiwa Wabunge nimearifiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kutokana na ombi langu la jana kwamba wajitahidi kumaliza shughuli zote jana hiyo hiyo. Basi ameniambia asubuhi hii kwamba walimaliza saa 4.00 usiku kwa hiyo hawajapata muda wa kuandika zile taarifa za kuwasilisha hapa kwa asubuhi hii.

Kwa hiyo, ameniomba na mimi nimekubali kwamba mjadala wa Muswada huu uanze saa 11.00 jioni. Badala ya mara baada ya hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa weli nisisahau nimeombwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge Wote wa CCM kwamba tutakapomaliza hoja iliyopo mbele yetu wabaki hapa kwa muda mfupi kwa maelezo ambayo watayatolea.

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii Pamoja na Mapendekezo Yaliyomo Katika Taarifa Hiyo

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Tulibaki na wasemaji wawili lakini kwanza natoa nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge wanaokwenda kunywa chai wafanye hivyo.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto naomba kuchangia hoja iliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Sophia Simba.

Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Pili, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge watatu waliopata nyadhifa kama vile Mheshimiwa Mongella, Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika, Mheshimiwa Ntagazwa, Rais wa Baraza la Mazingira Umoja wa Mataifa na Mheshimiwa Pius Ngw'andu, Rais wa Mawaziri wa Afrika wa Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nikiri kwamba Wizara yangu inashirikiana kwa karibu sana na Kamati ya Maendeleo ya Jamii inayoongozwa na Mheshimiwa Sophia Simba na Makamu wake Mheshimiwa Haroud Masoud pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa hii kuna hoja 28 kwa Wizara zote mbili yaani Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya vijana na Michezo. Kwa hiyo, nitajaribu kujibu baadhi ya hoja katika kijitabu hiki na baadhi ya hoja zilizojadiliwa hapa tangu jana na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nizungumzie kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Vyuo hivi vya Maendeleo ya Wananchi vipo 58 na kila Mbunge aliyesimama hapa amechangia kwa uchungu sana kwa vyuo hivi ninawashukuru sana. Sasa katika kujibu niseme kwamba hususan kwa upande wa ukarabati. Wizara imeendeleza na utaratibu wa kufanya ukarabati wa majengo ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa awamu kwa njia ya ukarabati mdogo mdogo kwa kati ya shilingi 4 milioni hadi 6 milioni kwa chuo ambapo vyuo 16 vilipelekewa fedha za ukarabati huo mwaka 2001/2002. Vyuo 16 mwaka 2002/2003 na mwaka huu vyuo 24. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu orodha ni ndefu na wala sitaweza kusoma hapa lakini naomba tu nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge mwenzangu sijui yupo, Mheshimiwa

Suru, Mbunge wa Kondoa Kaskazini jana wakati alipokuwa anachangia alikuwa anazungumzia ukarabati wa Chuo cha *FDC Munguri*. Nafurahi kusema kwamba Wizara ilipeleke kiasi cha shilingi 5 milioni kwa mwaka 2003/2004. Sasa ukarabati unaofuata mimi namshauri kwamba vyuo hivi kama walivyoshauri Kamati kwamba pia ni Halmashauri husika zisaidie. Sasa natoa wito kwamba Halmashauri husika ziendelee kusaidia vyuo hivyo pamoja na Serikali Kuu kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, pia mwaka huu 2004/2005 vyuo 12 ambavyo viliwekwa katika mpango wa ukarabati mkubwa vimepelekewa fedha katika robo ya tatu kama ifuatavyo. Hili limekuwa linajitokeza sana katika ziara hii tuliyokwenda Morogoro. Sasa naomba kutoa taarifa tu kwamba tayari Wizara imepeleka. Kagera tumepeleka shilingi 10,000/= Chitalu, Dodoma shilingi 14 milioni, Karumo, Mwanza shilingi 12 milioni, Kihinga, Kigoma shilingi 10 milioni, Kilosa, Morogoro shilingi 15 milioni, Kisangwa, Mara shilingi 12 milioni, Bugai ,Tanga shilingi 14 milioni, Mlale, Ruvuma shilingi 15 milioni, Monduli, Arusha shilingi 10 milioni, Mtawanya, Mtwara shilingi 10 milioni, Ruaha, Iringa shilingi 13 milioni na *FDC* ya Sofi Morogoro shilingi 10 milioni. Mheshimiwa Mhagama uliniuliza naja..........

**SPIKA:** Nataka kukuarifu Mheshimiwa Waziri kwamba una dakika zako 15 tu. Kwa hiyo, takwimu pengine ungezigawa.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Sawa. Mheshimiwa Mhagama naona sasa hayupo. Kwa hiyo, tunaendelea kuvikarabati hivi vyuo lakini ombi langu pia Wakurugenzi wahusika tuwe nao ili tuweze kuviendeleza hivi vyuo.

Mheshimiwa Spika, Wizara iwahimize Wenyeviti wa Bodi kuitisha vikao vya Bodi kwa wakati muafaka hasa Wabunge wanapokuwa majimboni. Mimi ninaafikiana na hilo kwa sababu Wenyeviti wa Bodi ni Wakurugenzi na nawasihi sana kwamba vikao hivi viitishwe wakati Wabunge wapo sio wakati Wabunge wako Bungeni ndio wao wanaitisha vikao hivyo. Ni vizuri kupata maoni ya wachaguliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze fungu kwa ajili ya kununulia vifaa na dhana mbalimbali. Naafikiana nalo na hilo. Kwa mfano, kwa mwaka 2003/2004 tulipewa kiasi cha shilingi 58 milioni na nimewasomea baadhi ya fedha zilizotumika. Pia kama Mheshimiwa Suru, Mheshimiwa Kimbau, Mheshimiwa Simpasa wamezungumzia kwa uchungu watoto wa kike kupata mimba. Naafikiana na hilo suala la watoto wa kike kupata mimba linapaswa liangaliwe kwa undani zaidi hasa katika nyanja za malezi, ujamiisho *(socialization)* katika familia zetu.

Baadhi ya wazazi huwaona watoto wa kike kama kitegauchumi na hivyo kuwaozesha hata kabla hawajamaliza Shule ya Msingi kwa manufaa yao kama vile kupata fedha, mifugo na mali nyinginezo. Mila na desturi zingine zinaingiza watoto kwenye vishawishi vinavyoweza kuwafanya wasipende shule. Mfano ni ngoma mbalimbali zinazokesha na watoto wakiwemo bila wazazi au walezi kukemea. Baadhi ya

wazazi au walezi kutokutambua umuhimu wa elimu na kutotambua nafasi pekee waliyonayo watoto wa kike katika kuleta maendeleo ya Jamii. Hata baadhi ya watu wazima au wazee hupendelea kuoa watoto wadogo. Ushauri wazazi walezi kwa ujumla wanatakiwa kubadilisha fikra zao na kutambua kuwa watoto wa kike wana nafasi pekee katika kuleta maendeleo ya jamii na hivyo kuwapa nafasi ya kujiendeleza kielimu.

Waheshimiwa Wabunge na Kamati pia walizungumzia masuala ya Chuo cha Tengeru. Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kinaendelea kuendesha kozi fupi ili kuwasaidia kupata kipato cha haraka na kuwapatia wataalamu na watu wengine zaidi hasa wa Vijiji. Kwa mfano kozi hizo zimekuwa kama vile mwezi Februari hadi Machi, 2004 washiriki kutoka nchini Rwanda walipatiwa mafunzo ya kazi ya Maendeleo ya Jamii. Mwezi Februari 2004 washiriki kutoka Bunda walipatiwa mafunzo ya ushirikishwaji kwa wakulima na bado kuna washiriki wengine kama vile *Marine Park* na *Monduli Farmers Group* watakwenda pale kupata mafunzo mengine. Chuo cha Tengeru pia kinashirikiana na Chuo cha *Development Planning Unit* cha London katika masuala ya utafiti. Wanafunzi hukipatiachuo kipato kwa kulipia mafunzo, malazi na chakula. Mkakati wa chuo ni kuandaa programu mbalimbali na kuzitangaza nje na ndani ya nchi. Kamati pia imeagiza kwamba chuo hiki cha Tengeru kipatiwe vifaa. Nafurahi kusema kwamba katika bajeti hii ya mwaka 2004/2005 tumewafikiria ili wanunuliwe kompyuta wapate *internet facilities,* umeme *phase* tatu na mambo mengi tu. Mheshimiwa Haroud Masoud na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu walizungumzia Chuo cha Tengeru ukae na uongozi wa chuo. Hapa kuna tatizo la ardhi na mipaka naomba nitajibu hapo baadaye. Pia alizungumzia masuala ya familia. Ninaafikiana na yeye kwamba familia ni kitovu cha maendeleo na kwa bahati nzuri kwa mwaka huu Tanzania kama nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa wanaungana na Mataifa mengine ya Umoja huo kuadhimisha miaka 10 ya Siku ya Familia Duniani, siku hii inaadhimishwa tarehe 15 Mei kila mwaka na mwaka huu siku hiyo itaadhimishwa mkoani Kigoma na kauli mbiu itakuwa: "Familia ni Kitovu cha Maendeleo". Mwaka jana siku kama hiyo iliadhimishwa na kauli mbiu ilikuwa :"Uvivu Katika Familia ni Adui wa Maendeleo". Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba anajali familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Suru na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu walizungumzia masuala ya utekeketaji. Mimi naafikiana nao. Ukeketaji ni kitendo cha ukatili. Ukeketaji unafanyika kwa siri sana. Lakini katika jamii hao mangariba wanafahamika kwa nini wasifichuliwe. Kwa sababu tunawafahamu kwa hiyo mimi natoa wito kwamba hawa mangariba wafichuliwe ili tuwachukulie hatua kama inavyotakiwa. Lakini nashukuru kwamba kuna baadhi ya mangariba wameanza kufanya hivyo kuacha kabisa kazi hiyo ya kukeketa nawashukuru na natoa wito kwamba hao waliobakia pia wafuate nyayo za wenzao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jenista Mhagama alizungumzia suala la uundaji wa Benki ya Wanawake. Wizara inapokea mapendekezo kutoka wataalamu kuhusu namna bora ya kuanzisha Benki hizo. Mapendekezo hayo yalichangiwa vizuri na wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Hivi sasa Wizara inafanyia kazi mapendekezo haya na rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri unakamilishwa. Hii itatuwezesha kupeleka mapendekezo hayo Serikalini kwa maamuzi ya mwisho.

Kuhusu eneo la Monduli na suala la KKKT. Wizara imefuatilia suala hili na imedhihirika kwamba kulikuwa na agizo la Rais wa awamu ya pili kwamba chuo kitoe sehemu ya eneo kwa ajili ya KKKT. Agizo hili lilitokana na ombi la KKKT kwake Mheshimiwa Rais wa awamu ya pili. Utafiti wa awali wa Wizara umeonyesha kulikuwa na maafikiano kwamba KKKT wapewe eneo hilo kwa masharti kwamba watakiendeleza chuo kimajengo. Hivi sasa Wizara inafuatilia kama hili lilifanyika na kama halikufanyika ni nini kinatakiwa kufanywa hivi sasa. Wizara inatekeleza jukumu kwa kushirikiana na chuo na Wizara ya Ardhi kabla ya kuwasiliana na KKKT ili nao watoe mawazo yao kuhusu suala hili.

Kuhusu utata wa *Rest House* iliyopo eneo la chuo Monduli. *Rest House* hii ilijengwa na *NORAD* wakati wakiwa katika shughuli za kimaendeleo katika eneo la Monduli. Inasemekana kulikuwa na makubaliano watakapoondoka *Rest House* iwe mali ya Halmashauri. Hata hivyo *Rest House* ipo ndani ya eneo la chuo. Jitihada za Wizara kupata makubaliano kutoka Halmashauri ya Monduli hazikufanikiwa pamoja na agizo la Waziri la kumtaka Mkurugenzi kuwasilisha nyaraka hizo ndani ya kipindi cha wiki tatu toka Kamati ilipotembelea Monduli tarehe 21 Oktoba, 2003. Hata hivyo ni muda mfupi tu kabla ya kuja Dodoma ndipo nyaraka hizo ziliwasilishwa. Hivi sasa zinachambualiwa na wataalamu ili tujue hatma ya *Rest House* hiyo.

Nimezungumzia mahusiano ya familia nimejaribu kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama. Lakini pia kulikuwa na *concern* ya *enrolment* ya wanafunzi wanawake katika *FDCs.* Tunaafikiana na Kamati kwamba *enrolment* yao sio nzuri lakini kulikuwa na sababu nyingi. Sababu kubwa ni majengo. Lakini baada ya ukarabati *enrolment* umeanza kuongezekana kama walivyoona Waheshimiwa Wabunge tulipotembelea mkoa wa Morogoro. Kwa mfano *FDC Bigwa* kwa mwaka huu wanawake wako 45 na wanaume 46. *FDC Ifakara* wanawake wako 30 wanaume 68. *again.* Kwa hiyo, tunasema kwamba tutakuwa pamoja katika kuwahamsasisha ili wanawake zaidi waweze kujiunga na vyuo hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda nimeshindwa kujibu hoja nyingi lakini tutawapelekea kwa maandishi. Naomba kuunga hoja mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kuhusu ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Pia naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti wa Kamati hii aliyoiwasilisha ripoti kwa niaba ya Kamati nzima. Lakini vile vile nichukue nafasi hii kuishukuru Kamati nzima ya Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano na ushauri wa karibu wanaoendelea kuipatia Wizara yangu. Napenda kuwahakikishia kuwa tunathamini sana michango yao na imetusaidia sana katika kuboresha utendaji wa Wizara yangu. Baada ya kusema hayo naomba sasa na mimi nichangie katika ripoti hii. Katika kuchangia ripoti hii na michango ambayo Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kusema, yapo mambo ambayo yatajibiwa au yatafafanuliwa na mtoa hoja mwenyewe, mimi leo sio mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, ripoti imezungumzia juu ya uhaba na kutowatumia wataalamu wa michezo waliopo. Tunakiri kwamba katika ngazi ya michezo ya Kimataifa ni kweli tunao upungufu mkubwa wa wataalamu. Kwa kiasi kikubwa hali hii inatokana na ufinyu wa bajeti wa sekta ya michezo ambayo inategemea ukuaji wa pato la Serikali. Lakini Serikali haikukaa tu. Juhudi za Serikali katika kutatua hili ni pamoja na hizi zifuatazo: Kuhuisha mikataba ya Utamaduni. Tunayo mikataba mingi ya Utamaduni ambayo ndani yake kuna vifungu vinavyohusu michezo. Sasa tunaangalia jinsi ambavyo vifungu hivi vinavyoweza kutumika ili kunusuru hali hii. Hivi sasa kwa mfano tuna mazungumzo na nchi mbili za Ulaya kutupatia wataalamu wa michezo japo kwa gharama nafuu. Lakini vile vile kama ilivyozungumzwa hapa jana tunaye mtaalamu wa *karete* kutoka Japan tumepatiwa na Shirika la *JICA* ambaye anatusaidia sana ku-*promote* mchezo wa *karate* na Tulipokwenda Manchester vijana wetu wa *karate* walifanya mambo mazuri.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna baadhi ya vilabu ambavyo vimefikia katika ngazi ya kucheza michezo ya Kimataifa. Kwa mfano klabu kubwa kama Simba, Yanga na Mtibwa nao vile vile huwa wanapata Makocha kutoka nje ili kuwaweka sawa katika kuimarisha mchezo wa mpira wa miguu. Hivi karibuni kuna ujumbe wa Serikali ambao utakwenda Cuba ili kutia saini mkataba wa utamaduni. Ndani ya mkataba huu masuala ya michezo yamepewa kipaumbele sana. Ujumbe huu wa Serikali utajumuisha na ujumbe wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar akiwemo Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Michezo, Mheshimiwa Harun Suleiman. Hatua ya pili ambayo Serikali inajaribu kuchukua kwa maana ya hali hii ni kuongeza fedha katika bajeti kutegemeana na kukua kwa uchumi na pato la Taifa. Kama tumekuwa tunafuatilia tangu awamu ya tatu ilipoingia madarakani tulianza na sifuri sasa hivi tunakwenda tunaongezewa katika sekta ya michezo jinsi ambavyo pato la Serikali linavyoongeza.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge la tatu ni kuanzisha kodi maalum ili kusaidia michezo. Ndani ya Bunge hili hili kama tunavyofahamu sisi sote Waziri wa Fedha alituambia Bodi iliyoundwa ili kusimamia utekelezaji wa sheria hii inaanza kazi yake mwezi Septemba. Kwa hiyo, tunayo matumaini kwamba baada ya kodi hiyo kuanza, huu ukame wa fedha tulionao katika sekta ya michezo kwa kiasi kikubwa utakuwa *addressed* au utaangaliwa na kupunguzwa. Lingine ambalo Serikali inafanya inapobidi huwa tunachangisha fedha kutoka kwa Makampuni, Mashirika na watu binafsi ambao ni wapenzi wa michezo na kupitia Bunge hili Tukufu naomba niwashukuru sana wadau hao kwa jinsi ambavyo wamekuwa tayari mara kwa mara kusaidia michezo ili kuhakikisha kwamba bendera ya Tanzania inaendelea kupepea katika michezo ya Kimataifa. Pia limezungumzwa suala la Serikali kurejesha michezo na mashindano ya michezo shuleni kama ilivyokuwa zamani. Serikali bado inalitafakari hilo ili kupata utaratibu mzuri zaidi ambao utafanya michezo na taaluma visiathiriane. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa michezo ngazi ya shule bado inaendelea haijapigwa marufuku.

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa Uwanja wa Taifa pia lilijitokeza. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa karibuni kila kitu kinachohusu kuanza ujenzi wa Uwanja wa Taifa kimekamilika. Serikali sasa iko katika hatua za mwisho mwisho za

uteuzi wa mjenzi. Lakini kwa kuwa mradi wenyewe ni mkubwa zoezi hili linapaswa kufanywa kwa uangalifu sana na vile vile kwa wale Waheshimiwa Wabunge wenye mazoea ya kwenda uwanjani pale, Uwanja wa Taifa Dar es Salaam bila shaka watakuwa wameona baadhi ya shughuli fulani fulani ambazo zimekwishaanza kama maandalizi kamili ya kuanza ujenzi wa uwanja wa Taifa.

Kuhusu suala la fedha na vifaa vya michezo wanazopata *FAT* kutowafikia walengwa. Hili suala kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge Serikali inaendelea kulifuatilia na ndio maana kuna kesi Mahakamani ya ubadhirifu wa fedha za *FAT* kesi ambayo sasa inatimiza miaka sita (6).

Kwamba fedha hizi wanaofaidi ni Simba na Yanga tu. Hiyo sio sahihi. Nina hakika kabisa kwamba Simba hawajapata hata senti moja na nadhani hata Yanga pia hawajapata chochote badala yake wao ndio ambao fedha zao zilichotwa na kuliwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Suru alizungumza kuhusu watoto kusahauliwa katika ile ripoti. Lakini nina hakika ripoti ile ukiisoma imezungumzia sana watoto wa mitaani na watoto yatima ambao ndiyo hasa wako chini ya malezi yetu. Sasa wale watoto wengine walio katika majumba ya mtu mmoja mmoja na hawa Wajumbe wenyewe wa Kamati nao vile vile ni wazazi, nadhani tutaendelea kushirikiana kwa namna ambayo wanaweza wakashughulikia suala hili.

Mheshimiwa Spika, vile vile alizungumza kwa uchungu sana juu ya akina mama wanaokeketwa. Nadhani hili nitamwachia Mheshimiwa Mwenyekiti kwa sababu inaelekea Mheshimiwa Suru anao uzoefu wa kutosha, nadhani mkimpata huyo atawaelekeza hata katika maeneo pengine na baadhi ya waathirika walivyopata matatizo, mnaweza mkapata habari zilizokamilika.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, alishauri *VETA* waanzishe kozi fupi fupi ili kuongeza ufanisi. *VETA* tayari wameshatekeleza suala hili na ndiyo maana tuna kitu tunachoita *Competence Best Education and Training (COBET).* Ni zile kozi fupi fupi ambazo zinalenga katika mahitaji ya kila mteja. Mtu anakwenda pale anasema: “Mimi nimekuja hapa kutaka kujifunza uashi.” Basi unamwangalia katika uashi ni masuala gani ambayo anataka kuyapa kipaumbele. Unampa hiyo kozi ya miezi miwili, mitatu anaondoka pale akiwa amekamilika zaidi, lakini bado kuna kozi za muda mrefu vile vile.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ya matunzo ya mtoto wa nje ya ndoa kuwa ni Sh.100/=. Hilo ni sahihi, bado ni Sh.100/=, lakini sheria hizi ndiyo zile zile kama zile Sheria za Kazi ambazo zilitungwa muda mrefu. Nadhani hii ilitungwa mwaka 1949 na sisi tumeirithi wakati inapitishwa kwamba matunzo yawe Sh.100=. Wakati huo mishahara ya Watanzania wengi ilikuwa iko chini sana, wengi ilikuwa ni Sh.30/= hadi Sh.40/= kwa mwezi. Kwa wale waliomaliza *form four* kama hukufaulu mshahara ulikuwa Sh.213/= na ukifaulu Sh.290/=. Sasa fikiria inachukuliwa Sh.100/= katika Sh.213/= au Sh.290/= ilikuwa ni hela nyingi sana na ndiyo jinsi ambavyo hata fidia kwa Wafanyakazi ilivyokuwa. Mfano ukifariki ukiwa bado kazini unapata Sh.80,000/=,

ukiumia kazini unalipwa Sh.108,000/=. Sh.80,000/= za wakati ule ungeweza kujenga nyumba ya maghorofa karibuni matatu na Sh.108,000/= ndiyo zaidi.

Kwa hiyo, ni kutokana na hali hiyo ndiyo maana mnaona kiasi hicho kilikuwa kimekadiriwa. Hivi sasa hali imebadilika ndiyo maana katika awamu ya pili ya *Labour Law Reform,* tutakaporejea zile Sheria za Kazi haya yote yataangaliwa, yaani hii sheria ya matunzo nje ya ndoa na katika kile kifungu kinachohusu hifadhi ya jamii na vile vile hii fidia kwa Wafanyakazi wanaoumia kazini. Hayo yote tunategemea kuyarejea wakati tutakapokuwa tunaleta hapa Miswada inayohusu Awamu ya Pili ya Kurekebisha Sheria za Kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kuhusu ukosefu wa wanafunzi katika Chuo cha *VETA Mtwara* limezungumziwa. Pia, Mheshimiwa Haroub Masoud na Mheshimiwa Halima Kimbau wakauliza kuna nini Mtwara? Mtwara kwema sana, kuna upepo, kuna marashi na kuna korosho.

Mheshimiwa Halima Kimbau, nataka nikuhakikishie kwamba hali ni shwari. Kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa na Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo kwa kweli tumehamasisha kiasi cha kutosha na sasa nafasi karibuni zote zimejaa katika Chuo chetu cha Mtwara kuanzia muhula wa Januari mwaka 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, Mheshimiwa Halima Kimbau alipongeza Shirika letu la *NSSF* kwa kupata hati safi ya ukaguzi wa mahesabu. Nakushukuru sana Mheshimiwa kwa pongezi hizo, lakini pia napenda kukuarifu kwamba katika ripoti hata Mashirika yetu mengine ya *NIP, VETA* na Taasisi ya Ustawi wa Jamii nayo pia yamepata hati safi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna suala la upungufu wa watumishi katika Mahakama ya Kazi. Suala hili linashughulikiwa katika zoezi zima la *Labour Law Reform.* Upo mpango kamambe ulioandaliwa wa kufanya *capacity building* kwa watumishi waliopo. Kwa mfano, juzi juzi tu hapa baadhi ya viongozi walikwenda Afrika Kusini ili kuimarisha *skills* zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Ustawi wa Jamii kilichopo Kilosa, chuo hiki kipo chini ya Idara ya Vijana. Chuo hiki kinafanyiwa ukarabati kwa sababu fedha tunazozipata mnazifahamu ni kidogo kidogo, siyo kwamba Serikali ni wachoyo, hapana, ni kutokana na uwezo wao. Sasa, tunapopata fedha kidogo kidogo tunafanya mambo kwa mpangilio. Tulianza kwanza kukikarabati ndiyo maana mlipokwenda mkakuta chuo chetu ni kizuri na kinapendeza kuliko cha wenzetu, hiyo ni kutokana na fedha ambazo tulipata. Katika bajeti inayokuja tumekusudia sasa kuanza mafunzo kwa sababu chuo hicho ndiyo chuo pekee ambacho kitakuwa kinashughulikia mafunzo ya uongozi kwa vijana, sasa kukitoa tena tutakuwa tumerudi nyuma sana. Naomba tuendelee kuachiwa hiki kwa sababu tunayo mipango ya kukitumia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Kazi Kanda ya Ziwa tatizo lilikuwa ni kupata majengo. Nashukuru uongozi wa Mkoa wameshatupatia majengo na ukarabati

hivi sasa unaendelea. Taasisi ya Ustawi wa Jamii kupata kasma yake, sisi tunaamini kwamba utaratibu uliopo hivi sasa unakidhi kwa sababu fungu lake lipo chini ya Katibu Mkuu, halipo chini ya Kamishna wa Ustawi wa Jamii na hakuna anayeligusa isipokuwa wao wenyewe, uongozi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii. Lakini chuo chenyewe kitakapoendelea kukua sisi tunaamini tutapeleka hoja Serikalini ili Serikali iweze kutoa kibali na Taasisi iweze kujiendesha yenyewe kama ilivyo *VETA, NSSF* na *NIP* ambazo zote zilikuwa ni Idara katika Wizara yangu na hivi sasa zinajitegemea.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kulijitokeza hoja ya wadaiwa sugu katika Mashirika yetu *NSSF, VETA* na *NIP.* Nataka nikuhakikishie kwamba, Bodi za Mashirika haya zimeshaanza kushughulikia masuala haya, wameshawapeleka baadhi ya wadaiwa hawa mahakamani japokuwa wengine wamepeleka *court injunction* ili hatua ambazo zingetaka kuchukuliwa zisichukuliwe na vile vile hata orodha kamili imekwishaandaliwa ya wadaiwa hao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mahesabu ya mwaka 2002/2003 yaliyoko *BMT* kutokamilika, Wizara ilikwishatoa maelekezo Mashirika yake yote kukamilisha mahesabu yao kabla ya Kikao cha Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii cha Bunge la Bajeti linalokuja na *BMT* wameishakamilisha, wanategemea kuwasilisha kwenye Kamati katika kikao kinachokuja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana kunyanyaswa na Halmashauri za Miji, Waheshimiwa Wabunge sisi ni Madiwani, kwa kushirikiana na Madiwani wenzetu ndiyo tunahusika katika kutunga hizi sheria ndogo ndogo na kanuni ndogo ndogo ambazo zinaendesha Manispaa na Halmashauri za Miji, huko ndiko ambako tungekuwa tunabanana. Sasa tukishatunga sheria zile, halafu baadaye tunakaa tu na kuiuliza Serikali Kuu kwamba Serikali mna msimamo gani, inakuwa si kutenda haki. Kwa hiyo, yale yote ambayo yanaendelea katika miji mbalimbali ikiwemo na Dar es Salaam, Wabunge wa Dar es Salaam ni Madiwani na Madiwani ndiyo wanaotekeleza hayo. Kwa hiyo, kama wanaona inawafaa hawaoni inatishia kura au vitu gani basi waendelee, lakini vinginenyo ni wakati muafaka wao kukaa katika Halmashauri zao na kulisahihisha hilo kama wanaona ni kosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA M. SIMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha taarifa yetu ya Kamati kwa kuanza kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuongea ni Mheshimiwa Haroub Said Masoud - Makamu Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Khalid S. Suru, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Stephen M. Kahumbi, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Halima Omar Kimbau, Mheshimiwa

Eliachima J. Simpasa, Mheshimiwa Profesa Juma A. Kapuya na Mheshimiwa Shamim Khan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwatambua waliochangia kwa maandishi kuwa ni Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita; Naibu Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu pamoja na Mheshimiwa George Malima Lubeleje; Mbunge wa Mpwapwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao ambayo kwa sehemu kubwa ushauri wao utatusaidia na kuboresha kazi ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi ya kwanza kabisa kuwashukuru Mawaziri ambao wametangulia kwa kunisaidia kujibu hoja mbalimbali. Nimshukuru Mheshimiwa Shamim Khan ambaye ametoa maelezo na majibu mazuri sana kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi hususan kazi kubwa inayofanywa ya ukarabati na uboreshaji wa vifaa vya kufundishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala ya watoto na tatizo kubwa la ukeketwaji na uanzishaji wa Benki ya Wananchi hayo yote yamepata maelezo mazuri katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Profesa Kapuya kwa kazi nzuri aliyofanya katika kutoa maelezo na majibu yaliyojitokeza katika taarifa yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu inathamini sana ushirikiano mzuri tulionao na Mawaziri wetu hawa wawili na kwa kweli wanaturahisishia kazi ya Kamati. Sasa naomba nijibu sehemu zile ambazo nadhani itakuwa vizuri kama nami nikichangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Haroub Masoud kwa mchango wake ambao umeelezea zaidi taarifa yetu ambayo nisingeweza kuisoma yote kwani amefafanua zaidi hasa matatizo makubwa yanayokabili Wizara zetu. Wizara zetu zinakabiliwa na tatizo kubwa la ufinyu wa bajeti. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ambayo ina majukumu makubwa sana inapata bajeti ndogo sana.

Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo ina ufinyu mkubwa wa bajeti hasa ukizingatia kazi kubwa iliyonayo katika Idara ya Ustawi wa Jamii ambayo inashughulikia wazee, watoto yatima, watoto wa mitaani, walemavu na kadhalika, haitiliwi mkazo na Serikali. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kupitia Bunge lako Tukufu ifikirie upya Wizara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya michezo ninaamini kabisa Mheshimiwa Waziri amezungumza vizuri zaidi. Lakini niende kwa Mheshimiwa Khalid Suru, ambaye aliulizia suala la ukeketaji. Kama nilivyosema mwanzo, tumelizungumzia vizuri na tumekuwa tukihudhuria makongamamo kuhusu mikakati ya kumaliza matatizo ya

ukeketaji. Mpaka sasa tumefikia hali nzuri sana kwani karibu wananchi wengi wameshahamasika na wanajua matatizo ya ukeketaji. Hata hivyo, tunawaomba wazazi hasa akina baba wawe mstari wa mbele kukataza jambo hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Suru ametuomba Kamati yetu iweze kutembelea Kondoa katika chuo chake. Kwa niaba ya Kamati yangu nasema tutaangalia hali ikituruhusu tutatembelea huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matatizo ya watoto yamejitokeza sana na yamezungumzwa tena na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Khalid Suru na Mheshimiwa Halima Kimbau. Ninaamini Waheshimiwa wengine wangepata nafasi nao wangezungumza. Suala hili pia Mheshimiwa Waziri ameligusia, lakini ningependa pia niliseme kwa ujumla.

Masuala ya watoto kama ilivyo masuala ya jinsia ni masuala mtambuka, yaani ni masuala *crosscutting,* kwa maana kwamba Wizara mbalimbali zinashughulikia watoto kama vile Wizara ya Elimu inashughulikia kwenye masomo, Wizara ta Afya inashughulikia chanjo na tiba, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo inashughulikia watoto yatima, watoto walemavu na wa mitaani na matunzo ya watoto wa familia zilizofarakana. Aidha, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inashughulikia hasa kuweka sera pana kwa kila mdau katika kuwaendeleza na kuwalinda watoto. Kwa kutilia umuhimu huo, Wizara ina Idara maalum ya Maendeleo ya Watoto.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo sheria ya matunzo ya mtoto na haki nyingine inashughulikiwa na mapendekezo yameshafikishwa ngazi ya juu Serikalini, tusubiri italetwa na tutaijadili kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Jenista Mhagama kuwa, vyuo vingi vimeanza utaratibu wa mafunzo ya muda mfupi. Aidha, taarifa iliyosomwa ni taarifa ya mwaka jana, lakini mwaka huu tumefanikiwa kutembelea vikundi vilivyo vjijini katika Mikoa ya Pwani, Morogoro na Arusha na hali ikiruhusu tutaendelea kufikia vikundi vya vijijini zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kahumbi ametoa kilio kikubwa cha matatizo ya uendeshaji wa Chuo cha Taasisi ya Ustawi wa Jamii. Kamati ilitembelea na maoni ya Kamati yamo katika taarifa itakayosomwa mwishoni mwa mwaka. Hata hivyo, tunaishauri Serikali iweke *vote* yake peke yake kwani hiki ni chuo kimojawapo ambacho kinatakiwa kitendewe kama vyuo vingine vinavyofanyiwa. Kwa hiyo, tutashukuru kama chuo hiki kikipata vote yake peke yake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu ambaye ni Mjumbe wa Kamati na pia ni Waziri anayesubiri, aliboresha zaidi taarifa yetu. Aidha, namshukuru sana kwa ushirikiano wake na kugusia zile sehemu ambazo aliona sikuzitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Halima Kimbau na Mheshimiwa Eliachim Simpasa wameongelea kwa uchungu kuhusu kukatishwa masomo watoto wa kike kwa kupewa mimba. Ninachoweza kusema kwa sasa ni kwamba, Sheria ya Elimu inasema:

"Mtu yeyote anayemkatisha mtoto masomo kwa sababu yoyote ni kosa la jinai." Hata hivyo, kama Waheshimiwa Wabunge tunaona sheria hii haitoshi na imepitwa na wakati tunao uwezo wa kuleta Muswada hapa Bungeni na kutunga sheria kali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa George Malima Lubeleje; Mbunge wa Mpwapwa, amezungumzia ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo na kupatiwa vifaa vya kisasa vya kufundishia. Hili linaendelea na pia walimu wenye sifa wanatafutwa. Kwa hiyo, nadhani asubiri.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nichukue nafasi hii tena kutilia mkazo pale ambapo Waziri alianza kujibu kuhusu michezo. Mimi ningependa kuzungumzia kuhusu *FAT*. Suala la FAT limezungumzwa kwa ukali sana na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Haroub Masoud na Mheshimiwa George Malima Lubeleje. Nadhani na wengine wangepata nafasi wangezungumza hasa kuhusu kuzorota kwa mchezo wa mpira wa miguu kunakosababishwa na uongozi wa *FAT*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ngawaiya alifikia mpaka kusema kwamba hatujafanya chochote na angependa kujua mpaka sasa tumefanya nini. Ningeanza kwa historia tu kwamba, Kamati yangu katika mwezi wa Julai mwaka 2003 ilikutana na Kamati ya Utendaji ya *FAT* ambao tuliwataka viongozi hao ama wajiuzuru au waitishe Mkutano Mkuu, ule ambao ulikatishwa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, haya yalitekelezwa kwa kuitisha Mkutano Mkuu na matokeo yake Kamati nzima ya utendaji ilisimamishwa na kuteuliwa Kamati ya muda, natumaini Waheshimiwa hilo wote mlilifahamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *FIFA,* Tanzania ni mwanachama wa *FIFA*, kwa hiyo, *FIFA* inayo haki ya kusimamia masuala ya soka na pale ambapo kuna matatizo ndani ya wanachama wake ni jukumu la *FIFA* kutatua matatizo kwa lengo la kuendeleza soka.

Mheshimiwa Spika, suala la viongozi wa zamani kurejeshwa madarakani huo ni uamuzi wa wanachama ambao waliwapigia kura kurejesha uongozi huo. Haya ni ya msingi tu.

Waheshimiwa Wabunge, sisi pia tuna kazi ya kuhakikisha na kurekebisha hali hii ya kukaa na wapigakura wa Chama cha Mpira ili wachague uongozi wa *FAT* kwa maslahi ya Taifa. Hawa wapigakura wanatoka kwenye Majimbo yetu, hivyo tunawajibika kukaa nao na kuwafahamisha wafanye kazi nzuri ili watuletee uongozi mzuri. Kwa hiyo, hili ni jambo la Waheshimiwa Wabunge pia. Kwa nia nzuri tu nadhani hawa Wajumbe ambao wanachagua viongozi wanaweza wakatusikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia niseme na kuwatanabaisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, sasa hivi kazi imeanza ya maandalizi ya Katiba mpya na tunaamini

Katiba mpya itakayotungwa inaweza ikasaidia kama na sisi tukitafuta njia zetu za kupeleka maoni yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusomwa na kujadiliwa taarifa yetu, sasa naomba Bunge lako Tukufu lipokee na likubali taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii pamoja na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Mapendekezo Yaliyomo katika Taarifa hiyo ilikubaliwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaeleza mapema, Muswada unaoonekana kwenye *Order Paper* ya leo utawasilishwa saa 11.00 jioni. Kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa hiyo 11.00 na Wabunge wa CCM kama walivyotangaziwa waingie ndani waendelee na kazi yao.

*(Saa 05.19 asubuhi Bunge ilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kodi ya Mapato wa Mwaka 2004
### *(The Income Tax Bill, 2004)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 *(The Income Tax Bill, 2004)* na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote naomba kwa niaba ya Serikali kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Fedha na Uchumi, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge Lupa kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri thabiti ulitusaidia katika kuukamilisha Muswada wenyewe. Aidha naomba kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew Chenge na Wasaidizi wake kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kuandaa Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa kutunga sheria mpya ya kodi. Muswada ulio mbele yenu una lengo la kutunga sheria mpya ya kodi ya mapato badala ya sheria ya

kodi ya mapato namba 33 ya mwaka 1973, inayotumika hivi sasa. Mabadiliko haya ni muhimu ili kuendeleza juhudi za Serikali za kukuza uchumi na kuwezesha usambazaji wa matunda na mafanikio yaliyokwisha patikana katika juhudi zetu za kurekebisha uchumi kwa wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu miaka ya hivi karibuni nchi yetu imeshuhudia mabadiliko makubwa katika sera na mfumo wa uendeshaji wa uchumi wa taifa. Mabadiliko hayo ni pamoja na kuongezeka kwa kasi ya kukua kwa uchumi na pia kuibuka kwa sekta binafsi, kama nguzo muhimu ya kukuza uchumi wetu. Wakati Mheshimiwa Rais, alipolihutubia Bunge mapema mwaka huu alielezea mafanikio mengi yaliyokwisha kupatikana kutokana na utekelezaji wa sera nzuri za Chama Tawala cha CCM. Naomba tu nikumbushe maneno yake kwamba: "Juhudi kubwa inahitajika ili kuongeza kasi ya mafanikio na ili kuyafikisha matunda yake kwa wananchi wengi zaidi tunahitaji kuboresha zaidi huduma katika maeneo muhimu ya kupambana na umaskini yaani kuboresha sana mazingira yatakayowawezesha wananchi wetu kupambana na umaskini ambao ni tatizo kubwa katika taifa".

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hivi karibuni imepitisha Sera ya Uwezeshaji *(Empowerment Policy)* ili itumike kama nguzo mojawapo katika kuwawezesha wananchi kuondokana na umaskini. Aidha maandalizi ya utekelezaji wa mpango wa kuzirasimisha mali na mitaji iliyo katika sekta isiyo rasmi inaendelea vizuri. Lengo la mpango huo ni kuwawezesha wananchi ambao mitaji yao imefungwa katika sekta isiyo rasmi na hivyo kukosa thamani waweze kutumia mitaji hiyo ili kujiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zetu za kusambaza mafanikio yaliyokwishapatikana zinahitaji siyo tu kuendeleza mazingira ya uchumi mpana na utulivu wa kisiasa yaliyotuwezesha kufikia hapa bali pia tutahitaji kutumia fedha nyingi zaidi katika kuweka mazingira yanayotoa fursa kwa wananchi kujiendeleza. Hata hivyo ni dhahiri kwamba mahitaji ya fedha ni makubwa kuliko uwezo wa walipa kodi hivi sasa kutokana na vianzio vilivyopo. Vile vile mafanikio yanayopatikana yanaongeza mahitaji ya fedha ili kuyaendeleza na kuyalinda. Mapato yetu ya ndani bado ni kidogo sana hasa kwa kulinganisha na nchi nyingine zenye uchumi unaofanana na wetu. Sasa ingawa nchi yetu imejenga uhusiano mzuri sana na wafadhili kianzio hiki si cha kutegemea sana kwa utekelezaji wa mkakati muhimu kama huu kwani kinawezakwisha wakati wowote. Hivyo hatuna budi kuongeza juhudi za kuongeza mapato yetu ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa kutunga sheria mpya ya kodi ya mapato unatokana pia na mabadiliko makubwa yaliyotokea Kimataifa katika nyanja za uchumi na biashara tangu sheria ya sasa ilipotungwa ambayo imesababisha sheria ya sasa ya kodi ya mapato ya mwaka 1973 kufanyiwa marekebisho ya mara kwa mara na hivyo kupoteza kwa kiasi fulani mtiririko wake wa awali na kwa baadhi ya maeneo husababisha utata wa tafsiri na hivyo kuathiri utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia bado yako mapungufu mengi katika mfumo wa sasa wa sheria ya kodi ya mapato. Kwa mfano sheria ya sasa imepungukiwa na uwezo wa kutoza kodi vyanzo vyote vya mapato na kudhibiti mianya ya ukwepaji kodi wa kugawa

kwa usahihi mapato yatokanayo na shughuli za hapa nchini mwetu dhidi ya yale yanayotokana na mapato ya nchi nyingine na kati ya walipa kodi tofauti kutokana na biashara kati yao. Kuibuka kwa biashara pepe *(electronic commerce)* kumechangia kuwepo kwa upungufu katika baadhi ya maeneo ya sheria kama vile ukaazi wa mlipa kodi *(residence)* na nchi ambapo mapato yamezalishwa *(source country).* Mapungufu haya na mengineyo husababishwa kukosekana kwa usawa miongoni mwa walipa kodi na pia kuifanya Serikali kushindwa kukusanya mapato yake halali kutokana na wanaotakiwa kulipa kodi za aina mbalimbali. Katika Muswada huu hatua zinazopendekezwa kuongeza usawa miongoni mwa walipa kodi ni pamoja na matumizi ya kanuni za kawaida za kiuhasibu katika kukadiria mapato yanayotozwa kodi, kujumuisha mapato yote kutokana na ajira *(employment income),* biashara *(business income)* na uwekezaji rasilimali *(investment income)* katika wigo wa kodi. Hata hivyo unafuu bado utatolewa katika utozaji wa kodi, mapato kutokana na ajira na yale yanayotokana na biashara katika sekta za kilimo, viwanda na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Muswada. Sasa naomba nizungumzie malengo ya ujumla ya Muswada wenyewe kama ifuatavyo:-

(a) Kubadilisha muundo wa sheria *(re-structuring)* kwa kuweka mpangilio mzuri wa vifungu vya sheria ili vifungu vinavyohusiana vikae sehemu moja. Hatua hii inalenga hasa katika kurahisisha uelewa na matumizi ya sheria yenyewe.

(b) Kuwianisha kanuni za ukadiriaji wa mapato yanayotozwa kodi na zile zinatumika kukokotoa faida au mapato katika hali ya kawaida *(neutralization).*

(c) Kuifanya sheria iwe ya kisasa zaidi *(modernization)* ili kukidhi mahitaji ya sasa na kujibu hoja zinazotokana na mabadiliko ya teknolojia, utandawazi, mbinu za kisasa za uendeshaji biashara na utawala wa kodi *(Tax Administration)*

(d) Kama nilivyoeleza awali sheria ya sasa imefanyiwa marekebisho mengi hata ikawa ni vigumu kuelewa baadhi ya vifungu vinavyotumika ni vipi. Aidha kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wadau kwamba sheria hiyo, haieleweki vizuri kwa kuwa imetumia lugha isiyoeleweka kwa urahisi. Muswada unalenga kurahisisha sheria *(simplification)* na kuwezesha walipa kodi kujikadiria wenyewe kama nilivyoelezea ili kuondoa malalamiko dhidi ya Maofisa wa Mamlaka ya Mapato *(TRA)* na kuziacha sheria za masuala ya kodi, kuchukua nafasi yake katika kukusanya na kudai kodi. Kwa ujumla Muswada unalenga kuongeza kasi ya ukuaji uchumi, kuziba mianya ya ukwepaji kodi, kupanua wigo wa kodi, kuleta usawa, kuboresha mfumo wa kuhasibu mapato yatozwayo kodi na kuweka bayana utaratibu wa ukadiriaji ili kuwezesha walipa kodi kujikadiria wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kubadilisha muundo wa sheria limekidhiwa kwa kubainisha aina tatu za mapato. Mapato kutokana na ajira, mapato kutokana na biashara na mapato kutokana na raslimali. Aidha vifungu vivyohusu wigo wa kodi vimekusanywa katika sehemu moja yaani kifungu cha 5 hadi cha 47 wakati vile vinavyohusu walipa kodi maalum kifungu cha 48 hadi 57 navyo vimekusanywa sehemu

moja. Makundi mengine ya vifungu yanahusu sekta maalum, masuala ya kimataifa, taratibu za kulipa kodi na athari za kutotekeleza wajibu chini ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kuwianisha taratibu za kukadiria mapato linafikiwa kwa sheria kutaka kanuni za kawaida za uhasibu zitumike katika kukadiria kodi. Katika sheria ya sasa hutokea mara nyingi makadirio ya mapato kwa ajili ya kodi yakawa tofauti sana na faida inavyoonyeshwa katika hesabu za mfanyabiashara husika. Hivyo viwango vya uchakavu wa mitambo *(depreciation)* vimelinganishwa na vile vinavyotumika katika mahesabu ya kibiashara. Aidha Muswada unataka mapato kutoka katika vyanzio tofauti yatozwe kodi kwa misingi ile ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mapya yaliyoingizwa katika Muswada kwa lengo la kuifanya sheria iwe ya kisasa ni pamoja na kanuni za utozaji kodi kwa biashara ya kimataifa na kuanzishwa kwa utaratibu wa *self assessment* ambapo mlipa kodi hujikadiria mwenyewe mapato na kodi yake na Mamlaka ya Mapato Tanzania kutakiwa kudhibiti tu. Utaratibu huu utatoa unafuu kwa walipa kodi wanaotekeleza wajibu wao na kuondoa malalamiko ya kuonewa na watumishi wa *TRA*.

Aidha Muswada unazingatia mbinu na taratibu za kisasa za kibiashara ikiwa ni pamoja na kudhibiti matumizi ya mikopo badala ya mitaji *(Thin Capitalization)* kama ujanja wa kuhamisha faida ili kukwepa kodi. Vile vile uwigo wa kodi umepanuliwa kwa kuingiza mapato ambayo yalikuwa hayatozwi kodi katika sheria ya sasa. Kwa mfano baadhi ya mapato kutokana na raslimali *(Investment Income)* hivi sasa hayatozwi kodi.

Sheria mpya inajumuisha mapato yote ambayo hayatokani na ajira au biashara kuwa mapato ya raslimali yanayopaswa kutozwa kodi. Vile vile baadhi ya mapato kutokana na biashara ambayo hayatozi kodi chini ya sheria ya sasa inapendekezwa yajumuishwe na kutozwa kodi chini sheria mpya. Haya ni pamoja na malipo ya kumzuia mtu asifanye biashara fulani au mahali fulani. Hata hivyo bado kuna aina za mapato ambazo hazitatozwa kodi chini ya sheria mpya yakiwemo baadhi ya mapato kutokana na ajira ambayo yameachwa kwa kuzingatia uduni wa kipato cha wafanyakazi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi imefanywa ili Muswada huu uwe mwepesi kueleweka kwa watumiaji. Kama tunavyofahamu sheria ya sasa ni ya zamani na imefanyiwa marekebisho mengi karibu kila mwaka. Aidha sheria ya sasa haizingatii hali halisi ya sasa duniani na imekuwa ni kero kwa watumiaji wote yaani watoza kodi na walipa kodi na kadhalika. Michango ya wadau imesaidia sana katika uandishi ili kupata vifungu vinavyoeleweka. Pamoja na hayo kanuni za matumizi ya sheria yenyewe *(practice notice)* zinaandaliwa ili kuweka bayana maana ya vifungu mbalimbali vya sheria. Pamoja na matumizi hayo ya *practice notice* mlipa kodi asiyeridhika anaweza kulalamika kiutawala kwa mujibu wa sheria hii au kisheria kwa njia za mahakama za kodi yaani Bodi ya Rufaa na Mahakama ya Rufaa za Kodi ili apate hati inayotafutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikishwaji wa wadau katika kuandaa Muswada. Katika kuandaa na kukamilisha Muswada huu Serikali, imeshirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Serikali zote mbili yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar, Jumuiya za Wafanyabiashara, Jumuiya za Wafanyakazi, Asasi zisizo za Kiserikali, Umoja wa Watendaji Wakuu wa Makampuni *(Chief Executive Officers Groups)* Wawekezaji *(Investors Round Table), Tanzania Investment Centre,* Watalaam mbalimbali wa masuala ya kodi, Waheshimiwa Wabunge, Wafadhili, Mashirika ya Fedha na kadhalika. Aidha mimi binafsi na Uongozi wa Wizara kwa nyakati tofauti tulikutana na wawakilishi wa jumuiya hizo nilizozitaja hapo juu, pamoja na Mabalozi wanaoziwakilisha taasisi na nchi zao hapa nchini kwa lengo la kupata maoni yao ili kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa naibu Spika, hata baada ya Muswada huu kusomwa mara ya kwanza Bungeni, mwezi Februari mwaka huu Wizara imeendelea kupokea maoni na hoja mbalimbali kutoka kwa wadau. Wizara ya Fedha iliandaa semina kwa ajili ya Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa lengo la kutoa ufafanuzi kuhusu vipengele mbalimbali vya Muswada huu ambapo tulipata mawazo mazuri ya namna ya kuboresha.

Aidha maandalizi ya Muswada yamefaidika kutokana na michango ya Wadau iliyotolewa wakati wa mashauriano ya wazi na wadau *(Public hearing)* yaliyoendeshwa na kamati ya Fedha na Uchumi siku chache zilizopita. Marekebisho yanayopendekezwa kufanywa katika Muswada kama yalivyobainishwa katika *schedule of amendments* iliyosambazwa ni matokeo ya michango mingi iliyopokelewa na Serikali tangu kuchapishwa kwa Muswada huu rasmi miezi mitatu iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya Muswada. Muswada umegawanyika katika sehemu 11 na unao majedwali matano.

Sehemu ya kwanza inahusu jina la sheria na tafsiri ya maneno yanayotumiwa katika Muswada. Katika maandalizi yalikuwa yamekamilika, inapendekezwa sheria hii ianze kutumika kuanzia tarehe Mosi, Julai mwaka huu 2004 ili kwenda sambamba na mwaka mpya wa fedha wa 2004/2005. Hii ni kwa kuwa lengo la sheria hii ni kuongeza mapato ya Serikali kwa mahitaji ya kibajeti na mengineyo na kwa sababu wadau wote wamekwisha shirikishwa katika kutoa maoni yao yenye hoja za msingi na ambazo zimefanyiwa kazi kikamilifu. Kifungu cha 142 cha Muswada kinafafanua taratibu za mpito kutoka sheria ya sasa hadi kutumia sheria mpya kwa mapato kutokana na biashara sheria mpya itatumika kwa mwaka wa mapato *(year of income)* unaoanza baada ya tarehe Mosi Julai mwaka huu. Kwa hela nyingine za mapato inapendekezwa sheria mpya ianze kutumika kikamilifu tarehe moja Julai 2004. Maandalizi yote yanayohusiana na kanuni za utekelezaji na maelekezo ya tafsiri ya sheria yamekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 2 Muswada ina ibara ambazo zinaweka msingi ya utozaji kodi na kuelezea watu wanaostahili kulipa kodi au kutozwa kodi. Viwango vya kodi na aina za kodi inayopaswa kutozwa. Sheria inayopendekezwa inatoza kodi ya mapato yanayotokana na ajira, biashara na uwekezaji kwenye vitega

uchumi kwa kutumia utaratibu mmoja wa kuhasibu na kukokotoa ambapo vipengele vya sheria vinavyotumika ni hivyo hivyo. Mapato ya ajira yanahesabiwa kama mapato ya mwaka ambayo yanalipwa badala ya kugawa kwa miaka tofauti pale malipo yanapohusu vipindi zaidi ya kimoja. Taratibu za kutathimini malipo yasiyo ya fedha *(benefit in kind)* ziko wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile mapato ya biashara yanatozwa kodi kwa mujibu wa taratibu na kanuni zilizo wazi, ambazo hufanya mapato yanayotozwa kodi kukaribiana na faida ya biashara kiuhasibu. Unafuu wa gharama za uchakavu wa mitambo *(depreciation)* unatolewa kwa kuzingatia muda hali na uwezo wa mtambo kufanya kazi, hivyo kukaribiana na muda halisi wa matumizi ya mtambo, *(economic life).*

Mapato ya ndani na ya nje ya nchi yanakokotolewa tofauti ili kuzuia hasara za biashara za nje kumeza faida au mapato ya biashara za ndani. Mapato kutoka kitega uchumi yanahusisha malipo yote ambayo si ya ajira au biashara ili kuhakikisha kwamba mapato yote yanatozwa kodi. Hasara za vitega uchumi vya nje ya nchi haikubaliki kupunguza mapato ya vitega uchumi vya ndani ya nchi kwa nia ya kulinda uwigo wa kodi wa ndani na kuepusha udanganyifu. Muswada unaweka kanuni madhubuti kusimamia uhasibu wa mapato na matumizi ya hali ya biashara za ndani na za nje hususan za watu au makampuni yanayohusiana *(associate persons).* Kuna taratibu madhubuti za kuzuia uhamishaji wa mapato kwenda biashara za nje au zenye msamaha wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ya Muswada inaweka utaratibu mpya wa uwigo wa kodi katika sehemu hii uwigo wa kodi umepanuliwa kwa kuhusisha mapato yote yatokanayo na ajira, biashara na uwekezaji katika raslimali. Wigo umepanuliwa kwa lengo la kujumuisha yale mapato ambayo hapo awali yalikuwa hayatozwi kodi na yalikuwa hayawezi kutambuliwa kama mapato yaliyoainishwa katika sheria ya sasa. Hii ilitokana na ufinyu wa tafsiri ya mapato katika sheria ya mwaka 1973 na ili kupanua uwigo huo wa kodi maeneo yafuatayo yamehusika.

(i) Kulinda uwigo wa sasa kwa kuziba mianya ya ukwapaji kodi.

(ii) Kudhibiti misamaha ya kodi.

(iii) Kuweka taratibu za kugawa mapato kati ya walipa kodi tofauti kutokana na biashara kati yao.

(iv) Kuingiza vianzio na mapato ambayo awali yalikuwa hayatozwi kodi.

(v) Kutofautisha mapato na gharama halisi ya biashara za ndani ya nchi na za nje ya mlipa kodi mmoja na kuzuia mgawanyo wa mapato kati ya watu wawili wakati inapaswa kuwa ya mtu mmoja *(income spriting).*

(vi) Kutoa upendeleo maalum kwa Sekta za Kilimo, Viwanda na Utalii ambazo zinaonekana kuwa na uwezo mkubwa wa kuubeba uchumi wa nchi yetu na kuongeza kasi ya ukuaji wake.

(vii) Kupunguza gharama kwa walipa kodi kwa kuirahisisha sheria yenyewe ili kuongeza uwajibikaji wa hiari.

Aidha misamaha ya kodi kwa Mashirika ya Dini *(charitable organizations)* itaendelea kuwepo chini ya Muswada huu unaopendekezwa iwapo mashirika hayo yatatimiza masharti yaliyobainishwa katika kifungu cha 64 cha sheria. Kuhusu mamlaka ya Waziri wa Fedha kutoa msamaha, Waziri wa Fedha atatoa misamaha pale ambapo Serikali itakuwa imeelekeza. Kwa misingi hiyo, Waziri wa Fedha atatoa misamaha kwa kufuata kanuni na taratibu zilizowekwa ikiwa ni pamoja na ya sheria za fedha *(Finance Act)* za kila mwaka kwa kuzingatia umuhimu wa maslahi kwa taifa. Ikumbukwe kwamba tayari umewekwa utaratibu madhubuti wa mashauriano baina ya Bodi ya Mamlaka ya Mapato, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Waziri wa Sekta husika na Kamati ya Kodi ya Serikali kabla ya Waziri wa Fedha, kutoa msamaha. Aidha misamaha hii huchapishwa kwenye taarifa rasmi ya Serikali *(General Notice)* ili iwe wazi.

Kwa mfano kati ya mwaka 1996 na sasa maombi yaliyowasilishwa kwa Waziri wa Fedha baada ya kuchambuliwa kwa utaratibu huo ni 12 tu. Kati ya hayo yaliyokubaliwa ni 10. Hivyo tatizo la misamaha linapotoshwa na wafadhili ambao miradi yao ndiyo yenye masharti ya misamaha mikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 4 ya Muswada inahusu aina za walipa kodi wakiwa ni watu binafsi *(individuals),* ubia, makampuni na asasi za dhamana *(trusts).* Kwa kila mmoja kati ya makundi haya sheria inaweka kanuni za watakavyotozwa kodi.

Sehemu ya 5 inahusu utozaji kodi kwa biashara maalum ikiwa ni pamoja na biashara ya bima, mifuko ya akiba ya uzeeni, asasi za hiari na vyama vya wafanyabiashara, *(trade associations).* Kuhusu biashara ya bima mapato kutokana na bima ya maisha yataharibiwa tofauti na mapato kutokana na bima nyinginezo.

Aidha mchango wa mwanachama kwenye mfuko wa akiba ya uzeeni ambao hauzidi kiasi kilichowekwa kisheria kwenye mfuko husika, hautatozwa kodi kwa mwanachama huyo. Vile vile mapato ya mfuko wa akiba ya uzeeni ulio hapa nchini hayatatozwa kodi wakati yale yanayotokana na mfuko wa nje yatatozwa kodi. Asasi za hisani zitatozwa kodi kutokana na mapato yao isipokuwa kama angalau asilimia 70 ya matumizi yatakuwa kwa ajili ya malengo ya hisani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 6 inahusu masuala ya kimataifa. Sehemu hii inafanunua kanuni za ukaazi wa mlipa kodi, namna ya kutofautisha mapato yanayopatikana hapa nchini na yale yaliyopatikana nje ya nchi na unafuu kwa ajili ya kodi iliyolipwa nje ya nchi. Vifungu vya 73 hadi 76 vilivyo katika sehemu hii vinalenga kuziba mianya inayoweza kutumiwa na Mashirika ya Kimataifa kukwepa kodi.

Sehemu ya 7 inaweka utaratibu wa malipo ya kodi ikiwa ni pamoja na tarehe ambapo kodi inatakiwa kulipwa, masharti ya kutozwa kodi ya kuzuia *(with holding tax)* namna ya kulipa kodi kwa awamu na taratibu za kuandaa makadirio *(assessment).* Kifungu cha 94 cha sehemu hii kinataka makampuni kujikadiria wenyewe kodi zao *(self assessment).* Lakini kifungu cha 96 kinampa Kamishna wa Kodi ya Mapato uwezo wa kurejea makadirio hayo iwapo kutakuwa na sababu za kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 8 inajumuisha vifungu kuhusu athari kutotekeleza sheria. Riba itatozwa kwa kuchelewa kulipa kodi au kujikadiria kodi kidogo kuliko ilivyopaswa. Sehemu hii pia inaorodhesha makosa ya jinai, yanayoweza kutendwa kwa mujibu wa sheria hii. Namna ya kukusanya kodi ambayo haikulipwa kwa hiari na mhusika taratibu za kuendesha mashtaka kwa makosa yaliyotendwa chini ya sheria hii.

Sehemu ya 9 ya Muswada inaelezea taratibu za kufuta kodi na urejeshaji wa malipo. Sehemu hii inatoa uwezo kwa Waziri wa Fedha kupitia katika Gazeti la Serikali kufuta kodi, riba au adhabu ya kodi pale anapoona kuna sababu ya kufanya hivyo. Pia inatoa uwezo kwa Kamishna wa Kodi ya Mapato kurejesha kodi ambayo haikustahili kukusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 10 ni juu ya masuala ya utawala wa kodi, sheria inatambua Ofisi ya Kamishna wa Kodi ya Mapato na kuruhusu kukasimu madaraka kwa maofisi walio chini yake. Aidha Waziri wa Fedha, amepewa madaraka ya kutengeneza kanuni *(regulations)* kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa sheria.

Vile vile kifungu cha 130 kinamtaka Kamishna kuandaa maelekezo ya utendaji *(practice notes)* ili kufafanua jinsi vifungu mbalimbali vya sheria vitakavyotekelezwa. Kifungu cha 131 kinaeleza kwamba iwapo mtu atawasilisha taarifa kamili kwa Kamishna kwa lengo la kupata ufafanuzi wa sheria katika suala fulani, ufafanuzi wa tafsiri uliotolewa na Kamishna utasimama kama ulivyotolewa, isipokuwa kama itagunduliwa kuwa mhusika hakutoa taarifa kamili.

Sehemu ya 11 inahusu masuala ya mpito. Sehemu hii inafuta sheria ya kodi ya mapato namba 33 ya mwaka 1973 na vile vile sehemu hii inafafanua kwamba masharti na misamaha ya kodi iliyo katika mikataba na hati za uwekezaji zilizotolewa chini ya sheria iliyofutwa itaendelea kutumika kana kwamba sheria hiyo haijafutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ina majedwali *(schedules)* matano. Jedwali la kwanza linaonyesha viwango mbalimbali vya kodi kwa aina mbalimbali za mapato, jedwali la pili linahusu mapato yanayostahili msamaha *(exempt amount),* jedwali la tatu linahusu viwango vya punguzo la uchakavu *(capital allowances)* wa raslimali na mitambo mbalimbali. Jedwali la nne linaorodhesha masuala yatakayohitaji matumizi ya namba ya kuandikishwa ya mlipa kodi *Tax Payer Identification Number (TIN).* Jedwali la tano linabainisha thamani ya matumizi ya gari la mwajiri ambayo itatozwa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho katika Muswada. Muswada unaowasilishwa mbele yenu umefanyiwa marekebisho mbalimbali kwa kuzingatia maoni

ya wadau yaliyotolewa tangu ulipochapishwa na kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza.

Naomba nieleze baadhi ya mabadiliko hayo ambayo yameelezwa kwa kina katika orodha *(Schedules of Amendment)* ambayo nimesambaza hivi punde. Posho za wafanyakazi, ili kuondoa utata katika tafsiri ya sheria, Muswada sasa unatumia neno yale yale yanayotumika katika sheria ya sasa ya kodi ya mapato kuhusiana na utozaji kodi katika posho wanazolipwa watumishi. Hii ni kwa sababu lugha iliyotumika awali ilitafsiriwa kana kwamba Serikali inakusudia kutoza kodi posho zilikuwa hazitozwi kodi chini ya sheria ya zamani ikiwa ni pamoja na posho za safari kwa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla chini ya sheria ya zamani na mpya posho inatozwa kodi isipokuwa kama ni fidia kwa gharama zinazohusiana na ajira. Gharama za aina hiyo ni pamoja na posho ya kujikimu safarini na zinazohusu huduma kwa Majimbo ya Wabunge. *(Makofi)*

Hivyo, posho ya Jimbo na nyingine wanazolipwa Waheshimiwa Wabunge, hazitatozwi kodi. Aidha, thamani ya nyumba ya mwajiri ambaye ni Serikali au Asasi ambayo mapato yake yanatokana na Bajeti ya Serikali, haitatozwa kodi.

Thamani ya mali ya kurithi, awali Muswada haukuweka wazi namna ya kutathmini mali itakayorithiwa ili kutoa unafuu wa gharama kwa warithi wanapotaka kuiuza baadaye. Sasa inapendekezwa Sheria ieleze wazi kwamba, thamani ya mali kama hiyo itakuwa ni ile unayoweza kununulia katika soko *(Market Value),* siku inaporithiwa.

Mapato kutokana na matumizi na gari la mwajiri, hapo awali Muswada ulilenga kutotoza kodi mapato ya mtumishi kutokana na matumizi binafsi ya gari la mwajiri. Sekta binafsi imeleta mapendekezo kwamba, hatua hiyo itawaumiza waajiri wanaogharamia marupurupu hayo. Kwa hiyo, sasa inapendekezwa kuwa, msamaha wa mapato ya aina hiyo uwe ni kwa watumishi wa umma, ambao mapato yao au ya waajiri yanatokana na Bajeti ya Serikali.

Marekebisho yamefanywa pia ili kusahihisha makosa kadhaa ya uchapaji kama ilivyobainishwa katika jedwali lililosambazwa.

Kama nilivyoelezea hapo awali, kutokana na mapungufu mengi yanayojitokeza katika sheria ya sasa ya Kodi ya Mapato na marekebisho yanayokusudiwa, ni dhahiri kwamba, Sheria mpya inahitajika ili kurahisisha ukusanyaji, usimamizi na ulipaji wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. NJELU E. M. KASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kutoa maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, kuhusu Muswada wa Kodi ya Mapato wa mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, baada ya kuchambua na kuujadili Muswada wa Kodi ya Mapato wa mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 70(ii) Toleo la mwaka 2004, naomba sasa niwasilishe maoni ya Kamati kuhusu Muswada uliotajwa hapo juu, ambao sababu kubwa na maudhui yake ni kufuta Sheria ya Kodi ya hivi sasa iliyotungwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka 1973. Muswada huu una lengo la kuunda upya mfumo wa kutoza kodi, kuboresha usimamizi wa kodi na kuondoa mapungufu na kuzuia udhaifu na kupanua wigo wa kukusanya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza na kuiunga mkono Serikali kwa kuleta Muswada huu hivi sasa kwani malengo yake yanakuwa ni kichocheo cha kuifanya nchi yetu kwenda na wakati husan katika kipindi hiki cha mabadiliko mengi katika uchumi wetu. Kamati yangu kwa nyakati mbalimbali, ilipata fursa ya kuujadili Muswada huo ambapo kati ya tarehe 23 mpaka 27 Februari, 2004 Kamati ilihudhuria Semina iliyoendeshwa na Wizara ya Fedha, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato, iliyofanyika katika Chuo cha Kodi Mjini Dar es Salaam.

Semina hiyo ililenga katika kuwaelimisha Wajumbe wa Kamati kuhusu maudhui na madhumuni ya Muswada. Aidha, kati ya tarehe 5 na tarehe 8 Aprili, 2004, Kamati ilifanya vikao na wadau mbalimbali ambapo walitoa maoni yao kuhusu Muswada, ambayo kwa kiwango kikubwa yaliisaidia Kamati katika kuishauri Serikali jinsi ya kuboresha Muswada huu na baadhi ya marekebisho yaliyotokana na kazi hiyo ndiyo ambayo yamesambazwa hapa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mijadala yote hiyo, Kamati ilipata kuelewa upana juu ya madhumuni na malengo ya Muswada yanayolenga katika kuupanua wigo wa ukusanyaji kodi, kuboresha usimamizi na mifumo ya ukusanyaji mapato na unaojenga mazingira mazuri ya uwekezaji na pia kuiwezesha Sekta hiyo isiyo rasmi, kuingia katika wigo wa kulipa kodi na kuziba mianya ya kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao cha pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kilichofanyika jana usiku, yaani tarehe 20 Aprili, 2004, Kamati ilipitia vifungu vya Muswada ambapo baada ya majadiliano, Kamati ilipitisha Muswada pamoja na mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa na Kamati yaliyolenga katika kuuboresha Muswada ambayo kimsingi Mheshimiwa Waziri aliyakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuafiki Muswada wa Serikali, Kamati ilikuwa na maoni kama ifuatavyo: Pamoja na makusudio mazuri ya Muswada huu, bado upo umuhimu mkubwa sana kwa Serikali kuweka mikakati na programu ya muda wa kati

na muda mrefu wa kuongeza mbinu za kuongeza upanuaji wa wigo wa ukusanyaji kodi na vile vile kupanua wigo wa walipa kodi.

Serikali iunde chombo au *Task Force* itakayoainisha na kuratibu programu endelevu iliyotajwa hapo juu, itakayokuwa inatathmini utekelezaji wa Sheria tunayoiunda kwa kuitolea maoni ya kuiboresha mara kwa mara ili iweze kuleta maendeleo ya umma wa wananchi ambao wanatafuta maisha yao nje ya sekta ya uchumi na kupanua wigo wa kodi ili kujiepusha na kuendelea kutoza kodi watu wachache na makampuni yao. Kwa kuzingatia haya ni vema kuangalia kinachokusudiwa katika kuweka wigo wa kodi ya mapato na yenye shabaha zifuatazo:-

Moja, kuongeza makusanyo ya kodi kutoka kwa waajiri wachache wanaojulikana kwenye wigo finyu, yaani hapa ni pamoja na wafanyakazi. Kwa sababu maadam wafanyakazi wanafahamika mahali walipo na mishahara yao inafahamika, basi Serikali inajielekeza kila wakati kwenda kuwatoza kodi wale wale badala ya kwenda kuwatafuta na wengine ambao pia wanayo mapato. *(Makofi)*

Pili, kuweka usawa wa haki kwa makundi mbalimbali ya walipa kodi. Hii ina maana kwamba, licha ya wafanyakazi ambao wanajulikana ni vema sasa ikaenda kuwatafuta na wengine wenye shughuli zao mbalimbali na hasa wenye uwezo mpana na matajiri, walipe kulingana na uwezo walio nao.

Tatu, kusaidia kuongeza ajira na mambo mengine yanayolenga maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri si vema mfumo wa kodi kuishia katika kukusanya tu mapato ya Serikali. Ni lazima pia ukidhi mahitaji ya watu na utekeleze sera ya Taifa. Suala la kuwaingiza wananchi katika mashindano ya kiuchumi na kibiashara ya Taifa letu na nchi nyingine, linahitaji maandalizi na mipango mipana ya kuwaendeleza na kuwawezesha wananchi wetu. Kamati inashauri Serikali ilete programu ya uwezeshaji na pia itungwe Sheria kwa ajili ya utekelezaji wake, bila ya kuwa na programu nzuri ya uwezeshaji na itakayosimamiwa vizuri, Watanzania walio wengi watashindwa kuhimili mikiki mikiki inayoambatana na utandawazi. *(Makofi)*

Wazo la kuwa na programu kuwawezesha Watanzania, limekuwapo tangu mwaka 1997 na mwaka 2002 Wabunge walifanyiwa semina ya suala hilo. Lakini hadi leo haijulikani nini kinaendelea katika suala la uwezeshaji. Wakati umefika suala hili litekelezwe sasa. Lengo la kuleta uwezeshaji ni kupanua wigo wa mapato kwa sababu watu wengi watakavyoingia kwenye uchumi wa kisasa ndivyo walipa kodi watakavyoongezeka na ndivyo mzigo wa kuwabebesha wafanyakazi peke yao utakavyozidi kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa upendeleo maalum kwa Sekta ya Kilimo, Viwanda na Utalii, kupitia Muswada huu. Ni matumaini ya Kamati kwamba, wawekezaji wa nje na ndani, watatumia nafasi hii kuwekeza kwa

wingi katika Sekta hizo. Sekta hizi hasa kilimo na viwanda ni muhimu sana katika kufanikisha mkakati wa kuondoa umaskini hapa nchini kwetu.

Kamati inashauri Serikali kuwa makini katika kuwachuja na kuwapata wawekezaji wote wa ndani na nje ili kuepukana na wawekezaji matepeli kwa kuwa na miongozo itakayoainisha stahili zote za kumpasisha mwekezaji kuwa *strategic investors.* Baadhi ya wawekezaji ambao tayari tunao wameonekana kuwa sifa zao hazitoshi kuitwa *strategic investors.* Kamati imebaini nyingi ya benki zilizopo hapa nchini, zina malimbikizo makubwa ya fedha ambazo hazizunguki katika uchumi wa nchi yetu.

Aidha, kutokana na masharti magumu ya ukopeshaji, wengi wa wananchi wetu wanashindwa kukopa na pia wawekezaji wa nje kupendelea kukopa kutoka katika mabenki ya nchi za nje ambako riba na viwango viko chini. Masharti mengine nafuu, Kamati inashauri Serikali kwa kushirikiana Benki Kuu ya Tanzania kuangalia Sera zetu za fdha na uchumi ili kuondokana na tatizo hili la fedha kurundikana katika mabenki na wafanyabiashara hawawezi kuzikopa.

Kamati inashauri pia ni vema Sheria iwe na mtazamo utakaokuwa na uwiano mzuri wa kutoza kodi kwa wafanyakazi wanaoiangalia na hali halisi ya mapato ya ajira. Huduma za jamii na jinsi zinavyoathiri uwezo wa kufanya ili kuwawezesha wafanyakazi hao kuishi vizuri na kumudu maisha yao baada ya kukatwa kodi. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kukiangalia kipengele cha *Threshold,* yaani kiwango cha chini kabisa cha kutoza kodi kipandishwe angalau kifikie shilingi milioni moja kwa mwaka. Nafurahi kusema kwamba, tulipojadiliana suala hili kwenye Kamati, Waziri alisema kwamba, atalitazama wakati wa Bajeti kwenye *Finance Bill.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, wakati wa kupokea maoni kutoka kwa wadau *(Public Hearing),* wadau wote walisema wanaihitaji sheria mpya ya kodi na kwamba, Sheria ya sasa imepitwa na wakati. Wadau walisisitiza tu kwamba, kuna ibara na baadhi ya vipengele katika Muswada vinahitaji kubadilishwa na ndiyo baadhi yake vimeendelea kufanyiwa marekebisho. Ni jambo la kupongeza kuona kuwa tangu Muswada huu ulipotangazwa mara ya kwanza Septemba, 2003, wadau wengi wametoa maoni na Serikali kila ilipoona maoni ya wadau yana mantiki, iliufanyia mabadiliko Muswada. Wakati wa kuupitia Muswada katika Kamati hii marekebisho zaidi yalifanywa ikiwa ni pamoja na kufuta ibara ya 7(ii)(b), ambayo ilikuwa inalalamikiwa sana na wadau. Ibara hii ilikuwa inakusudia kutoza kodi aina zote za mapato kama vile *subsistence allowance, leave allowance,* pango, gharama za maisha na kadhalika na kadhalika. Nadhani Waziri alikuwa analielezea hapa kwamba sasa limeondolewa. *(Makofi)*

Aidha, gharama za mwajiri kusomesha na kuwapa mafunzo wafanyakazi wake sasa zitahesabiwa kama sehemu ya gharama ya uendeshaji kampuni. Hii itakuwa ni motisha kwa waajiri kuweza kuwasomesha Watanzania. Muswada pia unatofautisha mkopo toka nje ya nchi na amana. Riba inayotokana na mkopo itatozwa kodi *(Withholding Interest)*, lakini riba inayotokana na amana haitatozwa kodi. Kamati inaitaka Serikali ieleze vizuri suala hili lipate kueleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majadiliano ya kina yaliyohoji maeneo mbalimbali ya Muswada na baadaye Mheshimiwa Waziri akisaidiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuyatolea ufafanuzi wa kuridhisha, Kamati iliupitisha Muswada wa Serikali pamoja na marekebisho ambayo yamesambazwa hapa leo ndani ya Ukumbi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, Wajumbe wa Kamati yangu na wale wasio Wajumbe, ambao walifika kwenye Kamati, kwa michango yao. Kwa kiwango kikubwa michango yao imesaidia sana kuuboresha Muswada wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kwa majina yao kama ifuatavyo: Kwanza ilikuwa ni mimi mwenyewe, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Raphael Chegeni Masunga, Mheshimiwa Lephy B. Gembe, Mheshimiwa Edson M. Halinga, Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail, Mheshimiwa Dr. Hassy H.B. Kitine, Mheshimiwa Stanley H. Kolimba, Mheshimiwa Mwanamkuu Makame Kombo, Mheshimiwa Prof. Simon M. Mbilinyi, Mheshimiwa Talala B. Mbise, Mheshimiwa Raphael N. Mlolwa, Mheshimiwa Juma Omar Juma, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Kilontsi M.M. Mporogomyi, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Hasnain M. Murji, Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mheshimiwa John L. Mwakipesile, Mheshimiwa Venance M. Mwamoto, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Suleiman A. Sadiq, Mheshimiwa Issa Mohamed Salim, Mheshimiwa Iddi M. Simba, Mheshimiwa Margareth J. Bwana, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono na Katibu wetu Ndugu James Waburg. *(Makofi)*

Wote nawashukuru sana kwa kazi nzuri walioifanya. Nawashukuru pia wadau wote waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao. Kamati ilifaidika sana na maoni yao ambayo pia yamechangia katika kuboresha Muswada. Miswada ya Kodi ni migumu na hivyo siyo rahisi kuondoa matatizo yote katika hatua hii ya awali. Kama *UDASA* walivyosema katika mada waliyotuwasilishia, *Tax Laws are highly technical and sometimes artificial.*

Kwa hiyo, baadhi ya mambo kadri tulivyopendekeza yataendelea kufanyiwa majumuisho na Wizara hadi hapo Sheria itakapokuwa sasa inakidhi mahitaji ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew Chenge, Katibu Mkuu wa Wizara, Dr. Grey Mgonja, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato, Ndugu Kitillya, pamoja na Maafisa wao, kwa kuisaidia Kamati kufanikisha kujadili na kupitisha Muswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU (k.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(v)(c), Toleo la 2004, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Kodi ya Mapato wa mwaka 2004 *(The Income Tax Bill, 2004).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Msemaji wa Wizara hii, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada huu wa Sheria ya Kodi ya Mapato wa mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umekuja kipindi muafaka, wakati Taifa letu la Tanzania linatafuta kila njia ya kuwa na uchumi wake huru na kuacha kutegemea sana misaada kutoka nje. Ni matumaini yangu pesa zitakazopatikana kutokana na hatua hii, zitasaidia zaidi katika vita dhidi ya UKIMWI na njaa na umaskini kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unalenga kuongeza wigo wa kodi na utaweka mazingira mazuri ya uwekezaji na vile vile kuiwezesha sekta isiyo rasmi kuchangia zaidi kwenye kundi la walipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mwananchi na mlipa kodi, sipingi wazo la Serikali la kutaka kutafuta njia za kuongeza mapato yake, ila Kambi ya Upinzani ina maoni yafuatayo kwa ajili ya uboreshaji:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna umuhimu wa kuwasamehe watumishi wa umma, ambao kwa kweli bado mapato yao ni madogo ukilinganisha na watumishi wengine wa sekta binafsi wanaopata mishahara mikubwa. Vile vile posho za safari wanazopata kwa kweli ni kidogo mno ukilinganisha na hali halisi ya gharama ya malazi, chakula na matumizi mengine ya dharura. Watumishi wa chini wanalipwa kiasi cha Sh. 20,000 kwa siku na Maofisa Sh. 30,000 na Wakurugenzi, Makatibu Wakuu na Waheshimiwa Wabunge Sh.40,000. Hii inaonyesha kwamba, waathirika wakubwa ni watumishi wa Serikali wa ngazi za chini na pia si rahisi kupata hizo safari mara kwa mara. Hata kama atapata *allowance* ya kuwa nje ya kituo cha kazi, pato zima kwa mwaka halizidi Sh. 600,000, ambalo ukigawa kwa miezi 12 atapata Sh.50,000, ambacho ndicho kima cha chini. Lakini pamoja na hayo tunamshukuru Waziri kwa kuondoa kodi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali inaonyesha mpaka hivi sasa walipa kodi waaminifu wa nchi hii ni wafanyakazi walioajiriwa katika sekta rasmi. Utafiti uliofanywa na *UDASA* kuanzia mwaka 1990 mpaka hivi sasa, unaonyesha wafanyakazi wa sekta hii wanachangia kati ya asilimia 45 na 50 na sekta ya viwanda inachangia kati ya asilimia 25 na 30 kwa mwaka. Ukiongeza Muswada wa Sheria wa kuanzisha Taasisi na Bodi ya Utoaji na Ulipaji wa Mikopo wa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu *(The Government Student's Loans Bill, 2004)*, mzigo mkubwa utakuwa kwa watumishi hawa ambao watatakiwa kuanza kulipa hiyo mikopo sambamba na utozaji wa kodi mpya utakaoanzishwa katika utaratibu huu. Kwa Muswada huu wa Sheria ya Kodi kama

utakamilika kuwa Sheria kamili, hakuna sababu ya kuwaongezea mzigo mwingine wa kodi kinyemela.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine la utozaji kodi kwa mauzo ya nyumba moja binafsi, kwa kweli mara nyingi mtu anapouza nyumba anakuwa na shida. Kwa hiyo, kumtoza kodi itakuwa ni kumwongezea matatizo mwananchi huyo aliyeamua kuuza nyumba yake. Kwa hiyo, ni vema basi Serikali ikatoza mauzo ya nyumba moja binafsi katika maeneo ya miji na siyo vijiji na vile vile huko mijini kuwe na baadhi ya maeneo. Kwa mfano, kwa Dar es Salaam kama vile Mikocheni, Upanga, *Oysterbay* na maeneo mengine, lakini siyo maeneo kama Manzese, Tandika na kwingineko. Maana huko ndiko wanakokaa walala hoi wengi wa nchi hii na vile vile maeneo haya mengi hayajapimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 82(ii) kinachohusisha *Withholding Tax on Interest,* ningependa kushauri kwamba, kiendelee kutozwa kodi ili kuchochea *local borrowing* na ku-*discourage foreign borrowing.* Zoezi hili liende sambamba na kuweka mazingira mazuri ya benki zetu kushusha riba ili watu waweze kukopa kwenye mabenki hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 10 kinachohusu misamaha ya kodi katika Muswada huu wa Sheria ya Mapato ya Kodi, Kambi ya Upinzani inaomba kupata maelezo ya ziada kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwani nchi hii huko nyuma ilishakumbwa na dhahama ya Waziri kutoa misamaha mingi kiholela na kusababisha Serikali kupoteza mapato yake. *(Makofi)*

Tusingependa Waziri apewe mianya ya kuendeleza utoaji misamaha kiholela. Kambi ya Upinzani haikubaliani na makato hayo kwenye vipengele vifuatavyo: Kipngele cha 7(ii)(a),(b) na (c) na kipengele cha 7(iii)(b)(d). Kwa sababu mapato hayo ni muhimu kwa mfanyakazi huyo ili aweze kuishi maisha ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninaendelea kupata wale wanaoomba kuchangia mpaka sasa wapo 14 na *list* bado haijafungwa kwa mtu ambaye angependa kuchangia. Kwa hiyo, kwa yeyote ambaye anaomba ajue jina lake, lipo kwenye orodha. Sasa orodha imepangwa kwa kadri tulivyopata karatasi za maombi. Sasa nitawaita wale wa kwanza, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Abu Towagale Kiwanga, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, hawa wanne wa kwanza wajiandae. Sasa namwita Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia mtu wa kwanza, ingawa ni Muswada mzito ambao unastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii iliyopo mbele yetu asilimia 100 kwa 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Wabunge wenzangu, ambao wamechaguliwa kwa nyadhifa mbalimbali kama ifuatavyo: Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, kwa kuwa Marais wa kutuwakilisha Tanzania sehemu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Waziri wa Fedha, kiungo cha maisha ya Watanzania. Pia nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu. *(Makofi)*

Baada ya pongezi hizo, ninaomba nianze kuchangia kama ifuatavyo: Kwa kweli nilikuwa na mengi sana ya kuweza kuchangia lakini kwa mtazamo huu na uwazi na mtandao aliokuwa ameutoa Mheshimiwa Waziri, nitakuwa na machache ya kuchangia kwa sababu asilimia kubwa ya Muswada huu, Kamati ya Fedha na Uchumi, imeweza kuuchambua kwa kina yale ambayo tungeweza kuyachangia Wabunge wote. *(Makofi)*

Nisiwe mchoyo wa fadhila kwa kutokumshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, iliyochambua Muswada mpaka saa 4 za usiku. Kwa kweli huu Muswada pamoja na kwamba nimeupitia sehemu nyingi, niliguswa na sehemu kuu mbili: Sehemu ya kwanza ilikuwa ni maslahi ya ajira ya wafanyakazi wa Kitanzania ambao hali zao ni za chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania hawa wameweza kuchangia, hawa ambao ni wafanyakazi wameweza kulipia kodi zao za utumishi kwa kipindi cha miaka 30 wakati wakiwa katika hali ngumu ya maisha bila kuwa na ubabaishaji au ulalamikaji wa aina yoyote, wameweza kuchangia kwa kipindi chote hicho. Sasa basi pamoja na kwamba, wamepitia utaratibu mzima wa kodi hii, ajira ya watumishi ambao kipato chao ni kidogo ukilinganisha na maisha ya sasa hivi ambayo tumeingia kwenye uchumi na teknolojia ambayo ni ngumu sana kwa maisha ya Mtanzania aliyokuwa nayo kwa hivi sasa, ningeomba Mheshimiwa Waziri, ambaye nimempa utukufu wa mwanzo kabisa, aweze kuliangalia upya suala hili la kodi ya wafanyakazi bila kujali kwamba huyu ni mfanyakazi wa aina gani, kwa sababu hii yote inagusa mfanyakazi wa Kitanzania, ambaye amefanyakazi hiyo ya kuchangia kodi hiyo kwa miaka yote 30.

Sasa basi, kwa kuwa sasa hivi tuko kwenye kipindi cha kuboresha uchumi wetu na kuondoa umaskini, ni vema kodi hizi zikaelekezwa kwenye masuala nyeti kama vile kodi za migodi ambayo tayari ni uchumi wetu ambao tunao mkononi. Viwanda ambavyo vimefufuliwa sasa hivi na kupata wawekezaji ili Watanzania wote wafaidike na mapato ya kuinua uchumi wetu ambao wanausikiliza tu kwamba, Tanzania iko katika hali ya juu kimapato au imeongeza uchumi wake. Lakini matunda yake ni yepi, ili waweze kuguswa na faida hiyo ni vizuri na wao wakafaidi matunda kwa kuondolewa kodi kama hizo zinazowagusa wananchi wa chini ambao kipato chao hakiridhishi na bado ni maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, pia napenda nichangie kidogo suala zima la hawa wawekezaji. Wawekezaji wakubwa ambao wanastahili kulipa kodi hiyo wako Dar es Salaam, ndio wengi lakini pia kuna msamaha wanaweza kusamehewa wakapanga taratibu za kulipa kodi, mathalani wakalipa nusu au

wakapunguziwa kufuatana na hali ya maisha ilivyo, lakini pia ningemwomba Mheshimiwa Waziri, aangalie wale wawekezaji ambao wako nje ya Dar es Salaam. Kwa mfano, kuna wawekezaji ambao wanaweza kuwekeza Dodoma, Mtwara, Tabora, hawa wawekezaji hawawezi kushindana na wale ambao wako Dar es Salaam, ambao tayari wameshajizatiti kwa sababu kila mwekezaji anataka kuwekeza Dar es Salaam.

Sasa kodi hii pia ingekuwa ni vizuri ikaangalia wale ambao wanataka kuwekeza nje ya Dar es Salaam, inawasaidiaje ili waweze kuhamasika, kuvutika kwenda kuwekeza nje ya Dar es Salaam au nje ya Arusha, Mwanza, ili na watu wengine waweze kufaidika na uwekezaji huu kwa sababu sasa hivi tunausikia kwenye mabomba tu, kwenye magazeti, vitabu kama hivi tunavyopitisha, wawekezaji wameongezeka lakini utamwambia aje kuwekeza Tabora, itakuwa sio rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako, naomba nitoe mfano mdogo tu, Kiwanda cha Zuzu Dodoma, nilikwenda mimi pale kama Mjumbe, mwekezaji yule ameacha mali yote, la kwanza gharama zake ni kubwa, pili, hakuna soko la kuuza zile *tiles* ambazo ni nzuri, mashine zake ni nzuri na bado mpya, sasa huyu mtu ameogopa kwamba akiendelea kuwekeza mle ina maana hatapata soko la uhakika na mtaji wake umekwisha, yule mwekezaji akakimbia bahati mbaya sina jina lake. Tulipokagua mle ndani tukakuta mali iliyopo ni *tiles* hizo hizo zinazoagizwa kutoka nje zikipitia Dar es Salaam, Dar es Salaam zipo sasa huyo mtu akiangalia gharama za kusafirisha kutoka hapa Dodoma kupeleka Dar es Salaam, bado atakutana na *tiles* nyingine kama mnavyosema, utandawazi. Sasa huyu mwekezaji tunamlindaje ili aweze kuja huku na tunampangiaje kodi zake ili iweze kueleweka, tunamsaidiaje mtu huyu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mdogo tu, Tabora tumepata tabu kubwa ya kutafuta wawekezaji wa Kiwanda cha Nyuzi, yote hiyo ni pamoja na hayo kwamba, mtu akiangalia gharama zake hizo nyuzi atauza wapi na akiangalia kodi imembana atapumulia wapi? Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, pamoja na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, ni bora na ni vizuri tukaangalia sehemu kama hizo ambazo ni nyeti, ikiwezekana Serikali ichangie hata umeme kwenye viwanda kama hivyo, ikiwezekana Serikali iangalie jinsi gani ya kupunguza kodi kwenye viwanda kama hivyo ili tuweze kuwavutia hata Watanzania, watu wengi wana uwezo wa kuweza kufufua viwanda au kuingia ubia lakini wanashindwa kulingana na kodi. Maana yake sasa hivi tunazungumzia wawekezaji, je, hawa Watanzania tunawasaidiaje kwenye viwanda vyao, kwenye miradi yao, kwenye mikopo yao, kwa sababu kuna Watanzania wana mikopo mikubwa sana hapa nchini lakini wanashindwa na kama alivyosema yeye mwenyewe, Mheshimiwa Waziri kwamba, kuna wengine wanashindwa kukopa pesa, wanaogopa watafanyia biashara gani wakati kodi inawabana. Namwomba Mheshimiwa Waziri, ayaangalie masuala haya kwa kina kwa pande zote ili tuweze kwenda sambamba na hayo tunayoyatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, Muswada huu nilikuwa na mengi ya kuchangia, niliandika karibu nusu ya kurasa nyingi tu, lakini kwa jinsi Mheshimiwa Waziri alivyofanya uchambuzi wa kina, nadhifu, imebidi niishie tu kumwonea haya na

kumwomba na kuendelea kumpongeza na namalizia kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyotangulia kusema wenzangu, nawapongeza Mheshimiwa Balozi Mongella, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mheshimiwa Dr. Pius Ngw'andu, kwa nyadhifa zao mpya walizozipata na hivyo kutuletea sifa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja, lakini naomba pia nichukue nafasi hii, kuwapa pole wapiga kura wangu wa Kilombero hususan Kijiji cha Magombera, kwa mafuriko yaliyotokea na kuwa mimi niko pamoja nao na kuwa ninajaribu kushirikiana na vyombo vingine vya Serikali ili kuweza kupata ufumbuzi wa tukio hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri wa Fedha na watendaji wake wote, kwa kuleta Muswada huu hivi sasa. Nimepitia sehemu zote Kumi na Moja za Muswada huu na kuona kuwa lugha iliyotumika ni nyepesi zaidi kuliko ile iliyotumika kwenye Sheria Na.33 ya mwaka 1973. Mtiririko wa zoezi zima la ukusanyaji wa kodi umepangwa vizuri zaidi, suala la mageuzi ya kiuchumi wa nchi pia yameelekezwa vizuri kabisa, suala la ubinafsishaji na uwekezaji limeelezwa vizuri kwenye Ibara mpya za Muswada huu kuanzia Ibara ya 30 - 35. Pia Muswada huu umeangalia kabisa taratibu ya *Fair Trade Practices* hususan kwenye Ibara ya 33. Jambo lingine kubwa ambalo Muswada huu umeleta ni kwenye Sura ya 10, Ibara ya 130 na 131, pale inapozungumzia *Private Practices* pamoja na *Private Ruling,* kitu ambacho hapo awali kilileta utata mkubwa kati ya mabingwa wa kodi na wale watoza kodi na wakusanyaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Muswada huu kuwa mzuri, una mapungufu yake. Ibara ya 35 imempa uwezo Waziri au Kamishna pale anapobaini kama kuna njia na taratibu za kukwepa kodi, ili yeye mwenyewe na taratibu nyingine aweze kurekebisha yale mapato ambayo yana utata.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu mwingine ninaouona, huu Muswada haukuangalia kwa kina kidogo taratibu za kuwawezesha walipa kodi ili waweze kukua na hivyo kutuwezesha sisi kama Serikali, kuwa na uhakika wa kudumisha viwango vya kodi tulivyokusanya na hatimaye kuwezesha hayo makusanyo kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Ibara ya 35, nashauri kuwa Waziri na wahusika wengine, waangalie utaratibu wa kuandaa *schedule* nyingine ili iweze kuweka sehemu zile ambazo zinaweza kuwa ndio mianya ya ukwepaji kodi. Mfano, tuzungumzie tu kama tulivyozungumza kwenye ule Muswada mwingine wa *Employment and Labour Relations Act* ya mwaka 2003, tulizungumzia tofauti ya mishahara kati ya Mtanzania na mtu wa nje. Tulipata kwenye michango ya watu wakati huo wakizungumzia kuwa kuna Mtanzania *Engineer* wa Madini, ambaye alikuwa anapata mshahara wa Sh.900,000

wakati Mcanada anapata mshahara wa Sh.5,000,000, tofauti ya mishahara ya watu hawa wawili ni karibuni Sh.4,100,000.

Sasa basi kama kweli tutafanya *Fair Trade Practices,* mshahara wa *Engineer* mwenye ujuzi sawa na huyu Mcanada utiliwe maanani. Kama Sh.900,000 ndio mshahara wenyewe basi Sh.4,100,000 ungefanyiwa kazi kikodi ili uweze kutozwa kwa sababu tukiachia hivyo hiyo hela itaruhusiwa kama matumizi ya kampuni na hivyo kuinyima Serikali mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano kwenye Sh.900,000 kodi ambayo atatozwa huyu mfanyakazi ni chini ya Sh.200,000 huyu anayepata mshahara wa Sh.5,000,000 kodi yake ni kama Sh.890,000 lakini kama Sh.4,100,000 ni ziada ambayo haiko kwenye soko, basi tunapoteza kodi karibuni ya Sh.1,200,000. Pia tukiangalia mwelekeo tuliouleta kwenye suala la *Anti-dumping,* juu ya malighafi zinazoingia, basi nadhani hiyo pamoja na vingine vinaweza kutupa uwezo wa kuweza kuongeza wigo zaidi wa kodi na hivyo kuliongezea pato Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati tunafanya hayo, lazima tuwe na watu ambao wana uwezo sawa kabisa na hawa watu wa nje ambao tunajaribu kuwazuia ili tuweze kuleta ajira kwetu sisi na pia kuheshimu mikataba tutakayoingia na hao wawekezaji na pia kuheshimu mikataba ya kikodi na nchi zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezeshaji ambao ndio upungufu mwingine wa mwisho ni kuwa bila kumwandaa mlipa kodi kuwa na *Tax Compliance* na kuwa na uwezo wa kuweza kuzalisha kodi zaidi, basi hizi kodi ambazo tunazikusanya sasa hivi hazitaweza kukua. Najaribu hapa kukumbuka tu kwamba, Sheria ya Kodi ya Canada ilizungumzia kitu kimoja tu kwenye aina za walipa kodi, mlipa kodi wa kati mwenye mtaji mdogo alikuwa akiruhusiwa aweze kulipa kodi ndogo zaidi akuze mtaji wake mpaka kufikia kiwango fulani ndipo atozwe kodi kama mtu mwingine.

Sisi pia tungeweza kuangalia kwenye mtazamo huo, kwa kumruhusu aingize vyombo, mitambo na vitendea kazi, ambavyo vitaweza kumzalishia hela zaidi ili aweze kupanda kutoka kwenye daraja ya mlipa kodi wa kawaida, mlipa kodi wa kati na wa juu ili sisi tuwe na uhakika wa kupata kodi nyingine zaidi baadaye. Najua kabisa Idara yetu ya Kodi ya Mapato, inafanya hilo kwa kuelimisha lakini kuna kila sababu ya kuhakikisha kuwa, tunawaandaa walipa kodi ili waweze kutupa kodi zaidi na kwa urahisi na wenyewe bila kuona kama wanadhulumiwa ili watambue kuwa ni wajibu wao kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo kidogo ni tofauti lakini ni muhimu ni juu ya haya Makampuni ambayo yameingia nchini na kuwekeza, ni kuwa kujaribu kwa taratibu ya kodi hii kuwafanya wawe *Public Companies* hapa nchini. Uwekezaji wao kwenye *Stock Exchange* nyingine badala ya hii *(DSA)* nchini inaweza kabisa kutuharibia sisi kwa kutoa mitaji kwenda nje na hivyo kutunyima sisi nafasi ya kupanuka.

Mfano mzuri kabisa ambao umeshatokea ni *Tanzania Breweries. Tanzania Breweries* wamekwenda wameuza *share* zao na sasa hivi wanalipa kodi si chini ya

shilingi bilioni 95 nchini na viwanda vingi vimepanuka na watu wengine wamewezeshwa ili Serikali kuweza kupata kodi zaidi.  Kwa hiyo, ushauri wangu ni kuwa, tujaribu ikiwezekana hawa wenzetu ambao wamekuja kuwekeza, wawekeze pia kwenye *Dar es Salaam Stock of Exchange* badala ya kwenda kuweka New York na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ninaomba kabisa tuwe makini hasa kwenye lile wazo nililotoa kwenye *Section 35* ya *Commissioner* kuweza kutoza kodi kwa kuandaa jalada jingine kwenye *Transitional Provision*, Sehemu ya 11 ili tuwe na sehemu ambazo tunaweza kuongeza mapato zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nashukuru kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. KIDAWA H. SALEH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kutoa mkono wa pole kwa Mheshimiwa Rais na Mama watoto wake, Mama Anna Mkapa, kwa kadhia iliyowafika ya kuunguliwa na makazi yao.

Aidha, nachukua nafasi hii, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa na Mheshimiwa Prof. Dr. Pius Ngw'andu, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mawaziri wa Elimu wa Afrika, nawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya marekebisho yaliyoletwa hapa leo, mchango wangu utakuwa mdogo sana katika Muswada huu tunaoujadili sasa hivi. Naanza kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao una nia ya kufuta ile Sheria ya Mwaka 1973, ambayo ilikuwa imejaa viraka tele na inakuwa vigumu kusomeka na kufahamika hasa kwa watu kama sisi ambao hatuna elimu ya kisheria. Kwa hiyo, wameliona tatizo hili na wameandaa Muswada mpya kwa kufuta udhaifu huo na vile vile Muswada ambao unaweza kupanua wigo wa kodi na kuwezesha kukusanya mapato mengi zaidi kuliko ambayo yanakusanywa hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa kuwa kianzio cha Kodi ya Mapato sio kianzio kidogo katika mapato ya Serikali. Kwa takwimu za mwaka 2002, Kodi ya Mapato inachangia karibu 23% na zaidi ya mapato yote yanayotokana na kodi. Kwa maana hiyo, kodi hii ni lazima iongozwe na sheria ambayo itakuwa madhubuti na haina viraka kama ilivyokuwa ile sheria ya mwaka 1973.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kodi ya Mapato inamgusa mlipa kodi moja kwa moja kwa vile inapunguza kiwango cha fedha ambazo anaweza kutumia *(Disposable Income),* kwa maana kodi hii inauma zaidi kuilipa kuliko ile kodi ya bidhaa ambayo mlipa kodi analipa kodi lakini wakati ule ule anapata bidhaa anayoihitaji. Kwa maana hiyo, kodi hii inatakiwa itolewe elimu ya kutosha kwa walipa kodi. Naelewa *TRA* ina utaratibu mzuri wa kutoa elimu kwa walipa kodi lakini nasisitiza tu kwa sababu kama kodi haitaeleweka italeta matatizo na manung'uniko na watu kuikimbia na kuikosesha mapato Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya vipengele tu nilikuwa naomba ufafanuzi. Kwa mfano, kipengele Na. 6(1) ambacho kimeainisha vizuri tu kuwa *Tax Base* ya kodi ya mapato ni kutokana na ajira, biashara na uwekezaji raslimali na ikaainisha vizuri tu baina ya mlipa kodi ambaye ni raia *(resident)* na mgeni *(non-resident)*. Imeainishwa kuwa *non-resident* atatakiwa kulipa mapato kutokana na vianzio hivyo kutokana na *source* ya mapato ya humu nchini Tanzania lakini mlipa kodi ambaye ni raia atatakiwa kulipa kodi *irrespective* ya *source* yake kuwa inatoka Tanzania au siyo Tanzania.

Kwa hiyo, naomba nipate *clarity* kwamba, je, kama ni Mtanzania amewekeza nje ya Tanzania mfano ana biashara zake Kenya au Uganda na anapata mapato yake kule, yeye mwenyewe anaishi Tanzania na anaingiziwa mapato yale kwenye akaunti yake Tanzania, Mtanzania huyu atapaswa kulipa *Income Tax* na kama atapaswa kulipa ni kwa misingi gani? Naomba Mheshimiwa Waziri aniweke sawa kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Section 35(1)* inazungumzia mambo ya *Tax Avoidance Arrangement* na kwamba *Commissioner* anapoona au anapodhani kuwa kuna *arrangement* imefanywa na mlipa kodi kwa makusudi ya kupunguza kulipa kodi yake au kwa kukwepa kulipa kodi, yeye anaweza kufanya marekebisho. Hapa ni sawa lakini la kuangalia ni kwamba, *Tax Avoidance* sio suala la uhalifu isipokuwa tu yule mlipa kodi anakuwa *smart enough* kuangalia kwenye sheria ya kodi kuna *loopholes* za aina gani na anaweza kuzitumia kwa manufaa yake yeye mwenyewe. Kwa hiyo, tuziangalie vema hizi sheria zetu sizije zikawa zinatoa mianya kama hiyo na tukiona kama kuna hiyo mianya zifanyiwe *amendment* haraka haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka kuna kipindi fulani kule Zanzibar kulikuwa na Sheria ya *ZIPA* iliyowekwa *Tax Holiday* kwa wawekezaji kwa miaka mitatu mpaka mitano. Ikitokea kila ikimalizika miaka mitano, hakuna kodi inayolipwa kwa sababu ikimalizika ile miaka mitano mmiliki anakuwa mwingine kwa hiyo, mmiliki anaweza kufanya *arrangements* labda na mwanaye, yeye ni *Mr. X* amemiliki kipindi hicho cha miaka mitano ya mwanzo inapofika wakati wa kulipa kodi basi utakuta mmiliki sasa ni *Mr. X1,* kwa hiyo, inakuwa ni *chain* na tunaweza kukosa mapato ya Serikali. Kwa hiyo, hili liangaliwe hata katika hizi sheria zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *Section 80(1)* imeelezea kuhusu uwekaji wa kumbukumbu kwa ajili ya kuamua *tax payable* kwa mlipa kodi. Kuna walipa kodi wajanja wanaweka kumbukumbu za aina mbili, moja ni kwa ajili ya kupeleka kwenye *Tax Authority* na nyingine ni kwa matumizi yao ya ndani. Kuna *incident* moja ilishatokea kule, ambayo naikumbuka kulikuwa na *business entity* ambayo mmiliki wake ni mgeni vile vile na Mhasibu wake alikuwa ni Mtanzania, mbinu hizo zilikuwa zinafanyika. Siku moja yule Mhasibu uzalendo ukamjia akasema hapana hii haitaendelea kwa hiyo akajaribu kuifichua hii siri, walipokuja wakusanya kodi akatoa ile kumbukumbu ambayo ni sahihi ambayo inawezesha kukusanya kodi ambayo inatakiwa. Yule jamaa ilim-*cost* ajira yake na hakukuwa na *means* ya kumrudisha yule kazini kwa sababu yule mwajiri ni mgeni kwa hiyo amemwachisha kazi kabisa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nakuomba

ujaribu kuweka kipengele katika sheria hii ambacho kitabana hili lisitokee katika kodi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi zaidi kwa sababu nilikuwa na mengi ya kuongea katika hii *schedule* ya kwanza *page 129* lakini baada ya *amendments* zilizotolewa hapa, sitokuwa na zaidi, lakini naipongeza Serikali kwa kufikiria kufanya marekebisho katika hii *schedule* kwa sababu ilivyo hivi sasa, wafanyabiashara wadogo wadogo wakiwemo akina mama, mama ntilie na wengine, watapungukiwa na huu mzigo wa kulipa kodi. Hii inaonyesha hasa ile dhamira ya Serikali ya kupunguza umaskini wa kipato kwa wananchi wake. Kwa hiyo, kina mama hawa sasa hivi watajihakikishia mapato wanayoyapata wanatumia na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDULLATIF H. ESMAIL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi nampongeza Waziri wa Fedha, wataalam wake, Naibu Mawaziri, *AG,* pamoja na Kamati ya Fedha, kwa kuujadili Muswada huu ambao ni mgumu sana mpaka tukafikia leo tumeuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Income Tax Act* ya sasa ina miaka 30, imeshakuwa *very old,* imepitwa na wakati. Huwezi kufanya kazi ya kesho kwa kutumia mbinu za jana. *I do not believe you can do today's job with yesterday's method and be in business tomorrow especially in this globalised era and free market system. (Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakumbusha tu *the rule of justice and fairness in taxation.* Kwa mfano, kulikuwa na mtoto mmoja aliyefiwa na baba yake, mama yake alikuwa na shida ya hela, akaandika barua kwa Mwenyezi Mungu, *Dear Sir God, please send me hundred dollar.* Akampa jirani yake ambaye alikuwa *Income Tax Officer.* Yule bwana alivyoona imeandikwa *Dear God* akafungua, akaona imeandikwa vile baada ya wiki akamtilia dola 20 akampelekea. Yule mtoto akafurahi sana kwamba, Mwenyezi Mungu amemjibu barua yake. Baada ya wiki yule mzee akapata barua nyingine akaisoma imeandikwa *Dear Sir God*, *please give me 100 dollar but this time don't pass through this Income Tax Officer he debited 80% from my money before.* Kwa hiyo, nakumbusha *tax to please not tax to kill (Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *to collect more taxes then absolutely necessary is a legalized robbery. Income Tax Act, 2004 is the modernized tax system, introduction* ya *self-assessment, is great step forward,* naiunga mkono, *I support it very much. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tulipokuwa tukijadili Muswada huu katika Kamati ya Fedha, Ndugu yangu Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, aliyasifu maji ya Dodoma, nikamwambia kaa kimya wahusika wa kodi watakuja kuyaongezea kodi haya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakusanya kodi wasijihusishe na kukusanya kodi tu, waangalie namna ya kuongeza walipa kodi. *They should think the way how to increase the number of tax payer not merely the collecting of taxes. The more the taxpayer the more the collection, the more the better the social service, the more the stable Government.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi leo wana *degree* ya *B.A, MBA, Ph.D,* lakini bahati mbaya hawana *job,* kazi hawana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mr. Andrew Young, Meya wa Atlanta, Mmarekani Mweusi, amewahi kusema kwamba, *people are not poor because they are dumb or because they are lazy but because society has not provide opportunity.* Tuwape fursa wafanyabiashara ndogo ndogo ya kujiendeleza na sio kuwapiga magongo na kuwanyang'anya bidhaa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Machangudoa wametushinda kuwaondoa Dar es Salaam tuwape ruksa ya kufanya biashara...

**MBUNGE FULANI:** Watozwe kodi.

**MHE. ABDULLATIF H. ESMAIL:** Biashara ya halali ina baraka. Mwenyezi Mungu anasema katika *Qur'an* Tukufu: *"Hala-Allahu Baiya-wa harama riba",* tumehalalisha biashara na tumeharamisha riba. Hawa ni maskini na ndugu zetu, wazee wetu, watoto wetu na kadhalika na watalipa kodi. *Jesus of Nazareth* amesema katika Yohana 12:8: "Maskini mtaendelea kuwa nao" hatuwezi kukataa ukweli huu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *the powers of Minister responsible for investment and Minister for Finance to grand specific incentive to strategic investor should grand further in this new Act,* mimi naunga mkono kwa sababu *delays are dangerous*. Kila tukisema mpaka kila kitu kiletwe Bungeni, tutakosa mambo mengi, Makamishna *they should exercise the power that they have been given by the law.* Misamaha yote iko wazi na inaweza kuonekana katika *website www.tra.tz.go Tanzania Government, there is full transparency* hakuna mtu anayedanganywa. *Anything delayed will get further delayed* tunatakiwa kuwa Wazalendo kwa suala la kulipa kodi japokuwa hakuna uzalendo wa kujiongezea kodi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nawakumbusha wakusanya kodi wazingatie haki za binadamu zisikiukwe, kwa mfano, ilitokea ajali ya *construction accident* Panama, watu wawili walijeruhiwa vibaya, Waandishi wa Habari wakasema *two people were seriously injured one was an English Men the other was the labourer. (Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina shida na Muswada huu na nautakia kila la kheri na ninauunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kabla sijamwita Mheshimiwa Felix Mrema, nieleze tu kwamba, sasa orodha imefikia watu 23, kwa hiyo, ninapopata makaratasi ya sasa hivi, kwa vyovyote vile wataendelea kesho.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mimi kutoa mchango mdogo. Kwa sababu hii ndiyo mara yangu ya kwanza, baada ya Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere kuchaguliwa, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuchaguliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge. Namkaribisha katika jengo hili, aliwahi kuwa hapa kwa kupitia Jimbo langu la Arusha. Bahati nzuri harakati zangu za kuja hapa zikamfanya yeye aje achaguliwe na Mheshimiwa Rais, kuingia hapa kwa njia nyingine hiyo aliyoingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika. Nitumie pia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Katibu Mkuu, Ndugu Mgonja, Mkurugenzi Mtendaji wa *TRA,* pamoja na maafisa wote walioshughulika kufanya kazi hii kubwa na ya aina yake ya kuleta Muswada huu mbele ya Bunge hili Tukufu. Mimi kwa sababu nilikuwa mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, niipongeze Kamati yetu ya Fedha na Uchumi, kwa kazi kubwa na ya kina, waliyofanya ya kuuchambua Muswada huu, kuratibu maoni ya wadau wote walioitikia wito wetu wa kuja kutoa mawazo yao na ushauri wao wa kutusaidia sisi kuweza kuifanya kazi yetu ya kuboresha Muswada huu. Wote walioshiriki nawapongeza, nasema mmefanya kazi yetu iwe rahisi zaidi kuifikisha hapa ilipofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nimefarijika sana kwamba baada ya kazi yote hiyo iliyofanyika, mapendekezo yote yale yaliyotolewa sehemu kubwa ya yale tuliyoyapokea na kuyakubali yamekubaliwa na Serikali na yakaoanishwa katika mapendekezo yao ya *amendments* walizowasilisha mchana huu kwenye Bunge hili Tukufu. Sasa yote hayo yanaashiria na kudhihirisha kwamba, Serikali ilikuwa tayari kupokea mapendekezo mazuri yaliyotoka kwa wadau na Kamati ya Fedha na Uchumi ya kuboresha mfumo mzima huu wa kodi ya mapato nchini. Hakuna aliyeburuzwa, kila hoja ilipewa nafasi ya kuelezwa na kufikiriwa kwa uzito wake na baada ya kazi hiyo nzima tumefika hapa tulipofika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa mchango wangu kwa kusema licha ya matatizo madogo madogo ya Muswada wenyewe, kwa ujumla mimi naungana na wenzangu kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, kuunga mkono Muswada huu mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu mwelekeo wake ni kuanza kukubali ile dhana ya kutoza kodi kwenye *total income* ya mlipa kodi na uioanishe hiyo na *total*

*expenses* ya kuzalisha yale mapato ya mlipa kodi. Sasa ukiangalia mwelekeo huo, inategemea sana *the filing of returns* na *filing of returns* inategemea sana *record* yako ya shughuli zako za mwaka mzima, *income* iliyoingia na gharama ulizobeba katika kuzalisha *income* hiyo iliyoingia. Sasa sio walipa kodi wote au siyo wananchi wote wana *culture* ya kuweka *record* zao za mwaka mzima. Kwa hiyo, tuna kazi kubwa ya kuanza kujenga utamaduni wa kuweka *record* zetu za mapato na za *expenses* ambazo tuna-*incur* zitakazotegemewa kuja kuondolewa kwenye hiyo *income* ambayo tutakuwa tumeivuna. Sasa hiyo kazi ya kuelimishana sio ndogo, ni nzito na lazima Serikali kama walivyosema wenzangu, waje na mikakati ya kuelimisha walipa kodi wajibu wao ni nini katika kuanza kuingia katika mfumo huu ambao unategemewa katika Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi binafsi nimefurahishwa zaidi na ule mfumo ambao upo katika *sections* za 91, 92 mpaka 97, nao ni huu utaratibu wa kujikadiria mwenyewe kodi *(Self Assessment).* Sasa huu utaratibu wa *self assessment* nimefurahi kabisa kwamba, Serikali imepokea ushauri na mapendekezo yetu kwamba, uwahusishe zaidi makampuni na zile taasisi zilizosajiliwa na wale walipa kodi binafsi ambao wataamua kwa hiari yao wenyewe, kuingia katika mfumo huu wa *self assessment.* Ilivyokuwa kabla ya Serikali kukubali haya mapendekezo yetu, ni kila mmoja ambaye alikuwa na sifa ya kulipa kodi, alitakiwa aingie kwenye huu mfumo wa *self assessment* na maana ya kuingia kwenye mfumo wa *self assessment* ni kwamba, tulikuwa tunatakiwa kila mwaka tuwe na tabia ya ku-*file income tax returns.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi ikanitia wasiwasi kwamba, kama tukiwahusisha, sina matatizo kabisa kwamba makampuni na taasisi zilizosajiliwa zinatakiwa ku-*file returns* kwa sababu wao wamezoea ku-*file retuns.* *Accounts* zao ni *audited* na kila mwaka wana-*file returns* ambazo zinawakilishwa kwa Msajili wa Makampuni, kwa hiyo, hiyo *culture* ya ku-*file returns,* makampuni yetu yamezoea kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, sikuwa na wasiwasi na kwamba huku ku-*file income tax returns* haukuwa mzigo mkubwa kwa kampuni na taasisi zilizosajiliwa. Wasiwasi wangu ulikuwa ni kwa hawa walipa kodi wengine binafsi ambao hawana utaratibu huo wa ku-*file returns,* wao wanangojea tu kodi iwe *assessed* halafu wanailipa, siyo wao wenyewe waji-*assess* halafu wampelekee Kamishna kumwambia sisi tunavyoji-*assess* kodi hii ndiyo tunatakiwa kulipa mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na wasiwasi kwamba, tusiende kwa haraka kuwafikia hao na kuwawajibisha wa-*file the income tax returns* kabla wao wenyewe hawajaenda *through the process* ya kuelimishwa kuelewa maudhui na masharti ya *self assessment and filing of income tax returns* ili waelewe kwamba, wanapo-*file* ile *returns* huko mbele ya safari wakija kukutwa kwamba kuna tatizo ya kile walichoki-*file,* kuna kuwajibika kisheria. Sasa nasema tufanye taratibu, tusite, tusiende kwa haraka kuwafikia hawa. Sasa nashukuru kwamba, Serikali imelipokea hilo na imefanya mabadiliko ya kuhakikisha kwamba hawa tunakwenda nao taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna upande mwingine wa hii dhana ya *self assessment.* Upande mwingine ni wajibu wa *TRA,* maana katika ule mfumo wa nchi zilizoendelea wanaheshimu sana *income tax returns* ambazo zimekadiriwa na walipa kodi

wenyewe, wanaziheshimu sana na ni mara chache sana *it is more by way of an exception rather than a rule* kuhoji *income tax returns* ambazo zinakuwa *filed.* Sasa hapa ndiyo wajibu wa *TRA* ili *culture* hii ikolee na kukubalika hapa Tanzania na mimi nashauri na nawasihi tuisukume nchi yetu ili walipa kodi wengi katika nchi yetu wawe ni walipa kodi ambao wanajituma wenyewe ku-*file the income tax returns* na kuji-*assess* wenyewe kwamba hii ndiyo kodi ambayo sisi kama Watanzania, wenye uchungu wa maendeleo ya nchi hii, tunatakiwa na tunastahili kuilipa, isipokuwa tu pale ambapo kuna *gross cases* za *dues, gross* za *float, TRA* watuamini. Najua kuna shida ya kuwaamini walipa kodi, lakini lazima tuanze kujenga hiyo *culture* ya kujaribu kuwafanya walipa kodi hawa waaminike na wapende kujituma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo la *self assessment,* niendelee kusisitiza mengine muhimu katika Muswada huu. Kweli kwenye kodi za wafanyakazi, nakiri na Waziri amekiri kwamba, huyu mfanyakazi ndiyo tumemfanya Mnyamwezi wetu wa kubeba sehemu kubwa ya kodi ya Taifa hili. Mfanyakazi ndiyo analipa kwa sababu yeye yupo pale, yuko tayari kushughulikiwa, hana njia ya kukwepa, kwa hiyo, tumembebesha sehemu kubwa ya mzigo mkubwa wa kodi. Sasa Waziri amekiri, kwa hiyo ni mategemeo yangu kwamba, katika bajeti inayokuja, atakuja sasa kwenye *Finance Bill,* atatuonyesha kwa njia ambayo ni endelevu, mikakati yake ya kumpunguzia huyu mfanyakazi mzigo huu mkubwa wa kodi ambayo anaendelea kubeba. Huyu mfanyakazi anabeba mzigo wa *direct taxes* na *indirect taxes* anazobeba ni kubwa sana na yote hayo yanahimiliwa na huo mshahara wake tu, hana njia nyingine ya kuhimili mzigo huo wote anaobeba wa *direct taxes* na *indirect taxes.* Sasa ni mategemeo yangu kwamba, Waziri wa Fedha wakati wa Bajeti atakuja na hiyo mikakati ya kumpunguzia huyu mfanyakazi mzigohuu mkubwa ambao anaendelea kuubeba, kwa kubeba sehemu kubwa ya kodi za Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi ni hili la kupanua wigo. Tunalisemea sana na tumelisemea sana kwenye Kamati, lakini Waziri alitutia moyo kwamba, kuna mikakati aliyonayo atakayotuletea wakati wa bajeti, tunaingojea kwa hamu lakini mimi nijaribu kutoa tu maeneo mawili ambayo nafikiri ayatilie maanani na aje na mikakati wakati wa bajeti, nayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeelezea kwenye Kamati hii *excess liquidity* ambayo ipo ndani ya nchi, ambayo haitumiki kwa ajili ya kupanua wigo kwa ajili ya uwekezaji. Sasa ni vizuri zile *financial institutions* zitafutiwe njia ya kupewa *tax credits* ili ziwahamasishe wao kuelekeza ile *excess liquidity* waliyonayo kwenye maeneo hasa ya kilimo na pili, kwenye *real excess business* kwa sababu mimi napenda kuamini kwamba, haya maeneo mawili, *real excess business* na hizi *excess liquidity,* zikielekezwa kule zinaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa kabisa kupanua wigo, kuongeza ajira na kufanya uchumi wetu ukue kwa kiwango kile ambacho tunataka ukue cha zaidi ya asilimia nane, tisa mpaka kumi. Sasa ni mategemeo yangu kwamba, Mheshimiwa Waziri, atakuja na mikakati hiyo ya kuhamasisha hii *excess liquidity* iweze kuelekezwa kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kuna hili suala la *practice notes,* ni mategemeo yetu kwamba, *practice notes* hizi zitakazotolewa na Kamishna, zitatolewa kwa lugha ambayo inaeleweka lakini kubwa zaidi Wabunge watapata nakala ili tuweze kufanya kazi ya kuwaelimisha wapiga kura wetu, nini maana na maudhui ya Muswada huu kwa lugha ambayo wapiga kura wetu na walipa kodi wetu, wataeilewa na itawahamasisha wao kushiriki kwa kikamilifu zaidi, kuchangia mchango wao wa kulipa kodi ambazo wanatakiwa kulipa katika Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kabla kengele haijalia, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami nieleze kidogo niliyonayo. Kwanza, sina mengi ya kusemea isipokuwa napenda nimshukuru sana Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kwa kweli kila akisimama kueleza kitu pamoja na kwamba haonekani kuwa ni mtu mrefu au amesimama, maneno yanayotoka pale yanaonyesha kina chake ni kikubwa. Namshukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naiomba Serikali imsaidie huyu bwana. Mimi nakubali ana mwono wa mbali, kwa hiyo, imsaidie. Tunapozungumza juu ya kupanua wigo, tunapanua wigo namna gani maana hawa wafanyakazi tulionao tunaowatoza ni hawa hawa, bado hatujapanua wigo. Suala la sera tuliyozungumza miaka yote na haijafika katika utekelezaji ndiyo njia pekee ya kupanua wigo kwa kuwawezesha hawa wa hali ya chini, wakulima wadogo wadogo, wapate msaada wa kuwezesha uchumi wao. Benki zetu ziwawezeshe hawa mikopo ili wazalishe zaidi na ndipo watakapoingia kuchangia katika uchumi wa nchi hii na kulipa kodi ya kutosha. Lakini vinginevyo hatutafanya lolote, tutaendelea kukamua wale wale wachache na manung'uniko yatazidi, tunafikiri tunasawazisha kumbe tunazalisha tatizo la kutopeleka uchumi wetu katika hali nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna sababu ya kuchelewesha sera hii isifike kuwa sheria na itekelezwe kwa dhati kwani ndiyo ukombozi wetu. Tunazungumza kuwaachia hawa wageni wawekeze humu na kuwapa nafuu sana ya kodi, lakini hawa wana lengo la kuchuma hawawezi kuwekeza kwa kutuletea uchumi, sisi kama tunavyotarajia. Watawekeza ili wanufaike wao zaidi, wabebe waende kwao waendeleze kwao. Sasa na sisi lengo letu liwe ni kuwekeza kwa hawa watu wa chini, wakulima wadogo wadogo, wafanyabiashara wadogo wadogo, hata hawa Wamachinga wawezeshwe kwa kutumia viwanda vyetu hata vidogo vidogo, wachukue mazao yale au matokeo ya wanachozalisha watembeze humu, yaani kitokane na viwanda vyetu, ndicho kitakachosaidia viwanda vyetu vikue na vipate soko. Sasa akina mama wanasuka nguo, vikapu na havina soko, nani avitembeze sasa? Tuwape nafasi hawa wavitembeze humu humu. Hii itatusaidia kuinua hali ya uchumi zaidi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia upendeleo katika kilimo, si suala la kusema tupendelee kwa maneno tu haitawezekana, tunahitaji vifaa, tunahitaji mbolea ili kuwezesha kuzalisha kwa kiwango kinachotakiwa. Sasa vitu hivi lazima tuhakikishe

vinakuwa na bei ya kumwezesha huyu mtu maskini amudu kununua, aweze kuvitumia na aweze kuzalishia. Tusipofanya hivi bado hatujamwezesha huyu mtu na hii sera ya uwezeshaji tulikwishaitangaza kwa watu na watu wanatushangaa, hawa watu walitangaza kitu ambacho hakipo! Tunaomba Serikali ichukue hatua za dharura na za haraka kuwezesha uwezeshaji wa hawa wananchi wetu waweze kuleta uchumi na kuzalisha tunavyotegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo tunachozungumzia ni kile cha kuwapa watu mwanya wa kuzalisha. Kuna vitu vingine vinarudisha nyuma uchumi wetu kama kilimo hiki cha pamba. Ni vizuri tukaangalia, Serikali iangalie hivi pamba Chunya inakatazwa kwa nini, Mbeya kwa nini, Usangu kwa nini? Ni kitu gani kinazuia pamba? Kama mdudu wanayemsema Malawi yuko na Malawi wanalima pamba sisi tumeshindwaje? Sasa tukikaa hapa bila ujasiri wa kukabili mambo tutazidi kufukarika na tutazidi kujaa maneno yasiyoleta tija hata kidogo. Vitu vingine ni kuamua kukabiliana navyo na kubanana na matatizo yale yanayotuzuia tusifanikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninaloliona mimi ni hii sheria yetu, hawa wenzetu wakusanya kodi, wasikusanye kodi kwa vitu ambavyo havijampa mtu wasaa wa kuonyesha mafanikio. Lipo tatizo kubwa linalofanya watu mara nyingine washindwe kujituma na kujitoa. Leo unalipa kodi, unakwenda kununua kitu bei yake ni kubwa haina udhibiti hivi tunafanyaje? Tunawapaje watu *morale* ya kufanya kazi? Ni lazima Serikali iwe na utaratibu wa kudhibiti bei ili kuwapa watu wasaa wa kutulia na kuzalisha bila matatizo ya mawazo ya kukosa maisha yao na kuendeleza hali yao. Serikali hilo ilidhibiti na hata hawa wanaouza madukani tulikwishasemka huko nyuma kwamba, kila mtu aonyeshe bei ya bidhaa zake mle, aandike pale. Ile ilisaidia sana kuona kwamba anachouza mtu bei inaeleweka na wakaguzi wa *TRA* wanapokwenda wanaona bei zipo, ni halali na zinawapa watu moyo, lakini sasa hakuna tabia hiyo. Mtu anajiletea kitu anauza bei anayotaka kwa kuona *scarcity* ya kitu hicho.

Sasa kama tunakwenda hivi hatutapata manufaa yoyote katika kufanikisha kudhibiti hali yetu ya biashara na bidhaa zetu. Sukari ya Kilombero tunasema isaidie kuongeza uchumi wetu hapa, leo sukari hii ipo kwenye shilingi mia nane kwa kilo, lakini nenda Tunduma mpakani, sukari inayotoka Zambia ipo kwenye shilingi mia tano au mia sita, hivi maana yake nini? Unaifanya hii sukari ya Kilombero ilete maendeleo kweli, nani atumie sukari hii ya Kilombero ambayo ni balaa kwa mtu wa hali ya chini kabisa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya ndiyo mambo Serikali iwe inadhibiti ili kuwapa watu nafasi ya kuona kwamba kweli wanalindwa na wawe huru kutumia kile walichonacho kwa kujua kwamba kitaleta mafanikio na kinakwenda. Naomba hii idara ya Kodi, orodha kama ilivyo katika jedwali la kwanza la Muswada huu, inayoonyesha kwamba kiwango cha kulipa kiasi hiki ni mapato ya kiasi hiki, ingetolewa kila mahali na hii itasaidia sana kuwapa imani wafanyabiashara Vijijini kwa sababu wataona orodha na kwamba yeye katika biashara yake anaangukia kwenye orodha gani. Lakini tukisema tu watu waende wakisiwe au waende wajikadirie, hakuna atakayejikadiria kwa hasara, kila mtu atajikadiria kwa faida. Kwa hiyo, orodha hizi zitolewe mtu wa kiwango cha shilingi

milioni tatu kodi yake ni hii, mwenye *grocery* yenye thamani ya shilingi milioni saba kodi yake ni hii, mwenye duka kubwa la vifaa lenye thamani ya shilingi milioni mia mbili kodi yake ni hii, kila mtu ajione ameangukia wapi na ukwepaji hautakuwepo. Vile vile na hawa wafanyabiashara wasisitizwe kuwa na risiti za kununulia vifaa wanavyouza katika maduka yao. Hii itatusaidia sana na haitakuwa na ukwepaji wala kuleta matatizo katika kukadiria kodi na kukusanya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ninashukuru sana na nampongeza sana Waziri na jumuiya yake na kwamba naunga mkono hoja hii na ninawaomba wenzangu tuiunge mkono ili Muswada huu uwe sheria, utusaidie kwa kweli katika kupunguza baadhi ya matatizo yanayotukabili na uwezeshe sera ya uwekezaji ipate nguvu na itusaidie kuongeza wigo wa walipa kodi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nitoe maoni machache. Kwa kuwa niliwahi kuhudhuria kwenye Kamati wakati tukiwa Dar es Salaam, kwa hiyo, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kunikaribisha na nimepata maoni mengi ya wadau. Lakini wale wadau kule Dar es Salaam niliwagawa katika maeneo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wadau ambao wanashiriki katika kusimamia masuala ya kodi katika nchi hii na vyombo vya sheria vinavyosimamia katika kurekebisha mambo ya kodi. Wadau wengine walikuwa ni wale walipa kodi wenyewe. Sasa niliwauliza ninyi walipa kodi ni wadau au ni wahanga, wakasema sisi ni wadau. Kwa hiyo, neno wadau linatumika vibaya kwa maana ya kwamba, mdau ni yule ambaye ana-*share* katika maeneo hayo. Sasa nikawauliza ninyi ni wadau? Wakasema tuitwe hivyo hivyo. Kwa hiyo, tukawaita wote ni wadau, lakini wamesaidia kweli kweli kufanya marekebisho. Katika marekebisho wenzetu walifanya kazi za kupona na kupona, hakuna kufa na kupona, kwa sababu mtu akifa hawezi kufanya kazi. Wamefanya kazi kubwa sana kurekebisha vifungu na maneno na mistari mbalimbali na tulikuwa tumelalamikia kwamba, kwa mfano, unakuta ibara ya 66 unasoma, wanakwambia hii ilinganishe na ibara ya mia moja na kitu. Unakuta mia moja na kitu wanakwambia linganisha na ibara ya sita. Nimeona kidogo *cross relation* imepungua na hii napongeza kwa kweli wanasheria waliokuwa katika Kamati hii, kwa kweli wametumika kitaalam na Muswada sasa unakwenda sambamba na mambo ambayo yanatakiwa au aliyoeleza Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia katika hatua za kistaarabu, kwa Muswada wowote ule, wadau wanachangia kwa malengo ya maendeleo ya Muswada huo na matokeo yake huleta mafanikio. Wakati tulipopitisha Muswada wa *VAT* hapa, *TRA* ilikuja na maneno mazuri sana, walisema kwamba Muswada wa *VAT* ni kodi ambayo inajichunga yenyewe kwamba kwanza, inakwenda asilimia ishirini, tena inakwenda asilimia ishirini, kwa hiyo matokeo inajichunga yenyewe. Niliwaambia hivi kuna kitu kinajichunga chenyewe mbele ya binadamu, kuna kitu kinajilinda chenyewe kama nanasi ambalo lina miba kuanzia shina mpaka tunda lakini linaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima kuwepo na *proper supervision* ili kuweza kuona kwamba, kodi pamoja na kwamba, inajichunga yenyewe na kipengele hicho, lakini kuwepo na usimamizi mzuri na ndiyo maana kuna mapato yanayopatikana kupita yale malengo yanayowekwa na yale yanatokana na umahiri na usimamizi mzuri wa *TRA* katika ukusanyaji wake. Tuliona takwimu, tulishuhudia katika Bunge hili Tukufu wakati wa Bajeti na vile vile katika hatua mbalimbali za mahesabu na *balance sheet* yanayotolewa na *TRA* kwa mujibu wa kanuni za Bunge ndani ya Bunge hili. Tumeridhika na kazi zao.

Sasa Muswada wenyewe uliokuwa unasimamia hali hii ulikuwa umepitwa na wakati na ulikuwa niwa muda mrefu. Kama mafanikio hayo yameletwa na Muswada ule wa zamani sasa unarekebishwa, unatangaza unasema sasa nimevaa koti jipya. Anasema mimi ni nani, wanasema wewe ni mama yetu na *whitedent,* sasa mnavaa koti jipya, na sisi tunategemea kwamba mtafanikiwa zaidi ya hiki kiwango ambacho tunatekeleza. Nikasema kodi kwa kweli haipendwi katika nchi zote, nilikuja na kitabu cha *World Almanac* hapa kuangalia kama kuna nchi yoyote ambayo inasherehekea kodi, hiki hapa hakuna. Hakuna siku ya *holiday* ya kodi katika dunia kwa sababu haipendwi. Watu wanasherehekea magonjwa, Siku ya Kifua Kikuu Duniani, siku ya Malaria, kuna siku ya UKIMWI, lakini siku ya kodi haipo. Ipo *tax holiday* lakini hawasherehekei. Kwa hiyo, wanaosimamia mambo ya kodi kwa kweli ni *hundred percent risk* katika kazi zao. Lakini kutokana na uelewa na kuwaelewesha Watanzania walipa kodi kwa ujumla, wanayajua haya na ndiyo maana tunapata mafanikio haya. Hii inaitwa *close partnership* kati ya mlipa kodi na mdai kodi.

Marekebisho yale yaliyofanywa katika vifungu kama 35 hivi vilivyokuwa vimefutwa, vingine vimerekebishwa na vingine vimefanyiwa mabadiliko, nimekuta kuna kitu kimoja mimi siyo Mwanasheria, nataka nipate ufafanuzi kidogo kuhusu unapokwenda kwa mfano, kwenye ukurasa fulani, unakuta wanataja sheria fulani ya miaka ya nyuma ambayo inafanya *cross reference,* kwa mfano, ukurasa 103 wamesema kuna *Act 30 of 1997,* halafu mkasema *Act 5 of 1996,* sasa unakuta hizi zilizokuwa *quoted* ni *Act* au ni nini hizi? Nataka kupata ufafanuzi, kwa sababu najua maana ya *definition* ya *Act* haiwezi kuwa ya zamani kiasi hiki? Kwa sababu ni *Act* kama hii tuliyoisoma sasa ndiyo *Act*. Lakini zilizokuwa *quoted* kweli ni *Act* au ndiyo sheria za zamani? Kwa kuwa mimi siyo Mwanasheria naomba tu nipate ufafanuzi wa hayo.

Baada ya kusema hayo ni kwamba, yapo mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa kodi kama nilivyotangulia kusema katika hotuba yangu. Wenzetu katika nchi zilizoendelea kwa mfano, kuna kodi hata ya talaka *(Divorce Tax Expenses),* kuna 33 katika *World Almanac* inalipwa kwa kushabikia kabisa. Kama *Tax Driver* anapata mahali ana-*park* na anakula, kuna kodi ya *dollar* moja kule Marekani. Kuna *tax holding memo* ambayo hiyo inashughulikiwa kama mtu ana hundi halafu anai-*deposit* kwenye Hazina ya nchi ile basi anapoteza *dollar* moja. Wametamka kabisa *dollar* moja na wametaja kiasi na wazee zaidi ya miaka 69 mpaka 65 wanapoteza *dollar* moja kwa kila anayepata *dollar* 15,000 katika ukurasa huo huo. Kwa hiyo, lipo jedwali ambalo nitawapatia, linaonyesha jinsi walivyoweka vipengele, yote ni lengo la Serikali kukata pua kuunga wajihi ili nchi iende.

Ninachangia nchi, wakati mmoja niliwaambia kwamba, kuna kipindi fulani wakati bahari ililalamikia mito kwamba mito ilikuwa inakusanya maji yote. Tunalipa kodi tunapeleka Serikalini, halafu matokeo yake kuna pato la jumla na kuna kipato cha mtu mmoja mmoja, mafanikio ya mtu mmoja mmoja. Sasa mtu mmoja mmoja si lazima urudishwe fedha. Sasa ni hicho kituko cha mito yote duniani, ilisomba maji wakati wa mvua kupeleka baharini na bahari ikajaa, baadaye wakati mvua zimekwisha bahari haikulipa. Ikaandikwa barua kwa nini bahari unatuonea sisi hutulipi. Ikajibiwa ikawaambia tunalipa. Kwa sababu tunaweka jua linafyonza kwa yale maji, inaenda juu inanyesha mvua. Kwa hiyo, huu ni utaratibu wa kulipa.

Kwa hiyo, hayo Watanzania ile kodi inayochangiwa ambayo inapanuliwa wigo, mtapata mafanikio kutokana na njia mbalimbali za mafao na njia mbalimbali za nchi hii katika viwanda, wafanyakazi, taasisi mbalimbali, katika upande wa tiba, huduma mbadala ambazo mtazipata, ndiyo hiyo ambayo Serikali inaboresha hayo, mtapata majibu huko. Bahari ndiyo maana hailipi moja kwa moja kwenye mito kwa sababu ingelipa maji ya chumvi wakati imeletewa maji mazuri.

Kodi za gharama nafuu ziangaliwe kwa sababu isiwe katika kipindi cha mpito. Kuna utaratibu mwingine waelezwe kabisa kwamba, hiki ni kipindi cha mpito ili kodi zile zisikusanywe mbili, zikawa kodi za aina mbili zinakusanywa katika kipindi hiki cha mpito kama ilivyoelezwa.

Vilevile katika kipindi hiki cha mpito ambacho kimepita inaendelea kuanzia tarehe uliyotamka hapa, wasiendelee kukusanya kodi ambazo zimefutwa na Muswada huu. Kwa sababu kuna baadhi ya watendaji wenu wanapenda kukusanya kodi, ndiyo maana elimu imesisitizwa hapa katika kukusanya kodi na kuwaelimisha walipa kodi wote. Kwa sababu tunapanua wigo, sasa kuna wengine wigo huu unapopanuliwa wanadhani aina za kodi ni idadi ya walipa kodi.

Kwa hiyo basi, ongezeni wawekezaji waingie nchini ili idadi ya walipa kodi waliotajwa katika vifungu vilivyoelekezwa hapo wataongezeka ili wigo huo uongezeke. Tusifanye kama tulivyozoea. Tulisema kabisa mtu kama anapenda kuandikia kwa kutumia mkono wa kulia, basi ukimpa wa kushoto ataanza kushtuka. Kwa hiyo, hata wakusanyaji kodi wenyewe kwa mfumo huu watakuja kupata matatizo wakati wa kuanza kutekeleza sheria hii. Kwa hiyo, hima zinduka, Idara ya *TRA* kuwepo na mabadiliko ya haraka ili Muswada huu baada ya kupita na kuwekwa saini, sasa wabadilike katika kukusanya kodi kwa utaratibu ambao umepangwa kwa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye kuna mambo ambayo yataongezea tija. Nime-*quote* Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, wakati anatoa hotuba kule Mbeya wakati wa *May Day,* alisema kabisa kwamba: "Hakuna nchi yoyote inayokusanya kodi zaidi ya asilimia 50." Hakuna, hata ukiwa na ufanisi wa aina fulani, lazima yapo mapungufu, licha ya kwamba, hata wote wanasikwepe. Anayekwepa ni yule ambaye unamlenga, lakini wapo watu ambao hawakulengwa kabisa, kwa hiyo, hawawezi

kukwepa kwa sababu huwezi kukwepa kitu ambacho hujarushiwa. Kwa hiyo, wapo wengine hawatambuliki kama wanalipa kodi au hawajui kama kuna kodi za aina gani katika nchi hii, kwa hiyo, hawawezi kukwepa. Wanakwepa kwa *style* hiyo.

Upo utaratibu mwingine wa kukwepa, kwa mfano, mwekezaji anakuja, anafungua hoteli, anaiita Pawa Hoteli, ile *Tax Holiday* inapita anabadilisha jina, kwa hiyo mtu kama yule siyo mkwepaji, huyo ni mhujumu. Wanashtakiwa chini ya Sheria ya Uhujumu Uchumi watu kama hao. Au mtu alikuwa na kiwanda kilikuwa kinaitwa pengine Khanga ya Dodoma, halafu kinaungua kinahamia Dar es Salaam, unabadilisha hiyo Khanga ya Dodoma, sasa ni *Trade Mark* unaita Khanga ya Dodoma, lakini umekijenga Dar es Salaam. Huu nao ni uhuni katika kodi. Hatutaki watu wa uhuni wa aina hiyo. Kwa kweli kodi lazima iwe na utaratibu wa mvua kama ya radi, mara nyingi haichezwi na watoto. Mvua ikinyesha vizuri watoto wanacheza cheza kule na nini, lakini mvua ikiwa na radi angalau, lakini zinapunguzwa radi kwa walipa kodi ambao ni waaminifu na wanaojitokeza kufanya mahesabu yao vizuri, wale waenziwe ili wapate motisha ya kuendelea kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, nimesema kwamba, kodi haina sikukuu yoyote, huwezi kufanya sherehe hapa, hata Waheshimiwa Wabunge hatuna sikukuu ya kusherehekea kodi hapa. Kwa kweli pato la mtu ukiliingilia tu, yapo matatizo angalau atahoji hoji kidogo, utamkata lakini kwa shingo upande si kwa moyo mkunjufu. Ataunga mkono kuchukuliwa kodi yake lakini atafanyeje lazima achangie. Katika kuendeleza nchi lazima tuchangie na tutachangia na Muswada huu umekuja wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya hapo wale watoza kodi ambao siyo waaminifu, wanaofanya kazi katika Idara hizi, basi muwaangalie kwa macho ya husuda ili waweze kuondolewa, ili isije kuonekana mfumo mzima wa *TRA* watu wakauogopa. Iwe ni kimbilio kwenda kujisafisha kwamba mimi ninadaiwa shilingi 20,000/= ya kodi, asilimia kadhaa nakwenda kujisafisha *TRA* ili nilipe kodi badala ya kufuatwa. Kwa hiyo, kodi haisakwi, kodi inakusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa na mimi ni mara yangu ya kwanza, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili, ambao wamechaguliwa kuwa Marais katika nyadhifa mbalimbali. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, mtani wangu, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika. Naomba vilevile nimpongeze Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mwenyekiti wetu Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani. Pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mkutano wa Mawaziri wa Elimu katika Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwapongeza hao, naomba kuchangia katika Muswada huu kama ifuatavyo: -

Kwanza, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, ili kupunguza matatizo wanayopata walipa kodi ambao ni wachache, tunapaswa kutafuta mbinu ya kuongeza mapato na hii tutaifanya kwa kuangalia kwamba wote wanaopaswa kulipa kodi wanalipa kodi. Ni nani anayepaswa kulipa kodi, kwa hiyo elimu inahitajika kutolewa kwa wananchi ili waweze kujua ni akinanani wanapaswa kulipa kodi. Kwa hili nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuondoa utitiri wa kodi kwa wananchi ambao kwa kweli walikuwa hawapaswi kulipa kodi, lakini walikuwa wanalipa kodi. Hongera Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Pili, wananchi wawezeshwe kupata mapato. Ni kwamba, wananchi walio wengi wanapenda kufanya biashara lakini hawana uwezo wa kufanya biashara na kwa kuwa hawana uwezo wanaikosesha nchi mapato. Mwezi uliopita nilikuwa nchini Burundi, niliwakuta wananchi wanakopeshwa na mabenki yao bila kuwa na dhamana isiyohamishika. Wanakopeshwa kwa kudhaminiwa na biashara wanayofanya. Kwa hiyo, wanawake wa Burundi wanafanya biashara kubwa kubwa kama ya kuuza magari kwa sababu wanakopeshwa na benki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mabenki yetu yakiweza kuwasaidia wananchi hasa wanawake ambao wana kipato kidogo, nina imani wataweza kufanya biashara na hivyo kujiongezea kipato na vilevile kuweza kuiongezea nchi mapato kwa kulipa kodi. *( Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huu imependekezwa kwamba, mfanyabiashara au mtu yeyote aweze kujidhamini. Hii ni nzuri ikiwa wananchi watapata elimu ya uhasibu au elimu ya kuendesha biashara. Kwa sababu mimi ninakumbuka kuna wafanyabiashara ambao walipaswa kujidhamini wenyewe, lakini walipaswa wawe wana mhasibu ambaye anaweza kufanya makadirio yao. Mhasibu anapopeleka makadirio ya mfanyabiashara kule *Income Tax* wale wanaohusika wana-*reject* mahesabu hayo na sababu kubwa ilikuwa wanataka huyo mfanyabiashara aweze kuwahonga. Mfanyabiashara anapoleta mahesabu yake wana-*reject*, kwa hiyo mfanyabiashara anapaswa ayarudishe, anapoyarudisha na kuyafanya upya, mhasibu anamtaka amlipe fedha upya. Mwisho mfanyabiashara anachoka anaona kwanza atoe chochote wamkadirie kidogo kuliko kurudisha mahesabu kwa mhasibu ambaye anamlipa tena kila anapokadiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natoa ushauri kwamba, kujikadiria ni vizuri, lakini wafanyabiashara wafundishwe namna ya kuweza kujikadiria mapato hayo na vilevile watoza kodi waweze kuwa waaminifu na kukubali hayo makadirio watakayofanya wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee biashara ya mpakani. Ni kwamba, biashara ya mpakani inaiongezea Serikali mapato. Lakini kwa sababu kodi wanazolipa ni kubwa na ni nyingi kuweza kufanya biashara na nchi jirani, wafanyabiashara wa

mipakani wanaona ni heri kufanya biashara ya magendo. Ndiyo maana nilipokuwa kule Burundi, nilikuta bidhaa nyingi za Tanzania zikiuzwa Burundi lakini hazikwenda kihalali.

*(Hapa umeme ulikatika na kurudi baada ya dakika moja)*

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Kuna biashara kama ya chumvi, Magodoro ya Dodoma na bidhaa nyingine nyingi ambazo zinauzwa Burundi kimagendo. Kama biashara hizo zingekuwa zimewekewa kodi ambayo ni nafuu, wafanyabiashara wangeweza kuuza bidhaa hizo kihalali na hivyo kuipatia nchi mapato. Kwa hiyo, nashauri biashara ya mpakani iweze kupunguziwa kodi kusudi wafanyabiashara wafanye biashara kwa uhalali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mawazo mengi ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nayaunga mkono kwa sababu mengi ambayo wengi walikuwa wamejitayarisha kuyachangia kama vile kodi kwenye malipo ya uzeeni na kodi kwenye posho, yote yameondolewa. Kwa hiyo, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia machache katika hoja ya Muswada wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa mchango wangu, naomba nichukue fursa hii nimpongeze Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, Naibu Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Bwana Grey Mgonja, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Kamishna Mkuu wa *TRA,* pamoja na Watendaji Wakuu wao, kwa kuandaa Muswada huu na kujumuisha mawazo mbalimbali yaliyotolewa na wadau mbalimbali na kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, niwapongeze wadau wote waliochangia mawazo mbalimbali katika hoja hii iliyo mbele yetu. Wingi wa wadau hawa waliojitolea kushiriki kuchangia mawazo yao kwenye Muswada huu na wingi wa hoja na mawazo waliyotoa, inaonyesha dhahiri uzito na umuhimu wa Muswada huu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi, napenda nitamke kwamba, ninaunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi leo hii Sheria ya Kodi ya Mapato katika nchi yetu ni ile Namba 33 ya mwaka 1973, ambayo kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha

alivyoiainisha na kama sote tunavyojua, ilikuwa na mapungufu mengi ikiwemo kutokuwa na wigo mpana wa kujumuisha vyanzo mbalimbali vya mapato pamoja na kutodhibiti kikamilifu mianya ya kukwepa ulipaji wa kodi.

Muswada huu ulioletwa Bungeni umekusudia kupanua wigo wa kodi na kuziba mianya ya kukwepa kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie hili la kupanua wigo wa kodi. Ni dhahiri kama tulivyoelezwa katika Muswada huu kwamba, Muswada huu umejumuisha vyanzo mbalimbali vya mapato yakiwemo mapato yatokanayo na ajira, mapato yatokanayo na biashara na mapato yatokanayo na uwekezaji wa vitega uchumi. Hivyo basi, ni wazi kwamba, wigo wa kodi umepanuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba, katika upanuzi wa wigo wa kodi ni dhahiri kwamba, kuna shughuli nyingi ambazo zinafanywa na sekta isiyo rasmi. Vyanzo vyote hivi vilivyotajwa katika Muswada huu, vinajikita kwenye sekta rasmi ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shughuli kama nilivyosema nyingi na kubwa zinazofanywa na sekta isiyo rasmi na Muswada huu haukujumuisha katika wigo wa kodi. Ni vyema basi Serikali ifikirie na itafute njia ya kufuatilia shughuli za sekta isiyo rasmi ili hawa wote ambao wana vipato ambavyo vinapaswa kulipiwa kodi wajumuishwe kwenye sekta rasmi ili walipe kodi na hivyo basi kuongeza wigo wa kodi zaidi ambao tunatarajia hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kipengele cha kodi ya mapato yanayotokana na mapato ya wafanyakazi. Mapato ya wafanyakazi yamekuwa ndiyo eneo kuu la kutoza kodi na eneo hili lina kodi nyingi sana. Tunashukuru kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amelitilia hili maanani na ameondoa baadhi ya kodi ambazo zilikuwa kwenye Muswada wa mwanzo na sasa hivi imeleta unafuu kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema basi Serikali ikatazama kwa undani eneo hili. Kodi ambayo Serikali inatoza imekuwa ni mzigo mkubwa kwa wafanyakazi hasa wakati wa zama hizi za *cost sharing,* ambapo wafanyakazi nao wanashiriki katika kuchangia huduma za jamii kama vile elimu na afya. Ni vema basi Serikali ikatazama upya eneo hili kwa nia ya kupunguza viwango vya kutoza kodi na kuongeza kima cha kuanza kulipa kodi kwa wafanyakazi. Aidha, Serikali ijitahidi kuibua ajira ili tuwe na wafanyakazi wengi zaidi na tuweze kuongeza wigo wa kodi na ukusanyaji wa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie kipengele cha *Self Assessment.* Muswada huu umeweka bayana kipengele hiki cha *Self Assessment,* ambapo mlipa kodi anajikadiria mwenyewe kodi ambayo anapaswa kulipa. Jambo hili ni zuri maana kama Serikali ilivyosema, inaondoa manung’uniko yaliyopo kati ya walipa kodi na wanaotoza

kodi, kumekuwepo na malalamiko mengi sana huko nyuma na hiki kipengele cha *Self Assessment* cha utaratibu huu mpya kitaondoa malalamiko hayo katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili ningependa kushauri kwamba, ili utaratibu huu mpya ufanikiwe, ni vema Serikali ikahakikisha kwamba, walipa kodi wote watakaohusika na utaratibu huu, wanaelimishwa kuhusu utaratibu huu na madhara ambayo yatakuwepo kutokana na wao kutotimiza masharti ya utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la *Excess Liquidity,* Serikali imetueleza na tunashukuru kwamba, Serikali inafahamu kwamba, kuna *Excess Liquidity* katika mabenki na *Financial Institutions* zilizopo katika nchi yetu. *Liquidity* hii iliyopo kwenye mabenki ni bora ielekezwe kwenye maeneo ya uzalishaji. Sitaji kilimo kwa sababu mimi ni mkulima, lakini ni bora fedha hizi zielekezwe kwenye maeneo ya uzalishaji hasa kilimo ambacho sasa hivi kwa kweli hakina wawekezaji wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii ya kilimo ina watu wengi ambao wataweza kuwa walipa kodi wa kesho wakiwezeshwa kuzalisha. Ni watu wengi, karibu asilimia 85 ya wananchi wa Tanzania wako kwenye sekta hii na asilimia kubwa yao wanaweza kujiajiri wenyewe wakipata msukumo na wakiwezeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali iandae na ielekeze fedha hizi katika maeneo hayo ya uzalishaji ili tuweze kupanua wigo wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, kwa sababu mimi nilikuwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, naomba niseme kuwa, naunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji ni ndefu, lakini wengi wamesema wangependa kuchangia kesho ili wapate nafasi ya kujiandaa vizuri zaidi. Kwa hiyo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.27 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi Tarehe 22 Aprili, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*